**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Tano – Tarehe 5 Novemba, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa Mwaka 2016 *(The Media Service Bill, 2016)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, nirudie yale niliyosema jana jioni kabla ya kuahirisha kikao chetu. Tunao wachangiaji wawili wale waliobaki jana ili kukamilisha uwiano wetu halafu ndiyo tutaanza na mzunguko mwingine. Hata hivyo, kwa sababu ya muda mjadala huu tutaenda nao mpaka saa tano halafu Mheshimiwa Waziri atahitimisha hoja yake, watagawana na Mheshimiwa Naibu Waziri ile saa moja watakavyoona wenyewe *and then* tutaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima, kwenye shughuli yenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, *schedule of amendment* ambazo tumepokea ni ya Serikali na ya Mheshimiwa Waitara. Kwa sababu Muswada huu tumekuwa nao haitapendeza kuleta marekebisho kwa kuchelewa. Kama kuna Mheshimiwa Mbunge ana matamanio ya kufanya marekebisho afanye hivyo mapema. Ndiyo maana jana niliwaomba sana tujiandae ili asubuhi hii Katibu wa Bunge aweze kupokea mawazo ya kufanya marekebisho. Hatutaruhusu mtu kuleta marekebisho wakati wowote, itakuwa ni vurugu tu maana Serikali na wenyewe lazima wapewe fursa ya kuyaona marekebisho hayo na kuyatafakari,

lakini yakiletwa sasa hivi kule kwa Katibu maana yake hatuwezi kwenda zaidi ya kipindi hiki itakuwa imesaidia sana shughuli za Bunge.

Baada ya kusema hayo, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Hawa Ghasia atafuatiwa na Mheshimiwa Mbene.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye amenijalia afya na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuweza kuchangia Muswada huu wa masuala ya huduma za habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kuuingiza Muswada huu Bungeni baada ya zaidi ya miaka 20 pamoja na vikwazo mbalimbali ambavyo vimejitokeza. Kwa hiyo, nampongeza sana Waziri na Naibu wake pamoja na Maafisa wa Wizara yao kwa kazi kubwa sana ambayo wameifanya kuhakikisha Muswada huu unaingia ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nichukie fursa hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana na katika mazingira magumu. Pia niwapongeze wadau wa habari ambao kwa kweli wamekubali kutoa maoni yao na kuweza kwa kiasi kikubwa kuboresha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masuala ya kawaida Muswada kuandaliwa na Serikali na kuupeleka kwa wadau na kwenye Kamati. Lengo la Serikali kupeleka kwa wadau na kwenye Kamati ni kuhakikisha kwamba wadau wanatoa maoni yao, yale maeneo ambayo wanaona yana upungufu wanayazungumzia ili Serikali iweze kuyarekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la ajabu sana Muswada ambao umekaa zaidi ya miaka 20 mdau kila siku ukiambiwa unasema muda hautoshi. Hivi tunao Muswada wowote ambao umejadiliwa zaidi ya miaka 20 ndani ya Bunge hili? Ndiyo maana nawapongeza wale wadau ambao kwa kweli hawakukubali kuburuzwa na hao ambao wamekusudia kuwaburuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kufuta kifungu cha 50(4),(9),(10) na (11) ambavyo vilikuwa vinaruhusu polisi kuchukua mashine au mitambo iliyohusika katika kuandika habari ya uchochezi. Hii inaonesha kabisa kwamba Serikali na Waziri wametambua mabadiliko ya teknolojia. Kwa sababu katika mabadiliko ya sasa ya teknolojia, mmiliki wa mtambo anaweza akauweka mtambo wake *automatic* na mchapishaji akaandika taarifa yake akaleta *softcopy* kwa ajili tu

ya kuchapisha na mmiliki wa mitambo ule asiwe na nafasi ya kusoma lile chapisho mwanzo mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kumchanganya na yeye kwenye makosa kwa kweli naona haikuwa sahihi, lakini naipongeza Serikali yangu kwa kupokea maoni ya wadau na kuviondoa vipengele vyote vinavyohusiana na kuchukua mitambo ambayo imehusika katika kuandika chapisho lenye uchochezi au ambalo kwa kweli linaleta madhara kwa baadhi ya wananchi. Hiyo yote imetokana na mapendekezo ya wadau, Kamati na usikivu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kabisa kwamba Muswada huu ni mzuri na unalenga kuboresha tasnia hii ya habari. Pia unalenga kulinda haki na wajibu wa vyombo vya habari. Hakuna haki isiyokuwa na ukomo, lazima tasnia kama hii ipewe haki, lakini pia ipewe ukomo na mipaka, ihakikishe haki hiyo wanaitumia vizuri bila kuathiri usalama wa nchi, bila kudhuru wengine na bila kukashfu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa Tanzania ni mashahidi, Rwanda imeingia katika machafuko na miongoni mwa sababu ni pamoja na uchochezi wa vyombo vya habari. Ndiyo maana mmiliki mmoja wa vyombo vya habari ni miongoni mwa waliohukumiwa kufungwa. Kwa hiyo, tasnia hii hatuwezi tukaicha tu ielee yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kwa kiasi kikubwa, ndiyo maana naipongeza Serikali yangu, unalenga kuwatetea na kuwasaidia waandishi wa habari. Ukiangalia katika kifungu cha 21 Muswada unaanzisha Mfuko wa Mafunzo ya Habari. Sasa kama Muswada unaanzisha Mfuko kwa ajili ya kumwendeleza mwandishi wa habari na tasnia ya habari, hivi unasimamaje mwanasiasa mwenzangu ukasema kwamba Muswada huu unakusudia kuua sekta ya habari au uhuru wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 10 cha Muswada huu inaanzishwa Bodi ya Ithibati ya Wanahabari. Katika kifungu cha 12 kazi za bodi hiyo zimeainishwa ambapo mojawapo ni kutoa ithibati kwa wanahabari, kusimamia kanuni na maadili za nidhamu miongoni mwa wanahabari na kusimamia viwango. Haya ni mambo ya kawaida kwenye taaluma mbalimbali. Hatujaanza na taaluma/tasnia ya habari kwani Bunge hili hili limeshapitisha kuwa na bodi kama hizi kwa Wahasibu (*NBAA),* tunayo Bodi ya Wahandisi, Bodi ya Wakadiriaji Majengo, Chombo cha Wanasheria, Baraza la Madaktari, Mafamasia, Wauguzi, Wakemia, hiyo ni mifano michache tu. Sasa kama taaluma nyingine zinasimamiwa kwa nini taaluma hii nayo isisimamiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipingane na wale wenzangu wanaosema kwamba enzi hizo mtu alikuwa anaajiriwa kuwa mwandishi wa habari bila hata kusomea. Hivi jamani hii nchi baada ya miaka 50 bado tunataka tuendelee kuajiri bila kusomea, yaani mtu atoke chuoni leo aende akawe Mkurugenzi wa Habari Maelezo au mtu bila kusomea hata kidato cha sita hajafika unataka na yeye awe mwandishi wa habari bila cheti, kwa kweli hapana. Ni lazima tuzingatie viwango, lazima tuweke viwango, lazima tuondokane na makanjanja na lazima tuwape heshima wale ambao wamepoteza muda, rasilimali zao kwa ajili ya kujiendeleza katika tasnia hii ya habari, uwatofautishe na wale wanaoandika kwa mazoea tu, lazima tuweke madaraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukienda katika utumishi wa umma Serikali ilikuwa inaajiri darasa la saba, *form four* ambaye hana cheti hana chochote hata mimi mwenyewe nimeanza kazi mwaka 1992, *fresh from school, form six* nikaajiriwa kama *PCA (Planning and Controller Assistant)* cheo hicho hakipo. Kwa hiyo, tusilazimishe mambo ya miaka 20 leo tuendelee kuwa na watu wa aina hiyo. Enzi hizo wakati watu wanatoka Makerere Tanzania hatukuwa na Chuo cha Uandishi wa Habari hata kimoja chenye kutoa digrii, sasa hivi vimejaa, wasomi wamejaa bado tuendelee na watu wa darasa la saba kuwaita waandishi wa habari? Kwa kweli ni kuidhalilisha tasnia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Muswada huu narudia tena kusema kwamba una lengo la kuwasaidia waandishi wa habari. Katika kifungu cha 58 kinataka kila mwajiri kuweka bima na hifadhi ya jamii kwa kila mtu aliyeajiriwa katika chombo cha habari husika. Wenyewe ni mashahidi, tunao waandishi wetu wa habari wengine wanafikia mpaka kufariki amefanya kazi kwenye chombo zaidi ya miaka sita hana ajira, bima na hajalipiwa kwenye Mfuko wowote wa Hifadhi ya Jamii. Tunao waandishi wa habari wanapata ajali hawana hata bima, hawawezi hata kutibiwa, wengine mpaka wanapata ulemavu wa kudumu hakuna hata bima ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli napenda niipongeze Serikali yangu kwa kuliona hili na kuja na sheria inayowatetea waandishi wa habari. Kwa sababu ukisema awekewe bima na alipiwe hifadhi ya jamii ndiyo moja kwa moja unamaanisha kwamba huyu ni lazima atakuwa na mkataba unaoeleweka, unaomwezesha kulipwa mshahara unaojulikana na sehemu ya huo mshahara ukamlipie kwenye Hifadhi ya Mifuko ya Jamii. Kwa kweli nashangaa kusikia kwamba eti kwa kuwa na hiyo bima na kulipiwa hifadhi ya jamii unanyanyasa, unadidimiza sekta ya habari. Waswahili wanasema ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu katika kifungu cha 21 kama ambavyo nilisema kinaanzisha Mfuko wa Mafunzo ya Wanahabari ambao utaweza kutoa mafunzo kwa wanataaluma ya habari, kukuza programu za uendelezaji maudhui ya ndani ya nchi na kukuza na kuchangia utafiti wa maendeleo katika nyanja za habari na mawasiliano ya umma. Hivi Mwenyezi Mungu awape nini wanahabari? Mie kwa kweli nasema huu Muswada kwanza hatukutakiwa hata tuujadili kwa siku mbili, tungeweza kuujadili kwa siku moja, tukaumaliza ili wenzetu wanahabari nao wajione wako sawa na wanataaluma wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilishangaa sana namsikia mwanahabari anasema eti mnatutaka tuvae suti wakati tunaenda kuandika habari. Ndugu zanguni huu Muswada tunavyoandika au tunavyopitisha sheria lazima tuangalie na sheria nyingine za Kimataifa zinasemaje? Sisi kama nchi tunayo makubaliano mbalimbali ambayo tumeingia na mojawapo ni makubaliano ya Mkataba wa Geneva wa kuwalinda raia na waandishi wa habari katika operesheni mbalimbali au katika maeneo ya vita. Sasa utalindwaje kama hutofautiani na watu wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuvaa mavazi rasmi katika maeneo maalum ni kwa lengo la kuwalinda wanahabari wenyewe. Usiangalie leo unaandika katika mazingira ya amani, unaweza ukapelekwa Sudan huko ukafanye *coverage*, lakini kwa vile umeshazoea huku kwenu hakuna kuvaa *uniform* eneo lolote hata katika mazingira magumu utafika kule utachekesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili linalenga kuwalinda wenyewe waandishi wa habari katika mazingira maalum. Kwenye operesheni za polisi, kijeshi hivi wewe usipovaa vazi rasmi la kukutofautisha, siyo kwamba kila siku uwe umevaa hiyo sare lakini katika mazingira maalum, Serikali ina wajibu wa kukulinda mwandishi wa habari usidhurike. Sasa itakulindaje kama haiwezi kukutofautisha na vibaka wengine na wale ambao wamekusudiwa kwenda kufanya operesheni. Kwa hiyo, ili iweze kukutofautisha na wengine na iweze kukulinda ni lazima ikuweke katika vazi linalokutofautisha. Tunaposema vazi siyo lazima iwe *uniform* chini juu hata ukivaa *reflector* ni vazi maalum. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Eeh!

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Kamati yake pamoja na Uongozi wote wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo kwa kweli niliona nilizungumzie ni kwamba, kwa mtazamo wangu, Muswada huu unampunguzia sana Waziri mamlaka kuliko ambavyo watu wanafikiri. Kwa sababu zamani Waziri mwenyewe alikuwa anaweza kufungia magazeti, chombo cha habari, lakini kwa Muswada huu masuala karibu yote ya kitaaluma yatapelekwa kwenye bodi na Waziri atabaki na masuala machache tu yanayohusiana na uchochezi, amani au usalama wa nchi. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba Muswada huu unakusudia kukandamiza tasnia ya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe tu wenzetu, kama kweli tumekuja hapa kuwatetea wananchi wanyonge tuungane kuhakikisha kwamba Muswada huu unapita kwa sababu unawalinda sana waandishi wa habari. Hata hivyo, kama nyuma ya pazia kuna mtu ametutuma kuja kumtetea ili hao waandishi wa habari wasiolipwa mishahara, wasiokuwa na mikataba, wasiolipiwa bima waendelee kunyanyaswa, hebu mkae ninyi wenyewe mzungumze ndani ya nafsi yenu, mumwogope Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mmh!

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Haiwezekani mtu awe na chombo cha habari, ameajiri watu hawana mshahara, hawana bima…

**MBUNGE FULANI:** Mikataba.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Anawalipa anavyotaka yeye…

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *(Hakutumia kipaza sauti)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Kwa kweli huo siyo uhuru wa habari tunaoutaka…

**MBUNGE FULANI:** Ni ukandamizaji.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Tunataka uhuru ambao pia unajali maslahi ya wale wanaoleta habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sugu hata kama inauma vumilia, hata kama sindano imeingia imekuchoma vumilia ndiyo uanaume. Watakaposimama wanaume wenzako utafanyaje kama dada yako tu akisimama unatapatapa hivyo, mwanasiasa lazima uwe na ngozi ngumu, uwe na uwezo wa kusikiliza wenzako. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ukiona mtu anapiga kelele ujue tayari imemgusa huyo na sindano imeingia. Ndiyo maana Chama cha Mapinduzi, chama kikomavu, mnazungumza, tunawasikiliza na tunagusa vifungu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *(Hakutumia kipaza sauti)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Ni kwa sababu tumesimama hapa kutetea wanyonge, waandishi wa habari lakini wengine hapa wanachofanya ni kuwaonyesha waliowatuma kwamba nilizungumza. Sisi tunawawakilisha wananchi, wanyonge, tusimame na tuzungumze kwa niaba ya wanyonge, tuache kutumiwa na matajiri wachache wenye vyombo vya habari ambao wanataka kuendelea kukandamiza waandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naona yanatosha, yamewaingia, wameelewa na nina imani Serikali yangu yale inayohitaji kuyafanyia kazi yamechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Janet Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali asubuhi ya leo na kunipa pumzi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Habari, Naibu Waziri na timu yake nzima. Napenda kuwapongeza sana Mwenyekiti wa Kamati husika pamoja na wajumbe wote wa Kamati ile. Napenda vilevile kuwashukuru wachangiaji wote wenye nia njema ambao wametoa michango mizuri sana ambayo inaenda kuboresha Muswada huu. Aidha, nataka kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo wamekuwa wasikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeelezwa hapa kuwa huu ni Muswada ambao umechukua muda mrefu sana kuletwa Bungeni, naamini huu ni wakati muafaka kwa Muswada huu kuja hapa. Naamini kuwa haya ni majira na nyakati sahihi kwa huu Muswada kufika hapa kwa sababu umepata nafasi ya kupitiwa na michango imetolewa mingi sana na tunaona jinsi ambavyo imeendelea kuboreshwa siku hadi siku, mwaka hadi mwaka hadi hivi leo tunaendelea kuujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niipongeze Serikali kwa sababu tayari kuanzia michango ilivyoanza kutolewa wamekuwa wakirekebisha yale maeneo ambayo yalikuwa yanaleta ukakasi katika Muswada wetu. Nataka kuamini sana kuwa Serikali yetu inaleta Muswada huu kwa nia njema kama ambavyo imekuwa ikifanya muda wote. Nataka kuamini sana kuwa Muswada huu umeletwa kwa nia njema ya kuhifadhi maslahi ya wanaotumikia tasnia hii ya habari hasa waandishi wenyewe lakini hata vyombo kuhakikisha kuwa vinawatendea haki watumishi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana mambo mengi sana yaliibuliwa humu ndani ambayo yanasemekana kuwa ni historia na tulikuwa tunataka kuaminishwa kuwa tuendelee na historia ile kitu ambacho hakiwezekani kwa sababu dunia hii haijasimama pamoja. Tunaendelea na kila siku maendeleo mapya yanataka hatua tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia nchi nyingi ambazo zimekuwa na sheria kama hizi na hata kama zilikuja kubadilishwa lakini zilibadilishwa kufuatana na mazingira yanavyoibuka. Hizo nchi zinazoambiwa zimeendelea sana, nazungumzia nchi kama Norway ambao wao pia huko nyuma wamekuwa na Miswada kama hii, wameenda wakiibadili kufuatana na hali halisi ya uchumi na maendeleo ya teknolojia. Hata sisi kwa kuleta Muswada huu leo tunaangalia hali halisi ya mazingira waliyonayo waandishi wetu na katika tasnia nzima hii ya habari. Katika tasnia hii hakuna udhibiti wa aina yoyote, hakuna mpangilio wa aina yoyote, kila mtu anaendesha tasnia hii kwa jinsi anavyoona inamfaa yeye kwa maslahi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kutokana na hali hiyo kuna wanaoumia na ndiyo maana Serikali imeona kuna umuhimu sasa kutokana na malalamiko ya hao hao wanaoumia kuona kuwa taaluma hii ichukuliwe kama taaluma nyingine yoyote. Kwa hali hiyo iwekewe utaratibu mzuri utakaohakikisha kuwa wanaohusika wanapata haki lakini vile vile Taifa halikoseshwi haki zake za msingi za kujieleza na vyombo husika havitumii nguvu yao ya kifedha kukandamiza wale ambao wanawatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikumbushe tu kuwa Marekani sasa hivi wao waliondoa mfumo wa kuwa na sheria ya kudhibiti habari, lakini badala yake wameweka sheria za kudhibiti ushindani ambazo vilevile zinahakikisha kuwa ushindani wa haki unafanyika katika kila taaluma na kila sekta. Hii ni kwa sababu inatambulika kuwa tasnia ya habari ina mchango mkubwa sana katika kushawishi sera za nchi, biashara na ushindani. Inaonekana kuwa kama watu matajiri, makampuni makubwa yakiachiwa wao kuendesha ushindani wanavyotaka wale wadogo watashindwa kumudu ushindani huo. Kwa hiyo, Serikali imeingiza sheria ambazo zinaleta ushindani bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatujafika mahali ambapo ushindani wa kibiashara au wa kiuchumi upo sawa kwa sababu bado nchi yetu inakua kiuchumi. Kwa hali hiyo, lazima hapa katikati kuwe na utaratibu wa kuhakikisha kuwa tasnia hii ya habari haitumiki vibaya. Tayari tumeshaona mifano, kuna watu wameingia humu ndani wote wanaimba *chorus* moja, hii moja kwa moja inaashiria kuwa kuna mahali wamepewa hiyo *chorus* waje waiimbe humu ndani. Hiyo tayari inaonekana jinsi ambavyo tasnia hii inaweza ikatumika kushawishi vibaya na inataka sasa kushawishi mpaka hata huu Muswada uende vile wanavyotaka wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kabisa kuwa hii sheria imechelewa kuletwa kwa sababu kila mara kulikuwa kuna upinzani unaozuia isiletwe na ukichukuza upinzani huo ni kwa wale wenye vyombo vya habari sio waandishi, sio watumishi. Sasa hii inaonekana dhahiri tayari kuna utumiaji mbaya wa madaraka yao ya kiuchumi kutaka kukandamiza wengine kwa manufaa yao. Sasa Serikali imeona umuhimu huo kuwa sasa hivi lazima wale wanaotumikia tasnia hii wafanye kazi kwa utaratibu ambao unakubalika bila kuathiri uhuru wa vyombo vya habari, bila kuathiri watu wanaotaka kujieleza na kutoa maoni yao katika Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali kuwa maana nzima ya kuleta udhibiti katika tasnia hii kwanza ni kuhakikisha kuwa maslahi ya Taifa yanaliandwa lakini vilevile ni kuhakikisha kuwa tunapanua vigo wa ushindani, kuhakikisha kuwa kunawekwa viwango vya taaluma hii. Mengi yameshazungumzwa kuwa taaluma hii kwa kweli haikuwa inazingatiwa, waandishi walikuwa wanajiendea vyovyote vile, wameitwa majina mabaya sana kwa sababu tu ni kweli walikuwa hawatambuliki. Sasa kama tupo tayari kuweka viwango, kama tupo tayari kuhakikisha kuwa haki zao zinalindwa, kama tupo tayari kuhakikisha kuwa ushindani unakuwa sawa katika vyombo vya habari kuna ubaya gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa maslahi ya Taifa sasa hivi lazima yazingatiwe kutokana na maendeleo ya teknolojia. Tunaona jinsi ambavyo vyombo vinatumika vibaya katika kueneza taarifa za uongo au za uchochezi au hata za kuharibia watu majina. Wote humu ndani kwa njia moja ama nyingine tumeguswa na haya mambo ya watu wanavyotuma taarifa ambazo sio za kweli, watu wanaunganisha mpaka picha anaonekana mtu kweli lakini sio yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vitu kama hivi hatuwezi kuendelea kuviachia na kwa kufanya hivyo tutakuwa sisi wenyewe hatujitendei haki. Tunakubali kuwa kuna haja ya kuwa na uhuru wa kujieleza na hiyo imewekwa wazi na mapendekezo ambayo yanaletwa sasa hivi ya kufanya *amendment* kwenye huu Muswada yote yameangalia mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuzuia kutangaza vitu ambavyo sio vya kimaadili hivyo ni vitu vinazingatiwa hata na nchi zilizoendelea. Nataka niwakumbushe tu mfano ambao sio mzuri sana kwetu sisi wanawake lakini ni kitu kilichotokea. Marekani kuna msanii mmoja maarufu anaitwa Janet Jackson alikuwa ana-*perfom,* bahati mbaya nguo ikadondoka upande mmoja wa mwili wake ukaonekana watu wakairusha, ikaonekana kuwa ile ilikuwa ni makosa na waliofanya hivyo walitozwa faini kwa kufanya hivyo. Sasa bila kuwa na sheria utamtoza faini mtu wapi? Kwa hiyo, vitu vingine tukubali kuwa lazima viwepo. Tunachotaka kusisitiza hapa ni uhuru wa habari usiminywe na hii imezingatiwa jamani, angalieni *amendment* zilizoletwa zimeangalia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la *sedition* au uchochezi ambao unaweza ukaleta machafuko. Ndugu zangu, Serikali imekubali kuleta *amendment* kuhusiana na suala hili na tayari mmeshaanza kuona kuwa zile adhabu ambazo zilikuwa zimewekwa za kijumla ambazo zinajumlisha aliyechapisha au aliyeandika zimeondolewa, atalengwa mhusika peke yake. Hii ndiyo maana nzima ya Serikali sikivu imeona kwa kweli hakuna sababu ya kutomtendea haki mtu ambaye yeye hahusiki na kosa sasa inaenda kumwadhibu mwenye kosa peke yake. Vilevile lazima tukubali kuwa Serikali inabidi isimamie na iingilie pale inapoona kuwa kuna ukiukwaji wa haki au usalama wa nchi, sasa hiyo haiwezekani bila kuwa na Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu maoni mengi yametolewa na ni mazuri sana na Serikali bahati nzuri inaenda kuyafanyia kazi. Sisi tutaendelea kutetea…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tumemaliza ile *round* ya jana tunaendelea na *round* ya pili. Mtanivumilia, ili tuweze kuendesha shughuli zetu vizuri mtaona sasa tunatenda haki lakini siyo kwamba tunaminya Kanuni tunataka tuwatendee haki, tukipunguza ziwe dakika 10 tunaongeza wachangiaji kidogo, nadhani mnalikubali hilo, limekaa vizuri kwa sababu ya haki. Sasa tunaendelea na wachangiaji wetu wanaofuata ni Mheshimiwa Abdallah Chikota atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Mmasi na Mheshimiwa Peter Lijualikali ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Nape na Naibu Waziri Mheshimiwa Wambura kwa jitihada zao ambazo zimewezesha leo kuwasilisha Muswada huu ambao umechukua takriban miaka 20, bado unasuasua tu. Kwa hiyo, nawapa pongezi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue nafasi hii pia kuwapongeza watendaji wa Wizara ambao kwa njia moja au nyingine wameshiriki katika maandalizi ya Muswada huu. Kipekee nimshukuru na nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ambayo amechambua Muswada huu. Kulikuwa na maneno mengi kwamba Serukamba sasa amekuwa upande wa Serikali lakini alisimama imara kuhakikisha kwamba kazi ya Kamati inatekelezwa na hatimaye kuja na maoni na mapendekezo ambayo yatasaidia sisi Wabunge kupitisha Muswada huu. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hofu nyingi sana na maneno ya upotoshwaji ambayo yalienea mitaani. Kuna watu walikuwa wanasema kwamba ukikutwa na kipande cha gazeti tu ambacho kina habari za uchochezi basi wewe umetenda kosa kitu ambacho Muswada hausemi hivyo. Watu wengine walikuwa wanaeneza kwamba Muswada huu haufafanui maana ya mwandishi wa habari kinyume na maelezo ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kabisa kuna ufafanuzi kwamba nani mwandishi wa habari na nini kitafanyika ili mwandishi wa habari aweze kuthibitishwa. Vilevile kuna upotoshwaji ambao ulienezwa kwamba *TV* zote kuna muda zitaambiwa kwamba zitangaze habari za Serikali ukiupitia Muswada huu mpaka mwisho kitu kama hicho hakipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandishi wa habari sasa unataka kuwa taaluma kama ilivyo taaluma nyingine, kwa hiyo, lazima uwekewe *professional code of conduct*. *Profession* zote zimewekewa *standards* kwa nini uandishi wa habari uachwe hivi hivi? Ukiangalia kifungu cha 10 cha Muswada huu kinaeleza wazi kabisa kwamba nini kinaanzishwa kwamba kutaundwa Bodi ya Ithibati. Hizi bodi kama walivyosema waliotangulia siyo kitu kipya, *profession* zote ualimu, uhandisi, udaktari, kuna kitu kama hicho na hata kada kama hizo kuna *register* na ndio maana wanasema kutakuwa na orodha ya wanahabari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *profession* ya ualimu kwa sababu mimi ni Mwalimu licha ya kuhitimu kwenye vyuo vyako unaandikisha na unapewa namba, wale Walimu wenzangu wanafahamu kuna *TSD* namba, unaorodheshwa na unapewa namba, kila Mwalimu ana namba yake. Kwa

hiyo, ndiyo kama orodha hii itatumika kwa wanahabari kwamba lazima tuwe na orodha ya wanahabari. Kwa hiyo, sio kitu cha kusema kwamba wanahabari wananyanyaswa, wanahabari sasa wanathaminiwa kwa sababu watakuwa na orodha yao ambayo itatambuliwa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18 kinaeleza wazi majukumu ya bodi na ukisoma kifungu kidogo cha kwanza unaona kabisa kwamba sasa waandishi wa habari sio kila mtu atakuwa mwandishi wa habari. Anasema mtu hataruhusiwa kufanya kazi ya uandishi wa habari isipokuwa kama mtu huyo amethibitishwa na sheria hii. Kwa hiyo, siyo kila mtu akiamka asubuhi atakuwa mwandishi wa habari na hii itasaidia sana kujua kwamba nani mwandishi wa habari na nani amerukia gari ya uandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tuupitishe Muswada huu ili hata sisi tutakapofanya shughuli zetu tujue kwamba tunaofanya nao kazi ni waandishi wa habari, kuna wengine wanachafua hii *profession* ya uandishi wa habari kwa sababu wao sio wanataaluma ya uandishi wa habari lakini wameingia tu kwenye uandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wanasema kwamba atakuwa amethibitishwa na imeelezwa wazi tu kwamba atakuwa amethibitishwa na bodi na kwa utaratibu ambao utaainishwa na kanuni. Sasa kuna watu wanalalamika kwamba Waziri ana mamlaka makubwa sana, hakuna sheria ambayo haimpi Waziri mwenye dhamana ya hiyo sekta kuandaa kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapo lazima Waziri aandae kanuni ambayo itasaidia kuandikisha hao waandishi wa habari. Hayo sio madaraka makubwa ya Waziri ni kuhakikisha kwamba ana dhamana katika sekta hiyo na anasimamia vizuri kwa sababu tusiseme tu kwamba hapa Mheshimiwa Nape atakuwa Mhariri Mkuu hapana, ni Waziri mwenye dhamana leo yupo Mheshimiwa Nape kesho atakuja mwingine kwa hiyo tusi-*personalize* hiki kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Muswada unatekeleza matakwa ya Sera yetu ya Habari ya mwaka 2003 ambayo inatamka wazi kabisa na inaitaka Serikali kuanzisha chombo huru kitakachosimamia masuala ya habari. Huu mwaka 2016 miaka takriban 13 sera imetamka hivyo na sisi bado hatujaunda, sheria hii sasa inaunda Baraza la Habari. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwamba mfupa ambao umeshindikana huko nyuma ameweza sasa kutekeleza sera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kuna watu walisema waandishi wa habari ni *passion* lakini hayo maneno siku za nyuma yalisemwa na watu wengine kwamba ualimu ni wito na Walimu sasa hivi wanakataa wanasema ni *profession* kama zilivyo *profession* nyingine. Uandishi wa habari ni *profession* na kila *profession* kuna *profession code of conduct,* kwa hiyo, tuache uandishi wa habari kuwa *profession*. Unakuwa na *profession code of conduct* halafu ndiyo inafuata *passion* lakini huwezi ukaanza na *passion* ukasema kusiwe na *profession code of conduct. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uki-*check* ukurasa wa 14 wa hotuba hii ya Kambi ya Upinzani inasema Serikali imeamua sasa kuja na aina ya waandishi wa habari ambayo inawataka. Jamani ku-*define* kwamba mwandishi wa habari awe na sifa hizi sio matakwa ya Serikali ni wakati wa sasa hatuwezi kuwa na watu ambao hawajawa *defined* kwamba mwandishi wa habari awe na sifa gani ya elimu na hiyo ni *standard* za kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, si kweli kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inataka kuleta waandishi wa habari ambao inawataka, ni matakwa ya mabadiliko ya dunia lazima tuseme kwamba mwandishi wa habari *minimum qualification* ya elimu iwe kiasi gani. Kwa hiyo, hapa tuna-*set standard* na hiyo siyo ya CCM ni suala la wakati wa sasa na mabadiliko ya kidunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu naunga mkono hoja na Mheshimiwa Waziri nikushauri tu kwamba sheria hii ambayo tutaipitisha muda siyo mrefu basi usichukue muda mrefu kutoa kanuni zake ili iweze kutekelezwa kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Mmasi atafuatiwa na Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye Bunge lako hili Tukufu. Kwanza kabisa naomba niseme kwamba naunga mkono hoja iliyoletwa mezani na kama tulivyoagizwa jana kwamba itakapofika pale haitalala itasainiwa hebu tuitendee kazi fursa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kuanza kueleza wenzangu kwamba Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwanza haijafilisika. Kwa nini nasema hivyo? Mkononi kwangu nimeshika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mheshimiwa Nape Nnauye naye alikuwa ni mmoja mshiriki katika kutengeneza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisoma ukurasa wa 216, aya ya 157, nitawasomea taratibu ili tuendelee ku-*cement* msimamo wetu kwa nini tunaona kwamba Muswada huu una tija kwa Watanzania walionyimwa fursa katika tasnia ya habari. Aya ya 157 inasema, ili kuendeleza tasnia ya habari na uhuru wa vyombo vya habari katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii 2015-2020 chama kitaielekeza Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya uhuru wa vyombo vya habari na kufanya yafuatayo:-

Kipengele cha kwanza kinasema, kuharakisha mchakato wa kupitisha na kuanza kutekeleza Sheria ya Uhuru wa Vyombo vya Habari. Tunayo sheria hii na tutaitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia imeendelea kusema hivi, kuimarisha uwezo wa Idara ya Habari Maelezo kama Msemaji Mkuu wa Serikali. Tunayo Idara ya Maelezo, naomba mrejee *Part III,* kipengele cha 4 na cha 5. Tunaye Mkurugenzi wa Habari Maelezo na hiyo ndiyo tunamaanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 216, aya ya 157, kipengele (e) kinasema, kuanzisha Mfuko na kuwaendeleza wanahabari kitaaluma. Hii tunapata *Part III,* aya ya 21 pale utasoma *Media Training Fund,* haya yote yanapatikana huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele (f) kinasema, kuhakikisha kwamba kunakuwepo na uhuru wa vyombo vya habari ili vitekeleze wajibu wake inavyopaswa kwa mujibu wa sheria. Napenda warejee *Part IV, section* ya 24 - 25 ambayo imeongelea *Independent Media Council.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niwaweke wenzangu vizuri, unajua bahati mbaya sana wakati Chama cha Mapinduzi kinakaa kutengeneza Ilani na miongozo ya nchi hii ili kuleta heshima katika mifumo yote ya Serikali wenzetu walikaa na kutengeneza Ilani yao kufikiri ama kujielekeza kwenye kufufua wafu, lakini Chama cha Mapinduzi hakikujielekeza huko, tulikaa katika kutunga miongozo ambayo tunaiweka ndani ya mifumo ili nchi yetu iweze kupata heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasiasa wenzangu tumekuwa hodari sana na mahiri sana ku-*point fingers* kwa nchi zilizoendelea mathalani Kenya, ona Wakenya wamefanya hivi lakini bila kufunga mikanda, bila kupita kwenye *transition* kama hizi, bila kuweka mifumo hivi tunafikaje huko wenzetu walikofika? Hivi tunahitaji nini katika hili? Tunahitaji *binoculars* kuona haya, mbona tunahitaji macho ya kwenye miili yetu kuona haya. Inasikitisha sana na hili ni jambo la aibu. Pia sishangai kaka yangu Mheshimiwa Sugu ulikuwa na haki ya kuja na maneno kama yale na ngonjera kama zile, angekuwa ndugu yangu Mheshimiwa Semesi Sware tungekana urafiki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Muswada huu ni mzuri, tumeongea pale kwamba tunahitaji kutengeneza ajira ambayo italeta heshima kwa Mtanzania. Pia tunahitaji kulinda ajira hizi na ndiyo maana tukasema tunahitaji ku-*secure* ajira za mwanahabari tuwe na mikataba. Pia tukaenda mbali tukasema hata hisa Mtanzania aweze kumiliki hisa kiwango cha 57%. Sasa wewe unakuja unamtetea Mzungu ambaye huja-*share* naye utaifa, ambaye huja-*share* naye dini, ambaye hata ukipata upungufu wa damu hawezi kukupa damu yake, tunahitaji nini ndugu zangu hebu tumwogope Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishika vitabu paletukaapa tukumbuke viapo vyetu tulisema tunakuja kutumikia nchi yetu ya Tanzania. Mnataka kupotosha umma kwa kuwa tu tumepita kwenye siasa zenye ngonjera nyingi zisizokuwa na vitendo. Kipindi kimefika siasa ni lazima ziende kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwenda haraka haraka kwa sababu muda haupo. Nikienda *section 7* na hiki kipengele tumepigiwa sana makelele, kwenye *obligation of the media houses* na ilikuwa inajikita kuongelea *obligation especially* kwenye upande wa *private media house*. Kifungu cha 7(1)(b)(iv) kinasema:-

*"To broadcast or publish news or issues of national importance as the Government may direct"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Mheshimiwa Nape Nnauye hiki kipengele kinatutendea haki na usibabaike wala isitokee unasitisha msimamo huu wala isitokee unafanya *amendment* katika mlango huu. Mlango huu ni mlango ambao utatunza amani ya nchi yetu, lakini pia ni mlango ambao utafunga kila aina ya pesa chafu zilizokuwa zinapitia katika mlango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwape mfano, mimi pamoja na wenzangu kwenye Bunge hili hili tulipata ridhaa ya kusafiri na kwenda nchi ya South Afrika na Mheshimiwa Ally Saleh pale akirudi atakuwa shahidi itaingia kwenye *Hansard* aje ani-*prove* mimi kwamba naongea uongo hapa. Nahitaji Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aliweke hili katika *regulations* na atoe maelekezo sahihi kabisa bila kupindisha ni mambo yapi ambayo yatapaswa kutangazwa ama kuwa *published* kwenye *private media house* na ni mambo gani ambayo hayapaswi kutangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokwenda South Africa ndugu zangu baadhi watakumbuka haya akiwepo kaka yangu Mheshimiwa Zedi pale, tulilipiwa *business class*. Tumeenda kule kama Wabunge wenye dhamana ya kuongoza wananchi tunaenda kuambiwa tuje ku-*promote lesbianism and gayism, bisexual transgender* na tulisafiri na mwandishi wa habari ambaye ametoka kwenye *private media house*. Vitu hivi ni vya kusikitisha, vya kudhalilisha,

tunapewa mizigo kuja kuleta nchini mwetu na mwandishi wa habari amelipiwa *business class* kuja kuhubiri habari za *lesbianism and gayism*. Leo hii mnasema kwamba tuache milango hii wazi Mheshimiwa Nape kaka yangu haiwezekani. Haiwezekani tukaacha milango hii wazi, haiwezekani kabisa, mwenye macho aone haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Bodi ya Ithibati. Dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama anayesimamia ajira za vijana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya malizia. *(Makofi)*

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja asilimia mia na ndugu zangu tunaoendelea kuunga mkono tuunge kwa ujasiri wa hali ya juu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Lijualikali, Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, naomba majedwali ya marekebisho ambayo tumeyapeleka Ofisi ya Katibu asubuhi hii yaingizwe kwenye mjadala huu kwa sababu Kanuni ya 86(11) ipo wazi. Kama tunataka kutunga sheria basi tufuate Kanuni za utungaji wa sheria, majedwali yetu yote tuliyoyapeleka yaingizwe ili sheria hii tuijadili na tuipitishe kama inavyotakiwa na Kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kufafanua mambo kadhaa ambayo yamezungumzwa utafikiri ni mambo mapya lakini siyo mambo mapya hata kidogo. Naomba sana Mwalimu wangu Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe anisaidie kama nitakuwa nakosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, inazungumzwa hapa kwamba suala la *accreditation* ya waandishi wa habari ni jambo jipya kwamba hatuwezi tukaachia holela tasnia hii, ni kitu kipya, ni kitu muhimu na kadhalika. Siku ambayo Sheria ya Magazeti ilitungwa mwaka 1976 siku hiyo hiyo ilitungwa Sheria ya Shirika la Habari la Tanzania (SHIHATA) na sheria ile pamoja na mambo mengine iliipa SHIHATA mamlaka ya kuandikisha waandishi wa habari na kuwapa vitambulisho. Kwa hiyo, kwa muda wa miaka 24 ambayo Shirika la Habari Tanzania lilikuwepo kwa mujibu wa sheria, moja ya majukumu yake

ilikuwa *accreditation* ya waandishi wa habari. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kama nakosea naomba aniambie Mwalimu wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mwaka 2000 ilipopitishwa Sheria ya Kufuta Shirika la Habari Tanzania, sheria ile ilikasimu mamlaka yaliyokuwa ya SHIHATA kwa Idara ya Habari Maelezo isipokuwa mamlaka ya ku-*accredit* waandishi wa habari yaliondolewa. Mamlaka ya kusajili waandishi wa habari yaliondolewa kwa mujibu wa kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Kufuta SHIHATA. Kama nakosea Mwalimu wangu nisahihishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kitu muhimu ni kwa nini mamlaka ya *accreditation* yaliondolewa mwaka 2000 na Sheria ya Kufuta SHIHATA. Sababu ipo kwenye taarifa ya Tume ya Rais ya mfumo wa Chama Kimoja au Mfumo wa Vyama Vingi maarufu kama Tume ya Nyalali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1991 Tume ya Nyalali ilipotoa taarifa yake pamoja na mapendekezo mengi mengine ilisema kwamba Sheria ya Magazeti, Sheria ya SHIHATA iliyokuwa inaweka utaratibu wa waandishi wa habari kuandikishwa, asipoandikishwa hafanyi kazi, sheria hiyo inakwenda kinyume na matakwa ya Katiba ya uhuru wa habari na uhuru kwa vyombo vya habari. Ndiyo maana *accreditation* ya waandishi wa habari iliondolewa kwa sheria iliyofuta SHIHATA. Kama nakosea Mwalimu wangu naomba unisahihishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuulizane kama *accreditation* ya waandishi wa habari iliondolewa kwa sababu inapingana na Katiba kwa sababu inazuia uhuru wa habari kwa nini inarudishwa sasa hivi? Tukijibu hilo swali tutakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee, masharti haya ambayo yako kwenye Muswada huu, masharti ya udhibiti wa magazeti yaliingizwa kwa mara ya kwanza katika sheria inayoitwa Sheria ya Magazeti ya mwaka 1928 *(Newspapers Ordinance 1928)*. Ndiyo iliweka utaratibu huu ambao umepigiwa kelele tangu mwaka 76 ilipotungwa hii Sheria ya Magazeti.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Taarifa.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kudhibiti magazeti kwa kutumia mamlaka ya usajili …

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Umeelezewa vizuri sana na mwandishi wa kitabu hiki, *The Media History of Tanzania.*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Lengo la sheria ya kikoloni, lengo la Sheria ya Magazeti ya mwaka 1928 ilikuwa kuhakikisha kwamba *an indigenous press* haikui.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya usajili wa magazeti ya mwaka 1928 yaliingizwa kama yalivyo na Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976. Sasa kwa wasiofahamu, naomba mkaangalie mjadala wa Bunge wa mwaka 76, Edgar Maokola Majogo alizungumza kitu gani. Edgar Maokola Majogo alisema sheria hii tunayopitisha ina harufu nyingi ya kasumba za kikoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii masharti ya Sheria ya Magazeti ya mwaka 1928 yaliyoingizwa kwenye Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976, miaka 40 baadaye yameingizwa kama ilivyo katika Muswada huu. Maana yake ni kwamba tangu mwaka 1928 utaratibu wetu wa udhibiti wa magazeti, wa udhibiti wa habari falsafa haijabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, vifungu vyote vya uchochezi vilivyopo katika Muswada huu vimeingizwa kama vilivyo kutoka kwenye Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976. Sasa hapa ni muhimu tujue vilitoka wapi kwenye Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1952 miaka miwili kabla TANU haijaanzishwa wakoloni wa Kiingereza walileta sheria, iliingizwa katika Kanuni yetu ya Adhabu kwenye *Penal Code* sheria ambayo iliingiza makosa yote ya uchochezi kama yalivyo katika Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na kama yalivyo katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mjadala wa Baraza la Kutunga Sheria *LEGCO* la mwaka 1952, wakati vifungu hivi vinaingizwa walikuwa wanasema kuna haja ya kudhibiti wanaopinga Serikali, kuna haja ya kudhibiti wachochezi. Ndiyo maana, Mwalimu wangu naomba anisaidie, watu wa kwanza kupatikana na hatia ya uchochezi kwa mujibu wa sheria hii walikuwa watatu. Wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wa pili alikuwa Robert Makange, Mhariri wa Gazeti la ... (*Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako umekwisha.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Hiyo kengele ya pili.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Andikeni.

**MBUNGE FULANI:** Siyo darasa hilo.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Wote wameshika peni.

**MBUNGE FULANI:** Wameandika.

**MBUNGE FULANI:** Mmeelewa watu wanaosoma siyo maneno maneno tu.

**MWENYEKITI:** Naelewa ulikuwa na mengi lakini muda wetu umekwisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ni Mheshimiwa Raphael Japhary Michael. Mheshimiwa Japhary.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nafasi yangu aichukue Tundu Lissu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hamuwezi kuniambia nifanye nini. Anayefuata ni Mheshimiwa Amina Mollel. Amina Mollel. *(Makofi)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Muswada huu wa Huduma kwa Vyombo vya Habari. Kwanza kabisa naomba ni-*declare interest* kwamba na mimi ni

mwanahabari na ni mwanahabari ambaye nina sifa kwa sababu nina *degree* ya uandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu wenye heshima kwa taaluma hii ya habari. Kwa muda mrefu waandishi wa habari wameitwa majina mengi, wamedharauliwa na wapo wengine ambao walikuwa wakijiita *critical thinker* lakini waandishi wa habari na nakumbuka hata nikiwa chuo tulikuwa tunaambiwa sisi siyo ma-*critical thinkers* kwa maana hiyo Muswada huu utaleta heshima kwa wanahabari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mengi lakini nianze tu kwa kusema kwamba siku zote ukiona jambo zuri, ukiona jambo linapigiwa kelele ujue basi hilo jambo ni zuri na limewakamata pabaya wale wasiopenda. Sisi ni wanasiasa basi tuwe wavumilivu tunapozungumza. Kelele za chura huwa hazimzuii ng'ombe kunywa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia baadhi ya vipengele la kwanza niipongeze kwa mara nyingine Serikali kwa kuondoa vile vipengele ambavyo vilikuwa na utata na kwa maana hiyo inadhihirisha kabisa kwamba ni Serikali sikivu na kwa maana hiyo imeondoa vile vipengele ambavyo kwa namna moja au nyingine vimezua mjadala mkali na hasa kwa wanahabari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taaluma ya habari inakwenda kuwa na heshima kwa maana kwamba wengi ambao walikuwa wakifanya kazi hii kwa namna moja au nyingine wamepitia changamoto mbalimbali. Lingine kubwa zaidi ni kutokana na malipo madogo au malipo kiduchu waliyokuwa wakilipwa na hasa kutokana na kutokuwa na sifa. Kwa maana hiyo Muswada huu utawabana wamiliki wa vyombo vya habari, utavibana vyombo vya habari kuhakikisha kwamba Mwandishi wa habari ambaye ameajiriwa katika chombo husika basi atalipwa kulingana na taaluma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la waandishi wa habari kuwa na bima ni jambo muhimu sana na hivi karibuni, nitumie mfano tu wa Mwandishi wa habari mmoja ambaye kwa muda takriban wa miaka miwili alikuwa akisumbuliwa na maradhi ya saratani. Waandishi wa habari walimuunga mkono sana mwenzao katika kumchangia ili kuhakikisha kwamba mwenzao anapata matibabu, lakini kwa sababu Mungu alimpenda zaidi hatimaye hatunaye hivi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama naye huyu angekuwepo katika mfumo huu wa malipo au wa bima hizi kwa waandshi wa habari, kwa namna moja au nyingine ingemsaidia sana pale tu alipogundua matatizo kuweza kuyashughulikia na bima hiyo ingeweza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la uchochezi kwa urefu kidogo na nitakwenda kwa kutoa mifano ambayo leo hii tunapozungumza tunayo, mifano halisi ya wale ambao kwa namna moja au nyingine wametumia kalamu yao vibaya. Tunajua kwamba *media is powerful* na kalamu hii inapotumika vizuri inaleta maendeleo na kwa maana hiyo Muswada huu utakwenda kusaidia pia waandishi wa habari kuhakikisha kwamba habari zipi ambazo tunamsaidia Rais wetu zenye kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1994, nchi ya Rwanda iliingia katika mauaji ya Kimbari na mojawapo ya mambo ambayo yalichangia kwa kiasi kikubwa ni mwandishi ambaye pia alikuwa ni Mhariri wa Gazeti la Kangura na huyu siyo mwingine ni Hassan Ngeze. Wengi tunamfahamu Hassan Ngeze ambaye kwa wale wanahabari ambao wanafuatilia habari wanajua leo hii yupo katika mahakama ya The Hague nchini Uholanzi amefungwa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hassan aliandika habari katika gazeti la Kangura kuhusiana na amri 10 za Hutu. Katika hizo amri ni kwa jinsi gani zikiwahamasisha hawa Wahutu kuua Watutsi na kwa hiyo habari ambayo iliandikwa katika gazeti hilo ndiyo ambayo iliyomsababisha Hassan Ngeze akafungwa maisha leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi karibuni tu nchini Ufaransa gazeti la *Charlie Hebdo* ambalo lilichapisha vikatuni vya Mtume *Muhammad (S.A.W)* na kwa maana hiyo vile vikatuni vilisababisha mauaji makubwa kwa waandishi wa habari. Hii inaonesha kwamba waandishi wa habari tusipotumia kalamu zetu vizuri zinaweza kutuingiza katika matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu suala la *Richmond* na katika suala hilo la *Richmond* mengi yaliandikwa na tuliaminishwa mengi sana. Naomba tu ninukuu baadhi ya mifano michache ambayo ilitumiwa katika vichwa vya habari katika magazeti. Mfano, katika gazeti la Mwanahalisi, gazeti hili la terehe 18 Januari, 2012 liliandika "Lowasa anajua uzalendo au ni machozi ya mamba?" Huu ni mfano mmojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti la Mwanahalisi la terehe 6 Aprili, 2011 liliandika "Lowasa hasafishiki", huu ni mfano mwingine. Lakini hapo hapo gazeti la Mwanahalisi likaja pia kuandika kwamba; "Lowasa karibu CHADEMA". Tuna haja gani ya kuwa na waandishi kama hawa ambao leo hii wanaamka, wanaandika habari kwamba huyu mtu ni mbaya, lakini kesho hiyo hiyo uwongo huo huo unabadilika na kuwa ukweli? Tunahitaji kuwa na Miswada na sheria kama hizi ambazo zitaweza kulinda taaluma ya habari. Taaluma ya habari, tunapokwenda kuupitisha Muswada huu ni kwa manufaa ya Wanahabari. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Nakutia moyo Waziri Nape, kaza buti hapo hapo…

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako.

**WABUNGE FULANI:** Lowasa, Lowasa!

**MBUNGE FULANI:** *Order*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba staha ndani ya Bunge. Naomba msimchezee chatu anaweza akakunyima ushindi. Tunaendelea, mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatwa na Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tuko hapa kujadili Muswada wa Habari. Kabla ya yote nimkumbushe dada yangu aliyemalizia kuchangia hapa kwamba kuna methali ya Kiswahili inasema: "Ukienda kwa wenye chongo fumba lako jicho" ili ufanane nao hata kama wewe macho yako yanaona sawasawa, lakini jaribu kufumba yako ufanane nao, kwa hivyo jiangalie.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu leo katika kituko cha karne kinachotokea ni anaponyanyuka Mbunge wa CCM ndani ya Bunge akatulaumu kwa sababu eti tunampenda Lowasa, hiki ni kituko cha karne. Waheshimiwa rudini kwenye kumbukumbu kidogo tu. Mkutano Mkuu wa CCM, jinsi kale kawimbo katamu "kweeli"...

**WABUNGE FULANI:** Kweli kweli Lowassa. *(Makofi)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Waheshimiwa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawasihi tena naelewa makando kando ya hoja hii, lakini nawasihi tuna kazi kubwa mbele yetu tujielekeze kwenye Muswada, Mheshimiwa changia bila kutaja majina ya watu ambao hawamo humu.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie tu kati ya watu ninaowaheshimu katika Bunge hili ni Mwenyekiti wewe kwa busara zako na hekima zako, lakini Mheshimiwa inapokuja hoja kutoka upande ule na tunaijibu kwa uzito unaofanana ule, naomba utupe nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala uliopita ulikuwa una nyenzo zote; una dola, una vitu vyote, Ikulu ilikuwa kwao, vyombo vya mashtaka vilikuwa kwao, kila kitu uwezo, *power* ya dola yote ilikuwa kwao. Katika kipindi chote walishindwa nini kumshtaki na kumshughulikia Lowassa mpaka yanakuja leo? Kwa hivyo, ninachosema ni kwamba ukienda kwa wenye chongo fumba lako jicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia kwa hadithi moja ndogo pia. Mheshimiwa Rais wa kwanza wa Zanzibar baada ya uhuru, marehemu Abeid Amani Karume, Mungu amuweke anapostahiki, alipokuwa na Maswahiba zake wa karibu baada ya nchi ile kupata uhuru, baada ya mapinduzi yale matukufu, moja kati ya sheria alizoweka, Zanzibar akiwa na maswahiba wake wa karibu kabisa, aliidhinisha chakula cha gerezani, Zanzibar kule kwetu tunaita Chuo cha Mafunzo kiwe ni dona, sembe na maharage, hiyo ndiyo kanuni aliyoipitisha. Hicho ndiyo chakula cha gerezani na kwa wakati ule Zanzibar kumlisha mtu dona na maharage ilikuwa kweli ni adhabu, ilikuwa ni adhabu kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haukupita muda mrefu alikosana na baadhi ya maswahiba zake waliotunga pamoja hiyo sheria. Matokeo yake wale mabwana wakaenda gerezani, watu wawili hao sipendi niwataje ni marehemu. Walipofika gerezani walikutana na chakula dona na maharage. Wale Mabwana mmojawapo alianza kula mmoja kilimshinda hakuweza kula. Siku ya mwanzo, siku ya pili, ilipofika siku ya tatu yule mwenzake amwambia "Shekhe inabidi ule kwa sababu hii sheria tuliipitisha wenyewe, tulikuwa pamoja wakati wa kupitisha hili na hivyo leo tumekuja hapa lazima tule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo sheria hizi, Muswada huu unaoletwa leo hapa, madhumuni makubwa ikiwa kwamba wanakomolewa watu fulani na kukiwa na lengo mahususi la kulenga uchaguzi wa 2020, Mungu ni mkubwa sana hapo katikati bado kuna safari ndefu sana. Linaweza likatokea lolote la kutokea, wanaotuletea huu leo wakawa waathirika wa mwanzo na *Inshallah* kwa Mwenyezi Mungu awajaalie wawe waathirika wa mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo binafsi sitaki niseme sana, lakini wakati mwingine tunapotoa hoja huku zinaangaliwa wanaotoa ni Wapinzani. Tunapotoa mawazo huku yanaangaliwa wanaotoa ni Wapinzani hata mazuri yanabezwa, matokeo yake leo hii tunaathirika kwa Sheria ya Ugaidi iliyopitishwa na Bunge hili. Sheria za ugaidi za kuwakamata watu na kuwaweka makorokoroni katika muda ambao hata haupatikani ushahidi ni moja kati ya sheria ambazo zilipitishwa na Bunge hili ambazo zinawaathiri, zinawanyanyasa, zinawanyima haki watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko ushahidi kadhaa, leo katika magereza Tanzania, kuna wafungwa wanaohusishwa na kesi za ugaidi walioko mahabusu wasiopungua 85, Masheikh wa dini ya Kiislam, ni miongoni wa zile sheria zinazopitishwa kwa uharaka ili kukidhi mahitaji ambayo wenzetu mnaona yana maana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili hili lilikaa Bunge la Katiba, yakapitishwa maamuzi tukashauri vizuri, Katiba hii siyo, rasimu inayofaa kufuatwa ni hii, mkafanya mliyoyafanya, mkaona yale mawazo yetu hayana maana, matokeo yake jana mmesikia Mtukufu Rais alivyosema. Yote hayo ni kutokana na kupuuza maneno yetu ambayo wakati mwingine msipokubali leo, kesho mtakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha zaidi katika hili, Waheshimiwa tunakaa hapa tunajadili hili jambo, kabla ya kujadili hili jambo ni nini kilitokea? Sote tunajua. Hawezi kutumikia mtu mabwana wawili kwa wakati mmoja. Uchague kutumikia wananchi au uchague kutumikia nguvu ya pesa. Waswahili wanasema penye udhia penyeza rupia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mtukufu Rais anasema ukiingia kesho anausaini na anao uwezo wa kusema hivyo kwa sababu anajua nini kilichotangulia, anajua, anajua nini kilichotangulia. Sasa ninachosema ni kwamba tunapoteza muda bure, leo Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi Mwenyekiti wa Kamati hii ambayo ameutetea Muswada huu na amekataa wadau wasitoe maoni yao katika muda muafaka ni sawa na mchawi aliyepewa mtoto alee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote asingekwenda vingine kwa sababu anajulikana ni mtu wa upande gani au ni mtu ana mwelekeo gani. Kwa hivyo, haya yanayotokea tunafanya kazi bure lakini kwangu mimi Muswada huu na mtayarishaji mkuu, Waziri huyu ambaye mwelekeo wake toka alfajiri alipoingia hapa tulianza kuuona, toka akiwa huko nje tulianza kumwona, mtu maarufu wa goli la mkono. Msitegemee katika maisha yake ataleta kitu cha heri katika Bunge hili hata siku moja. Msitegemee hata siku moja kama

ataleta jambo lenye heri kwa Watanzania, huyu ni mchafuzi, ni mchafuzi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naseme kwamba haya mnayoyafanya jiangalieni vizuri. Bunge lililopita tulikuwa tumeishia mstari huu hapa, Bunge hili tumebakisha ka-*quarter* kadogo. Mwaka ujao he! He! 2020 na matendo haya na kwa Mawaziri hawa akina Nape Nnauye, Watanzania wahukumuni *Musha-Allah*. *(Makofi)*

Waheshimiwa msihuzunike sana. Muswada huu naufananisha na utunzi wa mtunzi mmoja anaitwa Suleiman Rashid… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda. Mheshimiwa Devotha Minja

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikiliza sana Waziri wakati anawasilisha Muswada huu. Waziri amesema anaenda kuandika historia, nikubaliane nae anaenda kuandika historia ya kutengeneza Muswada ambao wadau hawakushirikishwa. Tumewahi kuona wapi? Tumejaribu kujifunza na kuangalia katika Mataifa mengine yenye sheria kama hii; wadau wanapewa nafasi, wadau wanapewa kipaumbele kwa maana ya kutoa mawazo yao na michango yao, lakini kwa Muswada huu tunakwenda kuupeleka kwa jinsi ambavyo Serikali imeamua, watekelezaji wa sheria hii wako kando. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iingie tu kwenye rekodi na ieleweke hivyo kwamba wadau waliomba waongezewe muda, ni kwa nini wadau wanataka muda? Muswada huu ulisomwa mara ya kwanza tarehe 16/9/2016 wadau wakaomba watoe mawazo yao, wakafika kwenye Kamati, wakaomba waongezewe muda. Kwa nini wanataka muda? Kwa sababu tasnia hii ya habari ina wadau wengi wakiwemo waandishi wa habari ambao ndiyo watekelezaji wa Sheria hii. Tunazungumza hivi sasa tukiwa na redio zaidi ya 200 ziko vijijini, tunahitaji kupata michango yao badala ya kupata michango ya waandishi walioko mjini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wakaomba waongezewe muda, Muswada huu uje Bungeni hapa katika Bunge lijalo lakini waliongezewa siku kumi. Hii imekuwa *novel* ya kusoma kwa siku kumi? Hii ni Sheria ambayo kila mmoja alipaswa aje na mawazo. Utaweza kuona katika Muswada huu Waziri anatuambia kwamba una maslahi mapana ya waandishi. Yako wapi maslahi

ya waandishi hapa? Tumeshuhudia waandishi wa habari wakipigwa, wakiuawa, wakimwagiwa tindikali, sheria hii inasema wapi kuhusu kuwalinda hawa waandishi wa habari wakiwa kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, Waziri anasema kwamba anakwenda kutengeneza historia. Historia gani ambayo hakuna michango na mawazo ya hawa waandishi? Historia gani ambayo hakuna popote palipozungumza hata kima cha chini cha mwandishi wa habari alipwe nini, iko wapi? Tuseme basi Muswada huu unatetea kwa maana ya kuwa na sehemu ambayo inaonesha mwandishi wa habari alipwe kiasi gani, awe na mazingira gani ya kutekeleza kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu ya wadau ni nini? Hofu ya wadau Mheshimiwa Waziri ameandika historia ya peke yake. Katika kipindi cha mwaka mmoja ya Uwaziri wake, amekwenda kufunga magazeti, amefunga redio, hana mikono misafi na ndiyo maana waandishi wana hofu, wanataka wahakikishe kwamba Muswada huu wanausoma vizuri, wanatoka na majibu ambayo watajua ni nini hatma ya vyombo ambavyo ndivyo wanavyovitumikia na ndivyo vinavyowapa kula yao asubuhi na jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu nyingine ya wadau katika hili, ni kwa nini Serikali haikuona kwamba kuna haja ya kuwapa nafasi. Nimeshiriki kwenye hii Kamati, baadhi ya michango ya wadau ambayo niliiona ni kutoka kwa TWAWEZA na kutoka kwa *TLS,* halafu tunasema hii ni michango ya wadau. *TLS* anafahamu, TWAWEZA wanafahamu shida, adha ya waandishi wa habari ambao wanatembea kwa miguu barabarani wakitafuta habari? TWAWEZA wanayaelewa haya? Ungeniambia *UTPC* wanaelewa, ungeniambia *TAMWA* wanaelewa, ungeniambia *MCT* wanaelewa, ningeelewa, lakini TWAWEZA?

Mheshimiwa Mwenyekiti, TWAWEZA wanafahamu *a, b, c* za uandishi wa habari? TWAWEZA wanajua shida waandishi wanayoipata? Kwa hiyo, tunakuja na mawazo kwamba TWAWEZA wametoa na *TLS* wametoa. Hii tunaifananaisha na kama, wao ni wadau walioalikwa tu kutoa mawazo yao lakini wadau halisi ambao walipaswa kuingia hapa hawakushirikishwa. Ni kama tuseme mtu unaandaa harusi waalikwa wanashiriki lakini bwana harusi na bibi harusi hawamo halafu unaita ni harusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unakwenda kumpa mamlaka Waziri ya kuamua ni nini ambacho waandishi wa habari wanataka waripoti, kwa nini? Kuna vipengele ambavyo vinasema kwamba Waziri ndiyo mwenye mamlaka ya kuangalia ni kitu gani kinaripotiwa kwa muktadha, kwa maslahi ya usalama wa Taifa, usalama wa Taifa ambao una sheria zake, ambazo zinafuatwa lakini Waziri ndiyo anasema kwamba yeye ndiye atakayeenda

kupewa mamlaka ya kuhakikisha kwamba kila kinachoripotiwa yeye ana mamlaka ya kujua ni kitu gani ambacho kinaenda kuandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tumeona kwenye hotuba yake Mwenyekiti wa Kamati anasema mazingira mazuri yanayoenda kutengenezwa kwa waandishi wa habari ni pamoja na kuweka *dressing* code. Leo hii Taifa hili ambalo tunaona umuhimu wa vyombo vya habari tunahitaji kwenda kuwa na *dressing* code? Waandishi wa habari wamekuwa wakifanya kazi za utafiti, wanahitaji kuvaa nguo kufahamika wanafanya nini? Tunafikiri ni vitu ambavyo Serikali imejenga mikakati kuhakikisha wanaenda kudhibiti, kuhakikisha waandishi wa habari hawafanyi kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Bima ya Afya kwa waandishi wa habari tumeliona na sisi tunasema kwamba hilo halitoshi pekee kusema kwamba ndiyo maslahi ya waandishi wa habari. Tumeweza kuweka misingi gani ambayo itawabana hawa wamiliki wa vyombo vya habari kuwasaidia hawa waandishi wa habari kwa maana ya kuwalipa mishahara ambayo inaendana na kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kuna kipengele kingine kwamba Waziri ndiyo atakwenda kutengeneza kanuni ambazo zitakwenda kusaidia baada ya Sheria hii kutungwa. Tuliomba kwamba iwekwe wazi hapa tujue ni *regulation* zipi ambazo zinawekwa kwa sababu ya matamko mbalimbali ya Waziri ambayo amesikika akiyazungumza kwenye vyombo vya habari kwamba anataka uandishi wa habari lazima uanze na *level* ya *degree*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Taifa gani ambalo lina sheria hizi ambalo limeweka kwamba kigezo cha mwandishi wa habari lazima awe na *degree*. Tumeona Mataifa mengi ambayo hata uchumi wake unaimarika, kuna *level* mbalimbali, kuna watu wa *certificate,* wapo watu wa *diploma,* wapo watu wa *degree* lakini wanatambulika kutokana na michango yao wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani tukizungumzia suala la kazi za udaktari, kuna madaktari wa *AMO,* kuna madaktari wa *MD,* kuna madaktari wenye *masters* lakini wote wanafanya kazi, lakini *council* ndiyo yenye mamlaka ya kuhakikisha kwamba wanatengenezaje madaraja ya hawa waandishi wa habari, lakini kuja na vigezo vya *degree* kama mbinu ya kuwagawa waandishi wa habari, leo hii wazee ambao wamefanya kazi iliyotukuka hasa ya kupigania uhuru wa Taifa hili basi wasionekane kama nao ni waandishi wa habari kisa hawana *degree* ya uandishi wa habari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tunataka Sheria iseme wazi kwamba ni kanuni zipi ambazo zinakwenda kutengenezwa kwa ajili ya kusimamia sheria hii. Kanuni ziwe wazi, zieleze kwamba mwandishi wa habari atakwenda kuwa ni

mtu wa namna gani na sisi tunasema kwamba mwandishi wa habari awe ni mtu yeyote ambaye amemaliza *form four,* mtu yeyote ambaye amesoma *certificate, advanced certificate* ya uandishi wa habari, mtu ambaye hata ana *diploma* atambulike, hata ana *degree* atambulike kwa sababu vyuo hivi vilisajiliwa na *NACTE,* kwa maana hiyo Serikali inatambua ni vyuo ambavyo vinafanya kazi ya kuwatengeneza waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuja na mkakati wa kwamba sasa tunakwenda kukomesha kwa kuleta suala la *degree* katika uandishi wa habari, hii itafanya waandishi wengi wenye *passion* ya kufanya kazi hii kuhakikisha wanatoka kwenye hii na sijui; tunasema tuna mpango wa kuongeza ajira lakini tunaenda…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Devota.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omar Ali King, atafuatiwa na Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie Muswada huu wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai na leo kuja kushuhudia haya ambayo tunayaona, mengine kusema kweli kwamba ni mambo ya kushangaza kidogo, hata katika nafsi yangu nashangaa sana. Lakini siwezi kushangaa sana, unajua mtu anapokumbwa na *sakaratul maut,* anapokaribia kufa pale basi chochote kile kinamtoka. Atasema maneno yaliyokuwemo na yasiyokuwemo. Kwa hiyo, na hii ni *sakaratul maut* imewakuta watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizungumzia hapa Mheshimiwa Khatib, alitaja habari nzuri kidogo. Habari ya wale waliokuwepo kule magereza Zanzibar miaka ya 90 wakati na mimi nilikuwa ni mtumishi kule. Hata hivyo, kitu kimoja tu alikosea, walikuwa rumande, kwa hiyo rumande walikuwa wakiletewa chakula kutoka nyumbani, nacheza na *super league* wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika Muswada. Katika Muswada huu ambao umezungumzia masuala ya kuipa hadhi hii taaluma ya habari, imezungumzia suala la *accreditation,* wengine walisema humu wanashangaa kwa nini wameikuta humu *accreditation* au wanaona ajabu kwa nini watu wanajadiliana nayo wakati hiki kitu kilikuwepo tokea mapema. Kusema ukweli, suala la *accreditation* ni suala muhimu sana kwa waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia hata *referee* basi pia naye wanafanyiwa mambo haya na wana daraja zao, leo tuje tulikatae katika uandishi wa habari. Yaani tunazungumzia habari hizi kana kwamba hatuoni nini faida yake. Kwa hiyo, hili suala la *accreditation* kwa waandishi wa habari ni suala muhimu na napendelea hilo suala liwepo. Cha kushangaza kwamba leo tunasema kwamba tunawatetea waandishi wa habari wakati mnawatetea huko mnakuja na nyimbo kwamba mna imani na mtu fulani, sasa mnatetea au nani aliyetetea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iko mbele yetu, kama tunawatetea waandishi wa habari basi hebu tujeni na kitu cha kuwatetea hao waandishi wa habari. Tukija na nyimbo hizi ambazo mnazileta humu, mnafanya kitu ambacho hakiwezekani kabisa, sio kitu kizuri kwamba hata hiyo imani yenu na hao waandishi wa habari wanaowasikiliza sijui wanawaweka daraja gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo katika mjadala wetu huu, nimesoma hoja zote; nimesoma hoja ya Waziri, hoja za Kamati na hoja za upande wa Upinzani, pamoja na wengine wenzangu waliochangia, ndiyo tumesikia jinsi gani watu wanavyochangia, lakini nilichobaini kwamba kuna watu wamekuja kutia kidusi tu, kwamba ni kidusi ili bata asilike, lakini tangawizi ya kumuoshea iko, atalika bata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama kwenye kitabu hiki cha Kambi ya Upinzani, katika *page* za mwanzo kama kilipinga lakini *page* za mwisho, kikaja kikakubali yale ya leseni, baraza huru, hiyo ithibati. Kwa hiyo, utakuja kukuta kwamba ni kakidusi tu, lakini hiki kitu kinakubalika. Sasa hicho kidusi hapa pana tangawizi, pataoshwa na italika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama humu unaweza ukaja ukakuta kwa lugha ya kilingala tunasema "poto poto" kwamba tope tupu. Huku unazungumza hivi, halafu unakuja unajikanyaga. Sasa katika hawa waandishi wa habari kama tunataka haki zao, basi moja ni hiyo *accreditation* kwa sababu tukitazama katika *perspective* ya waandishi wenyewe ambao wengi wametazama kule kwenye waandishi, hawakutazama kwa wale walaji wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la *accreditation* ni la muhimu, lakini hapa tukaja tukaleta historia, labda fulani alikuwa akifanya uandishi wa habari bila ya kuwa na taaluma, fulani alifanya uandishi wa habari bila ya kuwa na taaluma fulani. Sasa tusirudi huko, sasa hivi tunataka kwenda mbele, Taifa kama hili sasa hivi mambo mengi yamebadilika. Kuna mshairi mmoja anasema "zama zimebadilika na mambo yamegeuka" sasa zama zimebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa anauliza hapa Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba kwa nini iwe hivi katika masuala ya *accreditation? Wa tilkal ayyamu nudawiluha baina nnasi,* hizi ni siku ambazo mambo yanageuka, siku hazigandi, watu hawabakii vile vile, *we are not static!* Siku zote ulimwengu uko *dynamic,* mambo yako hivyo. Kwa hiyo, ni lazima tutazame jinsi ya kuweza kuwawezesha waandishi wa habari. Suala hili litawawezesha kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni katika masuala ya habari hizi za uchochezi. Kusema ukweli ni muhimu sana kuwa na Sheria hii kwa sababu wengi wanasema daktari awe na taaluma, lakini mwandishi wa habari asiwe na taaluma. Daktari anaweza akamuathiri mtu mmoja katika chumba cha operesheni, lakini mwandishi wa habari anaweza akaathiri jamii nzima, Tanzania nzima, watu milioni 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo *accreditation* ya mwandishi wa habari iwe kubwa zaidi kuliko hata ya daktari, kwa sababu daktari atamhukumu mmoja au atafanikiwa kumwathiri mmoja, lakini je, mwandishi wa habari kwa kalamu yake atawaathiri wangapi? Kuna mifano ya Rwanda 1994, kuna mifano ya Kenya 2006, kuna na mifano mingine chungu nzima ambayo inatumika. Kwa hiyo, ni lazima tutazame kwamba jinsi gani mwandishi wa habari ataweza yeye mwenyewe kupata sifa ya kuwa mwandishi wa habari na pia ile jamii ambayo anaitazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu limezungumziwa neno la kashfa, pendekezo langu kwenye neno hili, bora lingetumika neno lingine kwa sababu kashfa ni kuweka wazi kwa maana fupi. Sasa anaweza mtu akaja akaambiwa amekashfu lakini akaweza kujitetea kutokana na asili ya neno lenyewe. Asili ya neno hili maana yake kukashfu ni kuweka wazi, inawezekana mtu kasema ukweli yaani, inawezekana ikaonekana amekashfu, akapata nafasi ya kujitetea kwa sababu hili neno asili yake ni Kiarabu, kashfa maana yake ni kufunua. Hata mtu ambaye anayepita hapa mavazi hayako vizuri inakuwa naye pia amejikashfu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili neno kama tumekusudia kashfa ya kumsema mtu vibaya, kumwelezea mtu katika lugha mbaya ambayo itamharibia *image* yake, bora tungetafuta neno lingine ili hili neno la kashfa

ambalo limezungumzwa humu likapata maana na katika maana hiyo ikaeleza na ikaeleweka ili kuepuka watu kuja kuweza kujitetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la taaluma ya uandishi wa habari, huko nyuma au mpaka sasa hivi baadhi ya waandishi wa habari sio waandishi wa habari ni wanaharakati. Kwa hiyo, Sheria hii imekuja kuwafanya waandishi wa habari kuwa wanataaluma. Wengine ni wanaharakati na hata jinsi wanavyoongea, utawaona kwamba ni wanaharakati, sasa tuwatoe kwenye uanaharakati, tuwafanye wana taaluma…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Saada Mkuya, Hawa ninaowataja sasa Mheshimiwa wewe utaongea kwa dakika hizo kumi, wanaofuata, isipokuwa kwa Mheshimiwa Nkamia watagawana dakika tano, tano tu. Tunabaki ndani ya muda ule ule. Mheshimiwa Saada, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynabu dakika tano, isipokuwa kwa Nkamia nimesema; Mheshimiwa Peter Serukamba dakika tano, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete dakika tano. Mheshimiwa endelea.

**MHE. SAADA S. MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha leo kuwepo hapa asubuhi, kwa ajili ya kukamilisha majadiliano yetu. Nachukua fursa hii vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kukamilisha mchakato huu na kuleta Muswada huu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kalamu ni kitu ambacho muhimu sana. kama tutakitumia vizuri, tunaweza tukajenga nchi yetu na watu wake vizuri. Mwenyezi Mungu katika Sura ya 96, katika *Quran* kwenye aya ya nne anazungumza kwamba amemfundisha mwanadamu kuandika kwa kalamu, kwa kuonesha umuhimu na hii ni sura ya kwanza wakati inateremshwa *Quran*. Kwa hivyo kalamu ni jambo muhimu sana katika maisha ya mwanadamu ya kila siku. Kwa maana hiyo, katika *content* hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa na *gut* ya kusogeza Muswada huu hapa ambapo tunaujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongelea sana suala zima la uanzishwaji wa Mfuko wa Mafunzo wa Waandishi. Tumezoea sana zikija sheria hapa, pamoja na mambo mengine, kwamba zinakuja na uanzishwaji wa Mfuko. Lakini sheria zinatekelezwa au zimeendelea kutekelezwa isipokuwa utekelezaji wa Mfuko unachelewa sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Wabunge wenzangu *despite* ya kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja mwakani na bajeti Mungu akituweka hai na uzima, tuungane sote kwa pamoja tuhakikishe kwamba Mheshimiwa Waziri ametuambia *source of fund* ya Mfuko huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tukiwa tunazungumza tu kwamba, fedha zinazotokana na Mfuko huu ni fedha ambazo zitakazokuwa *appropriate* hapa na Bunge hii, nadhani haitakuwa sahihi. Maana yake, tunajua fedha ina mambo mengi na kama Mfuko haujawekewa *source of fund specific* kwa ajili ya *implementation* ya Mfuko huo, hatuendi mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mbali ya mambo mengine tunampongeza, lakini Wabunge wenzangu tuhakikishe kwamba yale maslahi ambayo tunataka waandishi wa habari wayapate, mambo mazuri ambayo tumekuja nayo pamoja na sheria hii ili yatekelezeke, tumwambie lazima tumsimamie Waziri tuone kwamba, ametuletea *source* maalum ya *fund* kwa ajili ya utekelezaji wa Mfuko huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hizi sifa zote zinaweza zikapotea kama hili jambo litakuwa halijatekelezwa. Tunakuomba sana, najua utafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili vilevile naunga mkono hoja hii ya kuweko *accreditation* bodi. Mwandishi wa habari amechukuliwa kama kibarua tu wa kawaida *every now and then*, sote tumeshuhudia maskini waandishi wa habari ukitoka nje ukiandikwa usitoe pesa uwagawie, yaani wewe mwenyewe unawaonea huruma kutokana na hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hii *accreditation* bodi itampandisha *value* hata yeye mwenyewe yule mwandishi. Itampandisha *value* kwamba yeye ni mwandishi ambaye tayari amekuwa *accredited* yaani ni mwandishi ambaye amepata ithibati. Kwa maana hiyo, mategemeo yetu, maslahi yake kwanza yatakuwa mazuri. Vilevile hata taarifa na habari ambazo ataziandika zitakuwa ni habari ambazo zimetokana na mwandishi ambaye amekuwa *accredited. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana hili ni jambo la msingi tukiachia tofauti zetu za kisiasa, lakini hili ni jambo la msingi sana. Kwanza kabla ya yote tunataka Mheshimiwa Waziri, mara tu Rais akishasaini hii, kanuni zisije zikachelewa. Tunaomba tupate na kanuni kwa haraka sana ili tuweze kutekeleza sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linatia mashaka kidogo Mheshimiwa Waziri na naomba sana tupate *advice* yako, ni kuhusiana na kazi ambazo zitakuwa zinatekelezwa na bodi. Hususan zile ambazo bodi itakuwa ina-*advice the Government on training* ya *media*, kuna *media* ama kuna *journalist* ambao watakuwa katika *public sector,* lakini wengine watakuweko *private*. Huu Mfuko ama hii bodi itaweza ku-*advice* vipi waandishi wa habari ambao watakuwa *private* na wao wakawa *facilitated* kwenye *training* ile. Sina uhakika hii itakuwa *covered* vipi kwa sababu *the way it has been written in the Bill* ni kwamba ime-*accommodate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Serikali ama Mfuko utakaoanzishwa sina uhakika *how far* utakwenda katika kuwasaidia waandishi wa habari, aidha, ambao ni *freelancer* au ambao wanaandikia vyombo binafsi. Kwa hivyo, hilo tunaliomba pia lifanikiwe. Naamini sana, kwa Muswada huu wa sheria tunaweza tukatengeneza Salim Kikeke wengi kutoka Tanzania kuliko ambaye yuko *BBC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Muswada huu tukiutekeleza vizuri, Mheshimiwa Waziri tutatengeneza akina Christiane Amanpour ambao ni waandishi wa habari weledi tu katika dunia na ambao tunawaamini. Kwa hiyo, tunataka huo utekelezaji uanze mara moja, lakini *with specifically* kwenye *fund* kwamba ianze kutekelezwa na Mheshimiwa Waziri atuambie hasa *source of fund* hii inatokea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri ni mwanamke, hujatuambia kwenye sheria wala mimi napata ukakasi sana kama hii itakwenda kwenye *regulation* hajatuambia kwenye sheria hii bodi *content* ya wanawake iko wapi? Eeh! hajatuambia tunaweza kusema *at least two* lakini hata wanaweza wakawa watatu mpaka wanne, hii haijasema katika sheria na sijaona kwenye marekebisho yake, kama hili amelirekebisha *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, waandishi wa habari hususan wanawake, kwanza ni watu ambao wanafanya kazi vizuri sana, vilevile mazingira tu yale yenyewe ya kufanyia kazi, ina-*pro* mwanaume kuliko mwanamke. Kwa hivyo, tunaona kwamba kuna umuhimu hasa katika bodi hii vilevile wawepo wanawake ambao wataweza kusimamia maslahi ya waandishi wa habari wanawake katika sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine na la mwisho, kalamu hii, nimesema mwanzo, kalamu ni jambo ambalo lina-*shape* Tanzania yetu. Unaweza ukaandikwa vizuri kwenye gazeti na siku hiyo *chart* yako ikapanda. Lakini tumeona *of recent* Mwenyekiti wa Kamati hii alivyopata kiki sana maana yake kila kwenye gazeti anachambuliwa yeye, kutokana tu na Muswada huu.

Naamini kwa sababu na aidha wahariri au waandishi wenyewe hawakusoma na wakaona hasa kitu kilichopo na ndiyo maana kilikuwa kinaandikwa *shell will*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi kwa maana hiyo, uandishi ni jambo ambalo litasimamia sana mwelekeo wa nchi yetu. Tumeona mwenzangu hapa Mheshimiwa Amina alitaja kilichotokea baada ya gazeti lile la…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja na natumaini Mheshimiwa Waziri atayatekeleza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Zaynabu Vulu, dakika tano na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, dakika tano.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Niwe miongoni mwa wale ambao watachangia katika jambo lililo mbele yetu ambalo ni Muswada. Muswada huu ni muhimu sana, kwa waandishi wa habari, lakini pia Muswada huu ni muhimu sana, kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri ameweka historia. Sote tunajua, waandishi wa habari walikuwa wanalitaka jambo hili kwa muda mrefu sana, kiasi ambacho kulianzishwa taasisi zisizo za kiserikali kwa maana ya *NGO's* za wanahabari wanawake, za wanahabari wa michezo, za wanahabari wa mazingira, wote hawa walikuwa na lengo moja la kutaka kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Muswada umeletwa, niombe Muswada huu uharakishwe kama Mheshimiwa Rais alivyosema na bahati nzuri tunaumaliza leo Jumamosi, kesho unasafirishwa, Jumatatu anaweka saini kazi mbele kwa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamesemwa, lakini niombe katika yaliyozungumzwa mle niweke msisitizo kwa mambo machache. La kwanza, bodi iwe na uwiano, wanawake watazamwe, kanuni ziharakishwe, kwa sababu ndiyo zitakazosaidia mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa umuhimu wa Muswada huu, ndugu yangu Kubenea hayupa a.k.a Yuda Iskarioti, amezoea kuajiri watu kuwalipa kwa posho ya stori anauogopa Muswada huu. Uharakishwe, wanaonyanyasika

na wanaodhalilika, waandishi wa habari ambao hawajawahi kupata mshahara kwa wakati, basi hii sheria itakwenda kuwasismamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ni suala la bima. Tumeshuhudia waandishi wa habari, wanapita katika maeneo mbalimbali hawana bima wanahitaji kupatiwa bima kwa sababu hayo waajiri walikuwa hawayaangalii. Kwa hiyo, nina hakika hili litawasaidia na litawapeleka kwenda kufanya kazi zao vizuri na kwa uadilifu na kwa uangalifu. Napata kigugumizi wanaposema watu wasipatiwe leseni, hivi dereva gani atakayepita na gari barabarani asiwe na leseni, *traffic* akamwacha, Daktari gani atakayemtibu mgonjwa hana cheti, tumeshuhudia Madaktari feki wangapi wanaokamatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelalamika sana kwenye tasnia ya habari, kwamba ilikuwa inaachwa nyuma haiangaliwi. Niombe wenzangu mliokuwa humu ndani tuhakikishe tunaupitisha na nawashukuru wale waliotoa historia ndugu yangu Tundu Lissu ametoa historia nzuri sana, wengine tumejifunza mengi, tulikuwa hatuyajui. Baada ya kuchangia yeye akaona atoe historia mdogo wangu na Devota Minja na yeye hali kadhalika. Kwa hiyo, nasema Muswada huu umekuja kwa wakati tuupitishe uweze kufanya kazi kwa urahisi kwa ajili ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kikwete Ridhiwani.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite moja kwa moja kwenye Muswada na mimi kama Mwanasheria naomba niitendee haki *professional* yangu kwa kutoa masahihisho ambayo ningefikiri Mheshimiwa Waziri akiyachukua yatatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nianze na *section six (6)*. Mheshimiwa Waziri *section six* (6) inatambua vyombo vya habari vilivyopo katika mtazamo wangu hasa nikitazama katika Sheria ya Mawasiliano inatambua uwepo wa *community radios,* lakini cha ajabu sana, Muswada huu hautambui hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri wakati anajumuisha atueleze kama *community radio* ni sehemu ya *public on the media* au ni *private on the media* kwa sababu hizi sizielewi. Pia nitoe angalizo zaidi, kwa kuwa sheria hii inakwenda kubadilisha sheria zote ambazo zinahusiana na maeneo ya redio na mahusiano katika *printing medias,* ningeomba sana nitakapomaliza jambo hili, basi pia tugeuke katika Sheria ya Mawasiliano ili kuweka uwiano ulio sawa, kwa sababu yatakapoanza mambo ya kesi tunaweza tukapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo *section seven (7)* kwenye *obligation* za *media houses.* Kwa mujibu wa dhana nzima ya utengenezwaji wa sheria hii inaonesha kwamba inataka kuleta kitu kinachoitwa *transparency and responsibilities.* Hata hivyo, nikiangalia katika vitu vyote hivi, sioni eneo lolote ambalo linagusia *accountability and transparencies* hasa katika upande wa *management of funds.* Kwa hiyo, ningeomba tutakapokuja kurekebisha jambo hili basi Mheshimiwa Waziri aliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije *Part* III ya Muswada wetu, katika *Part* III *section* 11 inaeleza muundo wa bodi, lakini kilichonishangaza mimi *section* 14 *and* 15 inaelezea kwamba kutakuwa na mtu anaitwa *Director General* wa Bodi hiyo, ambaye pia atakuwa ndiyo *Chief Executive Officer.* Cha ajabu zaidi, yeye si Mjumbe katika Bodi hiyo, sasa mnakuwaje na bodi ambayo Katibu wake si Mjumbe na yeye Mtendaji Mkuu wa kila kitu katika hiyo. Kwa hiyo, pamoja na hayo mazuri, Mheshimiwa Waziri angeliangalia hili jambo na atakapokuja atueleze kidogo tuone limewekwaje vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo *section* 29 nakwenda haraka haraka Mheshimiwa Waziri naomba anisikile vizuri. *Section* 29 ni suala tu la *language shake*. Kuna kitu hapa ninavyotazama kwa kingereza changu cha Kikwere, naona kuna kitu kinatakiwa kiongezwe pale. Sentensi inasema: "*There shall be a secretary to the Council who shall be appointed by the Council through competitive recruitment.*" Kiingereza nafikiri kuna neno linakosekana pale ambalo ningekuomba uongeze neno *process* ili sentensi ile ikae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo *section* 31 inazungumzia jambo la kumwondoa Katibu. Tunaposema kwamba Katibu anaweza kuondolewa *on any other ground that may justify removal,* kwa kweli binafsi yangu kuna watu wanafukuzwa kwa sababu tu wana sura mbaya. Sasa katika misingi ya haki za binadamu Mheshimiwa Waziri haiko sawa, nafikiri ni vyema sheria ikaeleza sababu zinazoweza kumtoa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekit, hata ukiangalia kwenye sheria nyingine hata unapotaka kumwondoa *Judge,* unapotaka kumwondoa Wakili, unapotaka kumwondoa Daktari, unapotaka kumwondoa mtu yeyote yule, hakuna sehemu inayosema *any other ground that may justify removal. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu unaweza kuweka wakati mwingine hata kwamba; watu wakafika sehemu ya kikabila au ya kidini ikawa pia ni sababu tosha ya kumwondoa mtu. Pamoja na hayo pia, nataka niongee jambo moja la kisheria zaidi, katika maelezo inaonesha wazi kwamba hii sheria yetu inalenga kuelekeza pia mahakama iweze kutunga sheria juu ya masuala ya *defamation*. Mheshimiwa Waziri, naomba nimkumbushe jambo moja mahakama ina taratibu zake. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RIDHIWAN J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa adabu kubwa sana na kwa niaba ya watu wa Chalinze naomba kuunga mkono hoja, asante. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati iliyopelekea Muswada.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Leo mwenzenu Waheshimiwa Wabunge nina furaha kubwa sana. Nina furaha kubwa, nitumie maneno machache sana kuonesha kwamba nina furaha; yametimia, lile jipu lililowashinda wengine kwa miaka 23, leo tunakwenda kulipasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili tujisifie, kazi ambayo iliwashinda wote sisi tunakwenda kuifanya leo. Waheshimiwa Wabunge mkitaka kujua kwamba Muswada huu ni mzuri sikilizeni waliochangia wote kuanzia jana mpaka leo. Kila aliyechangia hapa, kama kuna mtu asimame aliyepinga vifungu, wote waliamua kucheza siasa tu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya sheria yenyewe, hakuna aliyehangaika kuweka neno kwa sababu kila kitu kimefanywa. Kwa hiyo, nilikuwa nawasikiliza lakini kwa sababu sisi ni wanasiasa, ukipewa jukwaa lazima ucheze nalo, na kila mtu akawa anaamua staili yake. Hata hivyo, naomba kusema, nimesoma ripoti ya ndugu yangu wa Kambi ya Upinzani. Soma ile ripoti mambo yote anayoyasema kwenye Muswada yameshafutwa, lakini yeye ameyaleta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza wengine wote wanayoyasema kwenye Muswada hayamo. Tumebaki tunasema wadau hawakushirikishwa, naomba niseme Waheshimiwa Wabunge, kama kuna wadau ambao wanasema hawakushirikishwa ni kwa sababu hawakutaka kushiriki. Narudia tena, wadau ambao hawakushiriki ni kwa sababu hawakutaka kushiriki na hawakutaka kushiriki kwa makusudi. Maana wanasema Muswada hawajausoma, kesho unawaona kwenye kipindi cha *TV* wanaujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuja kwenye Kamati, wanasema mmetupa siku tatu hatujamaliza. Baada ya siku mbili wako *ITV* wanajadili kifungu kwa kifungu. Walitaka kuendeleza tabia ileile ya kuuondoa Muswada Bungeni, sasa wamesahau hii ni Awamu ya Tano, Awamu ya Tano hatutishwi,

basi. Niwaambieni Mwenyekiti huyu hatishwi. Tumeambiwa tufanye kazi tu, kazi yetu ni kutunga sheria, naombeni Wabunge tutunge sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wengine tena nawaheshimu kweli wanasema unajua uandishi wa habari ni moyo tu! Eeh, kweli? Uandishi wa habari ni *passion* tu basi, lakini kuwa Mchumi si *passion!* Kuwa *Engineer* si *passion!* Kuwa *Accountant* si *passion* kweli! Tunataka tupate sifa rahisi sana hizi, tusiwadanganye waandishi wa habari. Sheria hii imeweka vifungu vinavyowasaidia Waandishi wa Habari wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu anapinga *accreditation* hapa. Jamani tumesema tutaweka vigezo vya nani apewe leseni pamoja na *Press Card,* lakini wale ambao hawana leseni, hawana *Press Card* hawazuiliwi kuandika. Wale wenye *passion* anaowasema Mheshimiwa Zitto wataendelea kuandika, lakini hawatakuwa *accredited* kama ambavyo mimi ni *Accountant* kama sina *CPA* siwezi kusaini *Financial Statements,* lakini hainizuwii kuandika vitabu vya uhasibu. Ukiwa Mwanasheria hujashinda Uwakili Mahakamani huendi, lakini kazi za Sheria huwezi kuacha kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombeni tusiwadanganye Watanzania. Tusiwadanganye waandishi wa habari, wasaidieni wandishi wa habari, sheria hii inakwenda kusaidia *journalists in Tanzania.* Mambo yote ya *printing* yameondoka, 20(3) ambayo yalikuwa yana tatizo yamendoka, kila ambacho kina tatizo kimeondoka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko rafiki yangu mmoja mwandishi wa habari alinipigia simu, ni rafiki yangu wa siku nyingi sana, nikamuuliza swali niambie Muswada huu una tatizo gani? Akaniambia umesoma kifungu cha 20(3)? Nikamwambia nimesoma kina matatizo tutakiondoa. Akasema mengine sina shida, lakini namwona kwenye *TV* anasema Mheshimiwa Serukamba jipu! Ndugu yangu, sasa jipu kwa sababu ya 20(3)? Bahati mbaya jipu lenyewe hili halitumbuliki, ndiyo bahati mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnajua Waheshimiwa Wabunge hawa jamaa walitaka tuuondoe Muswada na wakaamua kushirikiana na baadhi ya wenzetu kwamba, waje na *pressure* tutoe Muswada, ukiwauliza sababu hawana! Ukiwaambia kifungu gani kibaya, hawakisemi! Sheria kandamizi, sheria ya mwaka 28, sheria ya kikoloni! Hata rafiki yangu msomi Mheshimiwa Tundu Lissu anaongea hapa, twambie Mheshimiwa Tundu Lissu kifungu namba fulani kina matatizo, ndiyo kazi ya kutunga sheria. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mbona mmekataa *amendment?*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawaelewa, jana Mheshimiwa Sugu alisema hivi, naomba niwakumbushe. Rafiki yangu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi (Sugu) jana alisema maneno yafuatayo, alisema, naomba nisome tu najua Muswada huu utapita, Muswada huu utasainiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge wa CCM, tuongee ki-CCM, tufanye kazi hii kwa sababu tuko wengi. Naomba wana CCM tumfanyie kazi na Rais ametuambia wana CCM tumalize hii kazi, akasaini, tumalize leo. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kwa hiyo, ni Muswada wa CCM!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niwaambieni ukiona unaleta jambo zuri wanaokupinga wakasema zuri, ujue jambo lenyewe baya; ukiona unaleta jambo wale wanaokupinga wanapiga kelele, maana yake jambo lenyewe zuri. Maana ukiangalia wote waliosimama hapa, hata ambao walikuja kwenye Kamati wakachangia mawazo yao yakaingia, rafiki yangu Mheshimiwa Devotha hapa kuna mambo yameingia yalikuwa ni mawazo yake yeye, leo anayakataa hapa ndani! Hii ni nini? Hebu tufanye kazi ya kutunga sheria *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeweza kwenda kifungu baada ya kifungu, ningeweza kusoma vyote, lakini ninachoweza kusema Serikali imekuwa sikivu, tumefanya hii kazi, tumetunga sheria nzuri. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mkimaliza nitaendelea kusema, endeleeni kusema! Endeleeni tena!

**MWENYEKITI:** Endelea kuchangia!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Endeleeni tena!

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Endeleeni tena! Simama kabisa uchukue *Mic!*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa changia hoja!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalize kwa kusema, Waheshimiwa Wabunge leo tunakwenda kumaliza hii kazi, tutunge hii sheria, naomba tuunge mkono Serikali. Isingewezekana na niwakumbushe Wabunge wa CCM, hivi Wabunge wa CCM ni lini kitu kililetwa hapa ndani wale wakatuunga mkono, lini? Maana bajeti ya Serikali walikimbia! Bajeti za Mawizara walikimbia! Mlitegemea leo watuunge mkono humu ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutekeleze wajibu wetu. Bahati njema sana kwenye suala hili wengi ndio wanaoshinda, mtapiga kelele, lakini sheria itatungwa. Mtatutukana, lakini sheria itatungwa, wala haina shida tukaneni tu, lakini sheria itafanyaje, itatungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mchangiaji anayefuata, ni Mheshimiwa Juma Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru wewe, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha salama na kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwenye Muswada huu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niunge mkono Muswada huu kwa nia njema tu kabisa, kwamba Muswada huu haujaanza leo na hata Bunge lililopita ilikuwa uletwe hapa kwa Hati ya Dharura. Nami ni mmoja kati ya watu waliotoa mchango mkubwa sana kwenye maandalizi ya Muswada huu. Kwa hiyo, nashangaa sana hata inapofika wakati Mheshimiwa Nape Nnauye anasingiziwa, Mheshimiwa Nape Nnauye amekuta kila kitu kimeshaiva, alichofanya yeye ni kusogeza mezani tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Habari kwa kuhakikisha Muswada huu umekuja sasa ndani ya Bunge letu. Lakini pia niishukuru sana Kamati yetu ikiongozwa na Mhesimiwa Peter Serukamba kwa kazi nzuri tuliyofanya kuhakikisha Muswada huu na sisi tunatoa mchango wetu na Serikali ikasikia na ikafanya mabadiliko kadhaa ambayo naamini yatakuwa na tija kubwa sana kwa Taifa letu na waandishi wa habari wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni muhimu kwa nini, kwanza kutakuwa na Bodi ya Ithibati, pili kutakuwa na Baraza huru la Habari. Niliwahi kusema hapa siku moja  nikapambana sana na watu wa *MCT* niliposema

kwamba, *MCT* ni *NGO,* lakini sasa inaundwa Bodi ambayo inatambulika kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashangaa sana baadhi ya waandishi wa habari ambao wanaupinga Muswada huu, nadhani si akili yao, kuna mtu kawatuma. Kuna mtu kawatuma, lakini wanajua kabisa kwamba, anawatuma ili jambo lao lenye manufaa kwao lisiweze kufanikiwa. Naamini huu ndio utakuwa muarobaini kwa tatizo la waandishi wa habari hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu jirani yangu pale Mheshimiwa Tundu Lissu amezungumzia suala la *accreditation*. Mimi nimefanya kazi maeneo mbalimbali duniani, huwezi kwenda nchi yoyote bila kuwa *accredited* kama mwandishi wa habari. Kazi hii si ya kuchoma mkaa, lazima uwe *accredited* ili watu wakujue wewe ni nani? Si kazi ya kuchoma mkaa, unaweza kuingia msituni ukakata mti tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilishangaa jana kuna mtu mmoja nasikia hapa ndani akasimama akasema Mheshimiwa Nkamia ni kanjanja! Mimi sifanyi kazi ya kuchunga mashamba ya chumvi ya Viongozi wa Chama Cha *CUF* kule Lindi. Mimi ni mwandishi wa Kimataifa, eeh! Kwa hiyo, kabla hujaja humu ndani kusema ingia hata kwenye *google* kwanza, *google* huyu mtu ni nani? Siyo unatumwa na wewe unakuja hivyo hivyo! Eeh, rafiki yangu Mheshimiwa Bobali, usibebe jeneza bila kujua kafa nani! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu kwa waandishi wa habari. Elimu kwa waandishi wa habari ni jambo la msingi sana, lakini pia wanasema *journalism is an art*. Bodi na Baraza waachiwe wafanye kazi ya kuhakikisha kwamba mwandishi wa habari huyu ni nani! Waziri anapotunga kanuni, ningemwomba sana kaka yangu Mheshimiwa Nape anapotunga kanuni awashirikishe pia na watu wachache waweze kumpa *inputs* za kutunga kanuni kwenye suala la elimu kwa mambo ya uandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tido Mhando ambaye ni mwandishi anayepewa heshima kubwa, amemaliza *form four* tu, eeh! Ni *form four leaver,* lakini anaheshimika kwelikweli. Kwa hiyo, nilichokuwa nataka kusema hapa ni nini…

**MHE. MBUNGE FULANI:** *(Hakutumia kinasa sauti)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Subiri, usiwe na haraka. Ukitaka kula muhogo hakikisha una maji jirani, eeh! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nasema ni kwamba, sasa mnapotunga kanuni hakikisheni jambo hili mnaliangalia kwa makini sana. Sisi kwenye Kamati tumeliangalia na tumetoa ushauri wetu na nashukuru Serikali imelisikiliza vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Wamiliki wa Vyombo vya Habari. Jambo hili linaonekana si jema sana na watu wanajaribu kulizungumza sana huko nje kwamba, Muswada huu ni mbaya, ni mbaya, ni mbaya, lakini naamini kwamba, Wamiliki wa Vyombo vya Habari inawezekana pia wenyewe hawajausoma bali wanafanya kazi kwa kusikia maneno ya uchochoroni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Muswada huu utawasaidia waandishi wa habari *to the maximum* na tutawaheshimu sana wandishi wa habari na wao pia wataheshimika kuliko ilivyo sasa. Mtu akimwona mwandishi wa habari anajua huyu ni mtu mwenye njaa tu na ndio maana wengi wanadharaulika, lakini Muswada huu utasaidia sana kujenga heshima ya waandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu tunakosea sana, mwandishi wa habari ni raia kama alivyo raia mwingine. Sasa mtu akija hapa ndani akisema mwandishi wa habari apewe ulinzi, Wabunge wenyewe hawana walinzi, mwandishi atapewaje ulinzi? Lazima mwandishi na yeye ajilinde mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kuhusu wadau, tulipokutana kwenye Kamati wadau walipewa muda kwamba, walete mapendekezo, lakini kilichofuata walikuja wakakataa kuleta, kwa hiyo wamezira tu. Lakini mimi naamini kabisa kwamba wadau hawa wengi ni waajiriwa wa wamiliki wa vyombo vya habari kwa hiyo, inawezekana wengi wameogopa kuleta maoni yao wakiogopa mabosi wao! Ndio tatizo tatizo linapoanzia hapo tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naamini tuungane wote hapa sisi Wabunge wote; na ningeomba hata Kambi ya Upinzani hapa tulete hizi *amendments* tuweze kufanya marekebisho pale ambapo tunadhani panaweza kuwa na tija kwa waandishi wa habari badala ya kulalamikalalamika tu. Hata wenzetu Kambi ya Upinzani badala ya kuandikiwa hotuba na watu ambao wewe mwenyewe hujaijua vizuri unakuja kusoma hapa mbele, ni vizuri ukaandika mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini narudia tena, mimi ni mwandishi wa habari wa Kimataifa. Wale watu wanaolinda mashamba ya chumvi kule Lindi wanakuja hapa na elimu yao ya kuungaunga ya Ualimu wa *UPE,* wanakuja hapa wanasema Mheshimiwa Nkamia ni kanjanja waache, eeh! Kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Nasikia yuko *UDOM* anamalizia *degree!*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako.

**MICHANGO YA MAANDISHI**

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni hatari kwa Wanahabari na maendeleo kwa ujumla, umelenga kuondoa kabisa uhuru wa habari. Muswada unasema Mwandishi wa habari akipewa taarifa na Afisa wa Serikali kuhusu jambo fulani anaweza kushtakiwa Mwandishi pekee na si aliyetoa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, jambo la kutaifisha mitambo ya kutangazia au kuchapisha magazeti halipaswi kuungwa mkono. Waziri amepewa mamlaka ya kuelekeza nini chombo cha habari ki-*report* kwa wakati huo, hii itavinyima vyombo vya habari kukosa uhuru wa wake. Waziri au Serikali anaweza kuelekeza waandishi wote waandike habari hata za CCM pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria za Tanzania zinamzuia Mwandishi wa habari kupiga picha au kuandika chochote wanapokuwa gerezani. Pia wanazuiwa ku-*record* au kutangaza *live* wakati Mahakama inaendesha kesi. Sasa Je, kwa namna hii, Tanzania kuna uhuru wa vyombo vya habari? Tunataka sheria hizi kandamizi zifutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sheria hii mpya imwondolee madaraka makubwa Waziri wa Habari. Kwa mfano kifungu cha 54 - 55 amepewa mamlaka makubwa sana, hivyo nashauri badala yake Baraza la Habari ndilo liwe na mamlaka ya kuvionya na kukemea vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania si yetu sisi wana UKAWA tu bali ni ya watu wote, hivyo Chama Tawala wakilazimisha kupitisha Muswada huu wajue wazi hawatukomoi sisi wana UKAWA tu bali wanaukomoa umma wa Watanzania na wao pia, siku moja utawageukia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wa CCM kama kweli wapo hapa kwa ajili ya kula posho za vikao hata kama tungeandika mpaka tukatokwa na povu Muswada lazima upite tu.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, pamoja na timu nzima ya Wizara yake kwa kuleta Muswada wa Sheria ya Huduma za

Habari wa Mwaka 2016 *(The Media Services Bill, 2016)*. Taaluma ya habari ni mojawapo ya taaluma muhimu sana katika jamii yetu kwa kuuhabarisha umma mambo mbalimbali yakiwemo ya kisiasa, kiafya, kielimu na masuala ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taaluma ya habari ni tegemeo kubwa la jamii yetu na hivyo inahitaji *a high degree of trust;* na kwa kwa hali hiyo taaluma hiyo inahitaji kuaminiwa na jamii na pia kuwa na maadili ya hali ya juu. Napongeza Muswada huu kwa vile unalinda uhuru wa vyombo vya habari kuhakikisha habari zina ukweli na usahihi na pia Muswada huu unalinda utu na heshima ya kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada huu kwa vile unalenga kuhakikisha nchi yetu inaendeleza kupinga ubaguzi wa aina yoyote ile. Pia Muswada huu uhakikishe kwa namna yoyote ile unazuia vitendo vya rushwa kwa wanahabari na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taaluma ya habari ihakikishe inalinda umoja na amani ya nchi yetu. Kwa vile Tanzania ni sehemu ya dunia, hivyo Muswada huu uhakikishe kuwa unazingatia sheria na maadili mema yaliyo katika Miswada ya nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Muswada huu kwa kuishauri Serikali yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mwandishi wa habari kutoandika habari za kiuchunguzi au zile zilizoko mahakamani ni kuwanyima watu kupata habari za kina, kwani ni waaandishi wa habari ndio mara nyingi huibua uozo mwingi katika jamii na mara nyingi hata TAKUKURU hutumia taarifa hizi katika kufanya uchunguzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo napendekeza kifungu hiki kifanyiwe marekebisho kwani mara zote watendaji kwenye Taasisi za Umma utoaji wa habari ni wasiri sana, hawako wazi hata kwa habari za kawaida. Kuwepo kwa vyombo viwili katika sheria moja kutaleta mgongano wa kiutekelezaji kwani kazi za Bodi ya Wanahabari ingeweza kufanywa na Baraza la Wanahabari ambako ndiko kuna watu wenye taaluma ya habari, lakini si hivyo tu, kuwepo kwa wateule wa Waziri au Rais hakuwezi kukifanya chombo anachokiongoza kuwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu kwa mwanahabari aliyekutwa na kosa, kunyang'anywa leseni ili asifanye tena kazi ya uandishi wa habari ni adhabu kubwa sana. Lengo la adhabu hii si kutoa funzo ama kumrekebisha mtenda kosa, adhabu hii inakusudiwa kuwatia woga wanataaluma hawa wasifanye kazi kwa uhuru, hivyo kushindwa kuibua maovu yatakayofanywa na watu wenye mamlaka makubwa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema hayo mambo yanayotajwa kama ni mambo ya siri, uchochezi, uhuru binafsi, faragha yakawa wazi kwani watu wenye mamlaka wanaweza wakatumia mwanya huu kuwazuia waandishi kupata habari kwa kigezo kuwa ni siri na mambo mengine kama hayo. Vilevile kitendo cha masharti ya leseni kuachwa kwa mtu mmoja (Waziri) kunaweza kuwafanya watu wengi kukosa au kufutiwa leseni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uingizaji wa machapisho nchini. Mamlaka aliyopewa Waziri katika kifungu hiki yasipofanyiwa marekebisho Waziri anaweza akayatumia vibaya. Hivyo mamlaka hayo yakabidhiwe kwenye Bodi ya Huduma ya Habari/Baraza la Habari kuepuka Waziri kuzuia machapisho kwa maslahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makosa Mbalimbali; mtu aliyefanya kosa kwa makusudi kumpa adhabu sawa (moja) na mtu aliyefanya kosa kwa uzembe si sawa kwani huyu wa pili hakukusudia kufanya kosa, hivyo adhabu ni bora zikatofautiana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 20 (2) kabla ya Mwandishi wa Habari kuondolewa au kukoma kuwa Mwanahabari kwa kosa lolote atakuwa amekiuka sheria hii, ni lazima kuwepo chombo huru kitakachothibitisha pasipo shaka kuhusu adhabu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 20(3) Mwanahabari aliyepatikana na kosa apewe fursa ya kukata rufaa pia apate fursa ya kujitetea kwenye chombo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 14(1) maneno kwa idhini ya Waziri yaondoke na badala yake yawekwe maneno kwa kushauriana na Waziri wa Habari. Ni vizuri sana na muhimu Bodi ya chombo hiki ikawa huru bila kuingiliwa majukumu yake, wala kuamuliwa nini cha kufanya ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ianishe wazi kwenye Bodi uwiano wa wajumbe wanawake na wajumbe wanaume ili mawazo yanayowagusa wanawake yapate nafasi kwenye Vyombo vya Habari na kwenye jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 7(2) ni vizuri habari zinazoandikwa zisihatarishe usalama wa nchi. Swali muhimu hapa ni chombo gani kinachothibitisha kwamba, habari iliyoandikwa inahatarisha usalama? Isije kutokea mtu mmoja tu akaibuka na hoja itakayokandamiza uhuru wa habari. Hivyo, ni vizuri sheria iainishe wazi chombo kinachothibitisha habari na kiwe huru.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha tatu, maana ya maneno, Chombo cha Habari za kielektroniki kunamaanisha na mitandao ya kijamii na njia nyingine zinazoendana na hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kwa kusoma itahusisha ma- *group* ya kwenye mitandao, *facebook, messenger na blog* na nyingine kama hizo zinazotumika kutoa taarifa kuwa zitaitwa vyombo vya habari na kufuata masharti kama ya vyombo vingine. Ku-*include* vyombo hivi ni kuminya kwa kiwango kikubwa uhuru wa kupata habari kinyume na Katiba 18(d). *Blog* hizi na *group* hizi zinahitaji kupitia *process* zote kama kupata leseni, Kifungu cha nane (8), hii ni kuendelea kuminya uhuru wa watu kupata taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 11; Wajumbe wa Bodi kuteuliwa na Waziri ni kuondoa kabisa uhuru wa Bodi na hii haioneshi nia njema kwa uhuru wa Vyombo vya Habari. Mheshimiwa Waziri ajiondoe kabisa katika uteuzi na badala yake nafasi hii igombewe na Kanuni ziandaliwe, mtu mwenye sifa apatikane kuongoza Bodi na nafasi nyingine zijazwe kwa mtindo huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 20(3), inayotaka Mwandishi kuacha kufanya kazi hii atakapopokonywa kitambulisho au kufutwa kwenye orodha ya Waandishi. Mheshimiwa Waziri, huku ni kukariri. Waandishi hawa wamegawanyika katika nyanja mbalimbali; anaweza kukosea katika kuandika akaenda kutangaza. Hii siyo haki kabisa kwa taaluma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona Mawaziri wanaweza kuharibu Wizara moja na kupelekwa sehemu nyingine? Tusikomoe watu kwa kuwa tuna mamlaka ya kutunga sheria juu yao. Katika taaluma nyingine kama Udaktari huwa wanafungiwa ili madhara hayo yasijitokeze tena na yanakuwa *irreversible*, hapa kwenye Uandishi wa Habari hali iko hivyo? *Let's be fair.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 32, mambo yenye kashfa. Tutambue hii ni nchi ya kidemokrasia ya Vyama Vingi na watu wenye mawazo tofauti. Kama tunaamua kufunga watu midomo kwa madai ya kuandika uchochezi tunaenda kuliangamiza Taifa, kwani kuwaza kwamba tunaweza kuwafunga watu midomo, sawa, lakini tutambue haiwezi kuwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 50, makosa ya uchochezi, Kifungu cha 51, kutia hofu na uwoga kwa jamii. Vifungu hivi vimelenga kudhibiti nia au kusudi la kutoa maoni tofauti na watawala wanachokifuata.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umechukua zaidi ya miaka 20 kufika hatua hii ya leo kujadiliwa Bungeni. Waziri alikuwa na nia njema kuwashirikisha wadau wa Tasnia ya Habari kutoa mawazo yao. Ni bahati mbaya Muswada huu haujasheheni mawazo ya wadau wa habari. Hakukuwa na ulazima wa kuingiza Bungeni haraka hivi ukiwa haujachangiwa na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5(e); Kutoa Leseni kwa Machapisho. Kifungu hiki nashauri kifutwe na badala yake msajili wa magazeti aendelee na kazi ya kusajili magazeti kwa sababu kuna hatari ya leseni kutumiwa vibaya kuvinyima vyombo vya habari haki ya kuchapisha.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 50(2 -11), vifungu hivi vinaadhibu wasomaji na wachapishaji wa magazeti. Nashauri vifungu hivi vifutwe vyote, vifungu hivi vinatishia maisha ya wasomaji na uwekezaji katika mitambo ya uchapishaji kwa kumpa ruhusa Mkuu wa Jeshi la Polisi kukamata na kuharibu mitambo.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Muswada wa Sheria ya Habari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuundwa kwa ithibati ya wanahabari. Hii itasaidia kuwezesha tasnia hii ya habari kuheshimika kama ilivyo bodi za taaluma zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza hisa zaidi kwa wamiliki wa vyombo vya habari kwa Watanzania 51% na wageni toka nje 49%. Hii itasaidia sana uimarishwaji wa ulinzi kwa nchi na kupunguza habari zisizo za kweli kwa Mataifa ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bima ya afya. Muswada huu wa sheria unatoa umuhimu wa bima ya afya kwa wananchi wote na itawasaidia wakati wanapopata matatizo wakiwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri. Ningependa kushauri kuwa pamoja na umuhimu wa Muswada huu, ni vizuri tukazingatia umuhimu wa kuandika kanuni mapema ili baada ya Mheshimiwa Rais kusaini, sheria hii ianze mapema kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada huu.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Bodi ya Ithibati, bodi hii imependekezwa kwenye kifungu cha 10(1) cha Muswada. Binafsi naona haijahusisha wadau kwa upana zaidi hasa kwa kuwaingiza wanahabari na wamiliki wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri wajumbe hao saba wachaguliwe na wanahabari na Waziri awapitishe. Waziri kapewa majukumu makubwa sana hata kuna maneno "Idhini ya Waziri" yaliyopo kwenye kifungu cha 14(1) na badala yake kuwepo na kifungu cha 14(3) ambacho kinasema "Waziri anaweza kuagiza bodi kurudia mchakato wa kuchagua Mkurugenzi Mkuu ikiwa kutakuwepo na uvunjifu wa kifungu 14(2).

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huduma za habari ni muhimu sana katika kuhabarisha jamii katika masuala mbalimbali yanayohusu maisha ya watu katika shughuli zao za kila siku. Kwa hiyo, katika kuhabarisha jamii lazima ziwepo sheria ambazo zitalinda haki ya mwananchi. Hii itasaidia kutooneana katika utoaji wa habari. Ipo tabia ya kuchafua watu bila kufuata sheria.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali na Wizara ya Habari kwa kuleta Muswada huu ili kufanya marekebisho ya baadhi ya vifungu vya sheria ambavyo haviendani na mazingira ya siku hizi. Mwandishi wa Habari lazima awe na taaluma ya habari ili aweze kutoa habari ambayo ina *quality* ya habari. Kwa mfano, unatoa habari inayohusu masuala ya uchumi wa nchi, lazima uwe na uelewa au elimu ya uchumi ili usiweze kupotosha habari inayohusiana na suala hilo la uchumi wa nchi ambayo unaitolea habari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mwandishi wa Habari lazima awe amesoma masuala ya Uandishi wa Habari, pia kujua kanuni na Sheria ya Habari. Habari lazima izingatie haki za binadamu ili kuhakikisha utu wa binadamu unalindwa. Ili wananchi kupata habari sahihi inayohusiana na taarifa ya jamii katika maeneo ya kisiasa, elimu, kiafya, kiuchumi na kijamii lazima taarifa au habari iwe na usahihi ili kuepuka upotoshaji ambao unaweza kuhatarisha usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa kuwa vyombo vya habari ni vya muhimu sana katika kuhabarisha jamii katika masuala mbalimbali, lakini kwa kufuata Sheria ya Habari ambayo imetungwa na Bunge kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa Muswada wa Mabadiliko ya Tasnia ya Habari kuelekea kuwa muhimili wa nne. Kifungu cha (7), wajibu na haki ya *media* lengo ni kuimarisha *National Security*. Kifungu cha 8(1) kwamba kutakuwa na leseni ya kuchapisha ama kuuza. Hiyo itasaidia kuongeza uwajibikaji, kufanya tathmini kila mwaka, ni *source* ya *revenue* na pia itaongeza uadilifu.

Kifungu cha 14(2) kuhusu sifa za *Director General,* naomba tuongeze awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha (1) kuhusu Mfuko wa Mafunzo ya Habari, mafunzo ya wanataaluma ya habari, kukuza na kuendeleza *program* na kuongeza utafiti. Naipongeza Serikali kwa kifungu hiki kwani kitasaidia kuwafanya wanahabari waende na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 23 kuhusu Baraza Huru la Habari; mwanahabari aliyethibitishwa atakuwa mwanachama, utakuwa na uwezo wa kujisimamia, italetea haki ya wanahabari. Vile vile Baraza hili litakuwa na uwezo wa kuishauri Serikali na kusimamia vyema tasnia ya habari.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 7(1)(b)(iv) - Serikali kuelekeza vyombo vya habari kuhusu jambo la kutangaza. Hii inaingilia uhuru wa habari. Serikali ingejikita kuelezea *issue of National importance,* ni zipi? Akija kutokea kiongozi wa nchi asiye na uadilifu, atatumia kifungu hiki vibaya. Mfano Mkuu wa nchi anaweza kusema *birthday* yake ni *National importance*. Kifungu kifutwe.

Kifungu cha 32(2)(3) kinasema, maiti anaweza kukashifiwa *(defamation in print media)*. Kwa kawaida kashfa imemgusa mhusika mwenyewe, hivyo maiti haiwezi ku-*feel* kashfa au udhalilishaji. Kifungu hiki kifutwe kwa sababu maiti haikashfiki na wala haina uwezo wa kutoa ushahidi wa kashfa husika.

Kifungu cha 33(1) katuni *(effigy)* zinaigizwa kwenye dhana ya kashfa. Duniani kote katuni ni kiburudisho kinachowasilisha ujumbe kwa njia ya burudani na dhihaka na dhana hii imekubaliwa duniani kote. Hivyo, Tanzania itakuwa ya kwanza kuingiza katuni katika dhana ya kashfa. Hivi Watanzania hawawezi kucheka au kuendeleza utamaduni wa utani wa asili? Kifungu kitanyima haki ya watoto kupewa kusoma magazeti ya katuni, kuangalia TV zenye vipindi vya katuni. Katuni zinafundisha watoto lugha ya Kiingereza, maadili na maonyo mbalimbali? Kifungu hiki kifutwe.

Kifungu cha 50(2) - (11); vifungu hivi vinaadhibu wasomaji na wachapishaji wa magazeti. Vifungu hivi vimetishia maisha ya wasomaji na wawekezaji katika mitandao ya uchapishaji kwa kumpa ruhusa Mkuu wa Polisi

au Maafisa wa Jeshi hilo kukamata na kuharibu mitambo ya uchapishaji na kukamata wananchi watakaokutwa na yanayodaiwa kuwa machapisho ya uchochezi. Hii italeta hofu na mtafaruku mkubwa nchini usio wa lazima. Kifungu hiki kifutwe.

Kifungu cha 55 kuhusu mamlaka ya Waziri kuzuia uchapishaji wa baadhi ya habari; Waziri hana haja ya kupewa mamlaka haya, kwani tayari habari zinahusu usalama wa Taifa, zinaangukia chini ya kifungu cha 72(a) (i) kinachozuia uchapishaji wa habari za aina hii na adhabu yake iko wazi katika Muswada huu. Kifungu hiki kifutwe.

Kifungu cha 56 kinatoa nguvu kwa Polisi na Mkurugenzi wa Idara za Habari, Maelezo kukamata mitambo. Dhana ya kukamata na kuharibu mitambo imetawaliwa katika kifungu cha 50. Kifungu hiki kifutwe.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Mawaziri, tunaanza na Mheshimiwa Januari Makamba dakika kumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe naye dakika kumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuanze na kitu gani ambacho hakipo kwenye mjadala. Jambo ambalo halipo kwenye mjadala leo ni umuhimu wa vyombo vya habari na umuhimu wa waandishi wa habari. Kwa sababu nimeona naona jana tumetumia muda mrefu sana kuzungumza kuhusu umuhimu wa vyombo vya habari na umuhimu wa waandishi wa habari, sote tunakubaliana katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wameenda mbali kwa kulinganisha waandishi wa habari sawa na taaluma nyingine, Madaktari, Wahandisi, nami nakubaliana na hilo, kwamba kwa hapa tulipofikia kwa umuhimu wa taaluma ya uandishi wa habari, kwa umuhimu wa tasnia ya habari katika ujenzi wa demokrasia, umuhimu wake ni sawa na taaluma zile nyingine ambazo tunazitaja kwamba, ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukishakubaliana hivyo kwamba, uandishi wa habari ni taaluma muhimu kwa vyovyote lazima tukubaliane kwamba, lazima kuwe na udhibiti wa Serikali katika taaluma hii na tasnia hii muhimu kwa sababu, huwezi kusema kwamba, uandishi wa habari ni muhimu sana sawa na uhandisi lakini ukaishia hapohapo. Kwa maana hiyo basi, tasnia hii, taaluma hii iendeshwe shaghalabaghala bila udhibiti mahususi, bila kuwepo na mamlaka na sheria inayoweka viwango. Kwa hiyo, sheria hii imeenda kutekeleza hisia

zetu, kwetu sisi, tasnia ya habari ni muhimu kwa nchi yetu, ndiyo maana tumeweka udhibiti, tumeweka viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda turudi kwenye dhana ya udhibiti kwa ujumla. Hapa kihistoria katika nchi yetu kuna baadhi ya huduma na biashara ambazo zimekuwa zinadhibitiwa na msingi wa udhibiti huo ni maslahi mapana ya jamii kutokana na shughuli zile. Kwa mfano, tunadhibiti huduma ya mawasiliano, tunadhibiti dawa, tunadhibiti shughuli nyingine muhimu; sasa msingi wa udhibiti wa tasnia hii ni kwamba, ipo njia panda kati ya huduma kwa demokrasia kwa upande mmoja, lakini vilevile biashara kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandishi wa habari na tasnia ya habari inatoa huduma kwa demokrasia ya nchi yetu, lakini wakati huohuo ni biashara vilevile. Kwa hiyo, hii dhana ya kuachia *self regulation* wakati kuna hatari kubwa kwamba, ile *self regulation* inaweza ikatumika vibaya na maslahi ya kibiashara yakachukua nafasi kubwa zaidi katika udhibiti kuliko huduma kwa demokrasia. Ndiyo maana tumeamua kwamba, Serikali angalau kwa sasa ndiyo ambayo ipewe nafasi ya kuweka viwango, kwa hiyo hii ni muhimu kufahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi ambazo zimeendelea katika tasnia ya habari zilishajaribiwa namna zote, kule Marekani, Uingereza kwa mfano, kulikuwa na kitu kinaitwa *Press Complaints Commission* ambayo ilikuwa ni chombo cha *self regulation* katika tasnia ya vyombo vya habari, tasnia ya magazeti, lakini tunafahamu miaka karibu 16 iliyopita kile kitu kilivunjwa. Kilivunjwa kwa sababu, kilishindwa kuweka *balance* sahihi kati ya maslahi ya kibiashara ya wenye vyombo vya habari na maslahi mapana ya umma na kikaanzishwa chombo kingine mahususi kabisa madhubuti ambacho kiko chini ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti,vile vile katika nchi ya Norway ambayo wote tunaisifia kwamba ni nchi ambayo imeendelea kidemokrasia, inajali haki za binadamu, kwenye Wizara ya utamaduni na mambo ya kanisa (*Ministry of Culture and Church Affairs)* kuna kitu kinaitwa (*Norwegians Media Authority),* chombo cha Serikali, ambacho kinatoa leseni, kinadhibiti ubora, kinasema nani anunue chombo kipi na kwa kiasi gani; yote ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba jambo hili linaendeshwa kwa namna nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kwamba Mheshimiwa Lissu, hapa ametoa historia kwamba wakati wa chama kimoja, wakati vyombo vyote vya habari vinamilikiwa na Serikali, wakati hakuna magazeti mengine ya binafsi kulikuwa tayari na *accreditation* ya waandishi wa habari. Sasa anachotuambia ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachotuambia ni kwamba; ithibati haina uhusiano na kuminya demokrasia au kuminya sauti. Kama wakati wa chama kimoja ambapo hakukuwa na ushindani wala upinzani bado Serikali iliamua kuwe na viwango katika tasnia hii, dhana ni ile ile, kwamba kinachotakiwa hapa ni kuwa na viwango sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaposema kwamba sasa hivi Serikali inalileta jambo hili kwa sababu inataka iminye waandishi, au iminye tasnia ya uandishi inaenda kinyume na historia ambayo ameitoa mwenyewe kwamba hata huko nyuma jambo hili lilikuwa linafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ningekuwa mwandishi wa habari, katika kutazama sheria hii ningejiuliza mambo mawili. Kwanza *liability* yangu katika shughuli yangu iko wapi, pili, je, sheria iliyowekwa inaruhusu au hairuhusu kwa kiasi gani watu kuivamia tasnia hii na kuiondoa thamani? Sasa uzuri wa sheria hii ni kwamba inatenganisha *liability* kwa kila kundi. Mwandishi *liability* yake iko peke yake na makosa ya mmiliki au mchapishaji hayawezi kuchukuliwa na mwandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sheria nyingi za namna hii, huu ni ubunifu mkubwa kwenye sheria yetu kwa sababu unamlinda mahsusi mwandishi wa habari asiingie kwenye *liability,* asiingie kwenye matatizo kwa sababu ya makosa ya mtu mwingine. Ingekuwa mimi hili jambo lingekuwa la kusherekea na kufurahia na la kupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, nadhani wenzetu, rafiki zetu ambao tunafanya nao kazi sisi kama Serikali, kama Chama Tawala, waandishi wa habari, ningependa na kufurahia utaratibu ambao unakinga hii taaluma isivamiwe na watu ambao wanaiondolea sifa. Sheria hii ndicho chombo kinachoweza kwa sababu sifa na heshima ya uandishi wa habari inaondolewa na watu wachache sana ambao hakuna sheria wala taratibu za kuwazuia wasiingilie. Kwa hiyo, ningekuwa mimi, ningefurahia *exclusivity* katika hii shughuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia, *best practices* za jambo hili duniani kote, mwaka juzi Kenya walipitisha sheria wakaweka na dhamana kabisa *(bond)*, kwamba ukitaka kuanzisha chombo cha habari unaweka fedha nyingi chini, ili pale utakapokutwa na makosa ikitoka *judgment* ile fedha inachukuliwa. Hapa sisi hatukuamua kufanya hivyo kwa sababu tuliona kwamba ni vyema watu wote wanaotaka kuingia kwenye biashara hii wapate fursa ya kuingia kwenye biashara hii bila kuwa na vikwazo, bila kuwa na upinzani wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani na naamini kwamba umefika wakati sasa kwenye baadhi ya mambo tukubaliane kama Taifa, kwamba lazima shughuli hii ambayo inaathiri sana maisha ya watu, uendeshaji wa demokrasia yetu lazima iendeshwe kwa utaratibu murua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma yalifanyika makosa ambapo haki za watu na nimshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Zitto amesema yeye amekuwa mhanga mkubwa sana wa kuandikwa na kutukanwa na yeye anadhani ni sawa na ni sahihi, lakini kwa watu wengine ambao si wanasiasa, ambao hawako kwenye shughuli yetu sisi ambao tumezoea kusemwa na kutukanwa, uvumilivu wetu na nafasi yetu ya kuvumilia matusi tusiihamishie kwa watu wengine ambao hawana hatia wala hawana makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumalizia nampongeza sana Waziri, kwamba ametengeneza historia kwa kutuletea sheria nzuri. Naamini kabisa tasnia hii ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Sisi tunapenda na tunategemea waandishi wa habari na uandishi wa habari kwa maendeleo na demokrasia ya nchi yetu, hakuna namna ambayo Serikali hii inaweza kuminya uhuru wa habari. Kama kuna kitu ambacho Serikali hii inataka ni kupata msaada wa waandishi wa habari katika kupambana na rushwa na ufisadi na maovu yote katika jamii kwa sababu wao wana nafasi kubwa ya kuweza kuisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii itawezesha waandishi wa habari waisaidie Serikali, wamsaidie Mheshimiwa Raisi wetu na chama chetu katika kuijenga jamii yetu upya na kujenga jamii nzuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, hongera sana na naamini kwamba tutaipitisha sheria hii na huko mbele kama kutakuwa na marekebisho tutayafanya yanapostahili, lakini kwa sasa kwa ilivyoandikwa ni nzuri na inastahili kupitishwa .

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na vile vile Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Naomba niseme mapema kabisa naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa Nairobi si kawaida kumwona mtu ananunua au ameshikilia magazeti mawili, matatu, manne ya kusoma atakuwa pengine na *Daily Nation*, *The Standard*, au Taifa leo. Ukiangalia sana unabaini kwamba magazeti hayo yanajitosheleza, yanatoa kiu yake yote kwa gazeti

moja moja, si lundo la magazeti. Ukienda Uganda, nenda Kampala utakuta mtu anasoma *The Monitor*, au *The Daily Mirror*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nakaa Ujerumani na wenzangu watatu, mwenzangu alikuwa anasoma Dzus Deutsche *Zeitung*, mimi nilikuwa nasoma *Frankfurter Allgemeine Zeitung,* ni magazeti ya kijerumani, lakini uwezi kwenda upande wa pili, kwa sababu yanajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania si kawaida kumkuta mtu ananunua gazeti moja, lazima ununue sita ili upate angalau picha ya kilichotokea ni nini katika nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba zipo sababu. Sababu ya kwanza magazeti yetu yako kibiashara sana, kurasa 16 kurasa 20, mwisho 40 ndiyo magazeti makubwa kabisa mawili siyataji. Sasa mtu anasoma bado ana kiu ya kujua, matangazo kwenyewe ni nusu ya gazeti zima. Lakini pili naweza kusema yapo mashaka ya wasomaji kupata *accurate information* kutoka kwenye magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, niliwahi kusema kwenye Bunge hili nilishambuliwa zaidi ya miezi sita lakini imezidi kuniimarisha na niko tayari kwa hili lakini nataka kusema kwamba tuna *crisis* ya weledi wa uandishi wa habari katika nchi hii na ni lazima tukubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *crisis* tumeilea sisi wenyewe mpaka kufikia hapa, sasa muda umefika tunamalizane na hii *crisis* na huu Muswada unatupa hiyo *solution*. Naomba niseme, ukweli tuna waandishi wazuri wenye weledi *(world class)* wachache katika nchi, lakini wengi hawana ueledi *completely*, sisi wote ni viongozi hapa. Unahutubia mkutano, umemaliza unatoka unafuatwa na waandishi hivi ulitaka kusema nini, tunaomba utuelezee vizuri. Huko ni kukosa ueledi katika *journalism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kuona kitu kama hicho, hakitokei dunia nyingine, ni Tanzania tu. Unaongea kwenye mkutano bado unafuatwa ulitaka kusema nini pale, lakini umeongea Kiingereza pale, naomba Kiswahili, ina maana hatuko tayari kufanya kazi ya uandishi, tumewaweka watu ambao hawafai katika hii tasnia, hii tasnia inaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona aibu sana, anakuja mgeni kutoka nje, mwandishi wa habari anatoa *not book* yake, *your name please! Write here!* Katika *proper journalism* hiyo ni aibu haijapata kutokea duniani, leo hali ni mbaya. Mheshimiwa Nape Nnauye nikushukuru sana mwenzako kwa kututetea huu Muswada. Mwandishi wa habari anakuja unamwona kabisa midomo imepauka, huyu kijana hana mshahara, hana bima, anategemea *source* impe

nauli kurudi ofisini. Hatutakuwa *serious* katika *journalism* tukifanya hivi. Jamani tuache kupakana mafuta ya uongo, hali mbaya na hii hali mbaya tui-*sort out*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi wa Chuo cha Uandishi wa Habari, tena Mwenyekiti wa mwisho, nikahamishiwa niende Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Nilipokuwa pale wananchi kwa mamia wanakuja kuniomba nafasi vijana kusoma au niwatafutie kazi. Anakuja mzazi, Mwenyekiti, mtoto amefeli darasa la saba, naomba angalau umtafutie nafasi ya uandishi wa habari, mtoto wangu amefeli *form four* basi angalau kazi ya uandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani uandishi wa habari wanakwenda watu ambao wameshindwa katika maeneo mengine yote, ndiyo lilikuwa *mentality* ya hiyo, tutoke huko, uandishi wa habari *is a profession*. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tusilewe na hizi propaganda za hawa *intellectual* wa ki-*liberally* hasa wengi kutoka Marekani kwamba waandishi wa habari *is not professional at all*. Hapana, fani yoyote ambayo inakulazimu ujikite kusomea maadili yake, miiko, kanuni zake *is a profession*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo haiwezekani ukasema kwamba kila Mtanzania, unajua pengine niseme tu kidogo kwamba kila mtu ni huru katika nchi hii kuvaa joho lolote hata joho jeupe, lakini si kila mtu anayevaa joho jeupe ni Daktari, anaweza kuwa mfanyakazi wa bucha, lakini kumtofautisha huyo na daktari, madaktari wana-*undergo specialize training* na wakishafuzu wana maadili, miiko na taratibu zao na ndiyo maana lazima kuwe na *accreditation,* mimi ni Daktari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanasheria kila mtu ana uhuru kusoma sheria lakini si kila mtu aliyesoma sheria ni Mwanasheria, na si kila Mwanasheria ni Wakili na ukishakuwa Wakili lazima tu ku-*identify*, tuku-*distinguish* na wengine, kuna *accreditation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu anaweza kuwa mwandishi wa habari, haiwezekani ila kila mtu ana haki kikatiba kutafuta habari, kupokea na kutoa kwa mtu mwingine, hiyo sawa, unampa mke wako, mjomba, lakini pale ambapo unakusanya habari ili utawanye kwa wengine, *at a fee, regulation* inabadilika. *Is not just a question of passion* ya kukusanya habari ni *expertise*, unaenda kwenye chuo cha habari unakuwa *trained, I have an advance diploma in journalism here,* naelewa ni kazi unasoma, sasa siyo tu kwamba unakaa tu pale, ni uandishi. Sasa ukishafika hapa *rules of the game* zinabadilika lazima uwe *accredited* wewe ni mwandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembea duniani kote sijawahi kuona waandishi wa habari ambao si *accredited*, ni wapi? Wamarekani wasitudanganye sana jamani, unajua ndiyo walikuwa wanaendesha hii *liberalism*, nimekaa nao sana kwenye *USIS*, nikiendesha semina zao huko. Wanapenda sana kusema hivyo, lakini wale watu siyo wa kuwaamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekani imepata Katiba 1787, Mmarekani huyo huyo miaka 68 baadaye 1865, akabadilisha katiba ikifuta utumwa Marekani. Miaka mitatu baadaye ikim-*declare* kila mtu aliyezaliwa Marekani n Mmarekani ana haki sawa mbele ya sheria. Imewachukua miaka 100 mtu mweusi kupiga kura, miaka 100 mtu mweusi kutambuliwa kama ni binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sisi tumepata uhuru mwaka 1961, *we are more advanced,* tujiamini Watanzania, mwaka 1961 tumepiga kura, kila mtu anapiga kura, Serikali yetu ya kwanza kuna wazungu ndani akina Dkt. *Leader Starling*, Bryson, tuna wahindi akina Mzee Jamal, *a mult cultural Nation*, kwa hiyo sisi tuna *experience* zaidi kupita hawa tunaowanukuu nukuu *as if* kwamba wao ndiyo wanatuzidi kwa kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekani leo hii kati ya majimbo 50, majimbo 28 yana sheria kali kweli kuhusu uandishi wa habari. Ukifanya upuuzi *deformation* ni *up to five thousand dollar,* lakini kifungo ni *up to five years* kwenda jela. Lakini wakija huku, aaa! *Liberal press* na sisi tunaimba *liberal press,* hakuna cha *liberal press* hapa, hakuna uhuru usio na mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema, kuna suala hili *la accreditation* alilokuwa anaongelea hapa mdogo wangu Tundu Lissu, ni kweli, amejenga hoja kisomi lakini ana-*miss point* moja kubwa. Sisi kwenye Serikali tuliamini kabisa katika *regulation* ya *media profession* na ndiyo maana mwaka 1995 tukaanzisha *Media Council of* Tanzania ambayo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba kuunga mkono. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa tunaelekea kuhitimisha hoja hii, tuna Dkt. Possi, dakika 10, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu dakika 10, Naibu wa Wizara hii dakika 10 na mwenye hoja mwenyewe nusu saa. Karibu Mheshimiwa Dkt. Possi

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kusema naunga mkono hoja na nataka kusema maneno machache. Nitafafanua ile dhana inayoongelewa kana kwamba uhuru wa habari ni *absolute*, ni *limit less,* kwamba hauna mipaka yoyote ile. Ila nianze tu kwanza kwa ujumla kwa dhana nzima ya haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe ni mtu wa haki za binadamu, naamini huko, lakini tuna nadharia mbalimbali, wapo wanaosema haki za binadamu ni *absolute*, hazina mipaka, lakini wapo wengine wanaosema kuna mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja wa jumla sana, unaweza usihusiane na uandishi wa habari. Kuna watu wanasema katika nadharia hiyo hiyo ya haki za binadamu, basi mtu atakuwa na haki pia kuwa na mapenzi ya jinsia moja, lakini hatakuwa na haki ya kuoa wake wawili upande mmoja. Upande mwingine wa dunia kuna watu wanasema aaa' unaweza ukaoa wake wawili lakini hiyo ya mapenzi ya jinsia moja hatutaki kwa sababu ni kinyume na utamaduni wetu na sisi tuna haki zetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wengine wakaenda mbali sana, katika dunia hii ambayo watu wana *interest* tofauti huwezi ukawa una mipaka kwa sababu unaweza ukajikuta haki yako moja inavuruga haki ya mtu mwingine. Sasa na hilo linajikita katika nadharia nzima ya sheria, wapo wasomi wa zamani wanasema pale ambapo hakukua na sheria binadamu alikua anaishi katika *state of confusion, state of anarchy,* kwamba kila mmoja anafanya analotaka matokeo yake na usalama unapungua. Sasa katika mambo hayo yote mawili lazima kuwe kuna *balance* kati ya haki pamoja na mipaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika dhana ya uhuru wa habari. Nafahamu katika ibara ya 18 ya Katiba, lakini bahati nzuri Katiba yetu ukiisoma ile sehemu ya haki za binadamu *(Bill of rights)* lazima uisome na kifungu cha 30(1) (2), maana yake nini? Haki zote zilizokuwemo mle ikiwemo haki ya habari ina- *certain restrictions*. Moja ya *restriction* hizo ni kuangalia masuala yanayohusu maadili *(morality),* usalama wa nchi, lakini haki za watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki hakikuja kwa bahati, tayari hapo maamuzi ya Mahakama Kuu yanasema Tanzania kwa sababu ilisaini Mikataba mbalimbali ya Kimataifa, basi ninavyotafsiri katika hii ni vizuri kuangalia na Mikataba mingine ya Kimataifa inasemaje, mimi nitaangalia Mikataba miwili lakini pia nitaangalia Azimio moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba hii miwili ni Mkataba wa Haki za Binadamu wa Afrika *(the African Chart of Human and People's right),* lakini Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kisiasa na za Kiraia. Kwa sababu mikataba hii ina chanzo katika *Universal declaration of human rights* ambayo wataalam wanasema ni azimio ambalo lina desturi za sheria za kimataifa nitakuja huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *the African Charter* kweli inaonesha Ibara ya 9(1), uhuru wa habari. Ukiangalia ibara ya 27(2) inazungumzia kuhusu *limitations,* ukienda ibara ya 29 moja ya uwajibu ni watu kutokufanya mambo ambayo yatahatarisha usalama wa nchi zao wenyewe. Nasema hivi kwa sababu kuna watu walikuwa wanazungumzia mambo ya uchochezi na nini, tutakuja huko baadaye. Mambo haya pia yanajitokeza katika ibara ya 19(3) ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kiraia, lakini pia na Ibara ya 20 ya mkataba huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema haya yana asili yake katika Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, kwa hiyo ukizisoma ibara ya 18 na ibara ya 30 utagundua kwamba kila haki ina mipaka yake. Sasa kwa nini kuna mipaka? Huwezi ukasema kwa sababu kuna uhuru wa habari, basi mtu aandike aseme sasa watu wachinjeni watu wa kabila fulani, sasa ni wakati wa jeshi kupindua nchi; haiwezekani, haiko hivyo Marekani, haiko hivyo Urusi, haiko Uingezereza, haiko Tanzania na haitakuja kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo tu la *public or state interest* tuangalie mfano unaoendelea leo. Leo ukiangalia *CNN* ya Marekani au ukiangalia *ABC* wanavyoelezea wao kuhusu vita ya Syria ni tofauti kabisa na inavyoelezewa kwenye labda *Russian Television,* kila mmoja anaelezea kutokana na *state interest.* Sasa sisi ni watu gani ambao hatujui *state interest* na hatutaki ku-*protect our state interest* kupitia *media*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikumbushe kitu kimoja kabla sijasahau Mheshimiwa Tundu Lissu alituongelea hapa kuhusu Nyalali *Commission.* Bahati nzuri ripoti tunayo hii hapa na tukaangalia ukurasa wa 48 na ukurusa wa 49. Ukurasa wa 48 ulikuwa unazungumza kuhusu *News Paper Act,* mapendekezo, akasema tu kwa mfano *the Act be amended according to allow more freedom of the press and expression and relaxation of censorship of information*, nitatafsiri baadaye. Ukurasa wa 49 ulikuwa unazungumzia kuhusu *Tanzania News Paper Agency* Na. 14 ya mwaka 1976.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Okay, the monopoly of the news correction and dissemination (SHIHATA) should be abolished, the provisions of the Act that violate freedom of the constitution and press should be repealed.* Sasa haya ndiyo yalikuwa mapendekezo, wapi waliandika kuhusu *accreditation?*

Mheshimiwa Tundu Lissu wapi waliandika kwamba vifungu vyote vya sheria hizo cha kwanza mpaka cha mwisho viondolewe na visirudishwe tena? Ni wapi katika mfumo wa sheria kwamba sheria haiwezi ikawa *repealed* na kurudishwa tena? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umekwisha?

**MBUNGE FULANI:** Ya kwanza hiyo!

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza? Okay, baada ya kusema hayo nisahihishe mambo mawili yaliyokosewa au yaliyosemwa kimakosa na Mheshimiwa Mbilinyi na Mheshimiwa Kubenea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbilinyi jana alivyoanza alisema eti tafsiri ya *media* kwenye Muswada eti ni chombo cha habari za ki-*electronic*. Chombo cha habari cha *electronic* kwenye huu Muswada wa kisheria maana yake ni *electronic media,* tafsiri ya media kwenye Muswada huu kwa Kiswahili ipo kule nyuma, ni sekta ya habari. Sasa iwapo mtu hapa anasimama kama Waziri Kivuli wa Habari halafu anashindwa kuona tofauti kati ya *media* na chombo cha habari cha *electronic,* haya ndiyo tunasema sasa umuhimu wa kuzingatia viwango na weledi unahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kubenea naye akaja na *analysis* yake moja, ile *statement* ukiisoma kweli ni sahihi, lakini ukifikiria kwa sekunde mbili kuna tatizo kubwa la uchambuzi. Alisema hivi, kwamba *Uhuru wa habari ni kitu tofauti kwa hiyo kuna haki ya uhuru wa habari, lakini hakuna haki ya kuwa daktari*, kweli hakuna haki ya kuwa daktari kama vile hakuna haki ya kila mtu kuwa mwanataaluma ya habari; kuna haki ya kupata habari, kuna haki ya afya kwenye mikataba mingine, lakini hakuna haki ya kuwa mwanahabari na hakuna haki ya kuwa daktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama *analysis* hii ndogo mtu nguli anayejitamba hapa ni mwandishi wa habari wa siku nyingi anashindwa kuwa nayo, basi inaleta matatizo kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda niwakumbushe tukio moja dogo tu linalosema ni kwa nini tuwe na weledi. Mwaka fulani alipouwawa Kamanda wa Polisi wa Mwanza bwana Henry Barlow, ikachapishwa picha ya dada mmoja

kwenye magazeti, mengine yanaheshimiwa sana akasema huyu alikuwa ni chanzo cha ugomvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri kuna watafiti wakasema mbona hii picha ilichapishwa kwenye *website* ya kimarekani na sisi wabishi tuka-*google* kweli tukagundua yule mama alikuwa ni binti wa Kimarekani, taarifa ilikuwa inahusu *obesity but somehow* mtu tu anapata *courage* ya kwenda kwenye *internet photocopy,* weka kwenye gazeti na Watanzania wote wanaaminishwa kwamba eti huyu alikuwa ni chanzo cha mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia hayo, utaona ni kwa nini tunahitaji weledi na *professionalism. (Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Possi. Mheshimiwa *AG* dakika kumi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia fursa hii ili kuweza kupata nafasi ya kuchangia na kutoa ufafanuzi kwenye masuala ya kisheria na ya kikatiba ambayo yamejiri hapa. Lakini nikupongeze pia wewe kwa kuongoza mkutano huu vizuri na wakati huo huo nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza mwaka mmoja ofisini akiwa mkuu wa nchi hii, kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa ya kumpongeza kwa umuhimu anaounesha kwa waandishi wa habari. Moja imedhihirika hata anapotimiza mwaka mmoja ofisini waandishi wa habari ndio watu aliochagua kuongea nao ili ku-*communicate* na wananchi wote. Kusema ukweli Serikalini na kwenye hizi taasisi za umma tunawasiliana kwa madokezo, kwa maandishi lakini ni Serikali kwa ajili ya wananchi. Huwezi kuwasiliana na wananchi kwa barua, kwa simu wala kwa dokezo; ndipo hapo unapokuja umuhimu wa vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili; ni kwa kuridhia tu kwamba Muswada ambao uliandaliwa na Serikali ya Awamu ya Nne na yeye aliposhika madaraka akaona umuhimu wa kuendeleza mwenzake alipoishia na akauleta Muswada huu ambao umeboreshwa kwa kiwango kikubwa na unaoenda ku-*regulate* taaluma hii ya waandishi wa habari kwa maslahi ya Taifa hili na kwa maslahi ya waandishi wenyewe, kwa hiyo, leo tuna kila sababu ya kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri waliyoifanya kuleta Muswada huu, lakini niipongeze sana Kamati ya Huduma za Jamii chini ya Mheshimiwa Peter Serukamba ambayo imefanya kazi kubwa sana. Sisi Serikalini tumeshirikiana nao sana kuboresha Muswada huu na nawapongeza sana. Kama tungeufanya utaratibu wa aina hii ukawa utaratibu wetu wa kudumu, tungekuwa tunafanya vizuri zaidi katika sheria tunazozitunga. Kwa hiyo niwashukuru sana Wabunge wote kwa kupata fursa ya kuchangia kwenye Muswada huu na Mwenyezi Mungu apate kuwabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kusema tu kwamba mambo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyasema na ambayo wameyasema humu ndani Serikali imechukua hatua imeyaboresha kwenye jalada la kwanza la marekebisho ya Serikali na jalada la pili lile ambalo tumeyaleta, yote yamezingatiwa. Muda ni mdogo lakini Waheshimiwa Wabunge wamepata kuyaona haya kweli tumeyazingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ninalotaka kushauri Bunge hili Tukufu; Katiba imetoa mamlaka ya kutunga sheria, ukisoma Ibara ya nne na Ibara ya 64 kwa Bunge, yaani Wabunge ndio mna jukumu la kutunga sheria. Jukumu la kutunga sheria halikuwekwa kwa wadau wala hata waandishi wa habari; kwa hiyo ninyi ndio mnatunga sheria. Kwa hiyo, hata kama wadau hawakuwa tayari kutoa ushauri, lakini nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri jana alitoa hata na taarifa mezani za jinsi wadau walivyoshiriki. Kwa hiyo, jukumu letu sisi Wabunge ni kutunga sheria si jukumu la wadau, hivyo ndivyo Katiba inavyosema, wadau tu wanaweza kutusaidia kuboresha. Kwa hiyo, hili nafikiri niliweke wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, imezungumzwa juu ya haki za waandishi wa habari kwamba zimekiukwa. Tumeshafanya mabadiliko kwenye *schedule of amendment* kwenye ibara ya saba ile ya Muswada, hizi haki zingine zimezingatiwa na Serikali isingeweza kwa sababu haki hizi zipo kwenye Katiba, Ibara ya 18 na ndiyo msingi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine ambayo ningeenda kutolea ufafanuzi ni suala kwamba masharti yaliyokuwepo kwenye sheria tangu ilivyotungwa wakati wa ukoloni baada ya uhuru, Sheria ya Magazeti ile yameendelezwa hata katika Muswada huu. Kwanza hakuna sharti la kikatiba wala la kisheria linalosema kwamba sheria inapotungwa mpya baada ya kufutwa sheria iliyopita mambo mazuri yaliyokuwepo katika sheria inayofutwa hayataletwa kwenye sheria hii. Ndivyo tunavyotunga na ndiyo maana pia hata tunakuwa na *clause* ya *serving* pale; sasa mambo haya kama yalikuwa mazuri lazima yaendelezwe tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme tu kwamba, mambo yote yaliyopo kwenye ibara ya saba yale hakuna hata sehemu moja ambayo yamekiuka Katiba ya nchi hii na yamewekwa pale kwa kuzingatia sheria nyingine zozote zile. Sheria hii haikusudii kuwabana Watanzania kuwashughulikia watu wanaokiuka maadili katika utumishi wa umma au awe anafanya ufisadi kwa sababu unaisoma sheria hii pamoja na sheria nyingine; kwa sababu tuna Sheria ya *Tanzania Extractive Industry Transparency And Accountability,* tulitunga kwenye Bunge la mwaka jana. Kwa hiyo, hatukufichi kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetunga sheria ya *Whistle Blowers Protection Act* haiwezi kuficha watu sijui wanafanya kwenye mikataba, kwa hiyo *lawful interest* ambazo zimekuwa *protected* pale wamesema *lawful interest, commercial interest including intellectual properties,* huu ni utaratibu wa kawaida katika utungaji wa sheria kwa sababu kwenye mikataba hii kuna vitu vinaitwa *confidentiality clauses* zinazolinda maslahi haya, lakini ni yale ambayo ni *lawful.* Kuna sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kile jinsi kilivyo kinachosema kuhakikisha kwamba haiathiri hiyo hakikusudii kumlinda mtu yeyote mhalifu, waandishi watakuwa na haki ya kuripoti tu, lakini wana mipaka yao pia. Kwa hiyo, niliona hili nilisemee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumerejesha baada ya kushauriwa na Wabunge hapa kwa sababu makosa haya ni *sensitive*. Sheria iliyopo ilikuwa ili umpeleke mahakamani kwa kosa la uchochezi, *seditious offence* kupata kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka, *essentially* kibali cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu ilikuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeshauriwa hapa na Wabunge tumekirejesha kile kifungu na inaendelea pia hata ambaye mitambo yake imechapisha *seditious content* naye huwezi kumpeleka mahakamani mpaka upate kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka ili kufanya sasa polisi akikaa pale hamtaki Zitto, anaye-*print* anaenda anakamatwa. Kwa hiyo, tumeangalia yote hayo Waheshimiwa Wabunge na tumeyazingatia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nafikiri nichangie hapa ni hili suala la kufungia magazeti. Limezungumzwa hapa kwamba Waziri anabaki na madaraka ya kufungia magazeti. Suala hili lilishasikilizwa na kuamuliwa mbele ya mahakama kwenye kesi ya kikatiba iliyofunguliwa hapa Dodoma na Mchungaji Mtikila dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na malalamiko kwamba vifungu vile jinsi vilivyo kwenye Sheria ya Magazeti vinakiuka Katiba, sijui Jaji alikataa na ilikuwa ni kesi ya kikatiba na alienda hata Mahakama ya Rufaa wakakataa.

Kwa hiyo, mlioona vitabu hivi nendeni msome *Tanzania Law Report of* 1995 *page* 31, *go and read page* 55 *and page* 56, muda hauturuhusu ningewasomea hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahakama ilisema hivi vifungu hivi havikiuki Katiba na *as per role* ni *administrative and implementation,* ni kwa ajili ya utawala na kusimamia utekelezaji tu. Hata hivyo, katika Muswada huu ambaye haridhiki na maamuzi ya Waziri amepewa fursa ya kwenda mahakamani. Kwa hiyo, hiyo hoja na yenyewe niliona niitolee ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo ningetolea ufafanuzi ni *issue* ya *accreditation*. *Accreditation* ilizungumzwa hapa kama ni kuwadhibiti waandishi. Wazungumzaji waliopita wamelifafanua vizuri. Taasisi nyingi zina hizi hivi vitu, sana sana ni kuwasaidia wao wafanye kazi yao tu kwa mujibu wa taaluma. Sasa hii habari ya haki na hapa ndipo tunapo-*miss point*; katika *scheme* ya katiba yetu haki zinaenda na wajibu na hakuna haki isiyokuwa na wajibu, someni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale yote yaliyopo kwenye ibara ya sabae yamekuwa *saved* yanalindwa na ibara ya 30(2) ya katiba someni yote yaliyopo pale. Hata ibara ya 29(5) na hii ningependa nisome, ibara ndogo ya tano inasema:-

*"Ili watu wote waweze kufaidi haki na uhuru vilivyotajwa katika Katiba hii kila mtu ana wajibu wa kutenda na kuendesha shughuli zake kwa namna ambayo hataingilia haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi wananchi mnataka tufungue kwamba hata mwanamke aliyebakwa kesi yake isikilizwe *in the open court?* Hata mtoto mdogo aliyekuwa *defied* au kubakwa kesi yake isikilizwe *in the open court* na haya yamelindwa hata kwenye Katiba na haki za watu ambao wana mashauri yao mahakamani imezungumzwa kwenye ibara ya 30, masuala ya ulinzi na usalama haya *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi kwa mara nyingine tena nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na kuongoza mkutano huu vizuri. Naunga mkono hoja basi na Mwenyezi Mungu atubariki hii ni siku takatifu. Amina. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana *AG* kwa ufafanuzi wako mzuri. Tunaendelea sasa na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Anastazia Wambura, dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia zawadi ya uhai pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote. Nichukue pia nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Nape Moses Nnauye kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa, lakini vilevile kwa ujasiri na kazi kubwa ambayo ameifanya hadi kufikia hatma ya kufikisha Muswada huu Bungeni; hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuishukuru Kamati ya Bunge kwa ushirikiano wao na kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kutengeneza vizuri Muswada huu. Vilevile niwashukuru watendaji wa Wizara kwa ushirikiano ambao wametupa hadi kufikia dakika hii tunayozungumzia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumshukuru mume wangu mpenzi Lawrent Paul pamoja na familia yangu kwa kuniombea kila wakati. Kwa namna ya pekee kabisa naomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana na ya kujenga ambayo naamini kabisa baada ya hapa Muswada huu unakwenda kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nina masuala machache sana, matatu tu ambayo nitayazungumzia. Suala la kwanza ni ushirikishwaji wa wadau. Nizungumzie ushirikishwaji wa wadau na hasa pale ambapo liliibuka suala kwamba wadau walihitaji wapate miezi miwili zaidi na kikubwa ambacho baadaye kimezungumziwa baada ya kuwa ufafanuzi wote wa kina umetolewa na Mheshimiwa Waziri na Kamati, lakini baadaye ikaibuka kwamba kulikuwa na hitaji la kufika mikoani ili kusudi wadau waweze kuongea na *press clubs* kule mikoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kusema kwamba sisi Wizara tulikuwa tunajua kwamba tuna Muswada huu na tuligawana kazi na Mheshimiwa Waziri. Katika kazi zetu za Wizara tulikwenda mikoani na tulipokwenda mikoani moja ya kazi ambayo tuliifanya ni kukutana na *press clubs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba walitupa ushirikiano mzuri sana; walikuwa wazi kutoa changamoto zao wakajieleza vizuri, lakini kati ya hizo changamoto ambazo tuliziona ni za muhimu kuletwa na kuingizwa katika Muswada wa Huduma za Habari ni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ilikuwa ni masharti magumu ya kupata *press cards* na changamoto ya pili ilikuwa ni kutokuwa na bima katika kazi zao, lakini pia kulikuwa na uhitaji wa kuwekwa katika Mfuko wa Hifadhi za Jamii. Haya yote tumeyaingiza katika kifungu cha 12(a) kinachoeleza kwamba Bodi ya Ithibati itakuwa ikitoa ithibati lakini pia itakuwa ikitoa *press cards.* Nashukuru kwamba hata Waheshimiwa Wabunge akiwemo Msemaji wa Kambi ya Upinzani wameliunga mkono na wamelipongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bima pia linaonekana katika kifungu cha 58; na hiki pia tumepongezwa kwamba ni jambo zuri ambalo limefanyika. Kwa hiyo, kimsingi suala la kuwashirikisha wadau na hasa pale ambapo tunatakiwa tuongeze muda mpaka mwezi wa Pili ili kusudi wale *press clubs* waweze kutoa mawazo yao, tayari tulikwishalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la pili ambalo limejitokeza na nataka kulizungumzia ambapo inaonekana katika michango yetu tumekuwa tukichanganya kati ya leseni, ithibati pamoja na vitambulisho. Sasa naomba nitoe ufafanuzi tu kidogo hapa kwamba, masuala ya leseni; leseni zinatolewa kwa vyombo vya habari hasa machapisho na hili linaonekana kwa mujibu wa kifungu cha 8(1), ila masuala ya hawa waandishi wa habari wao hawapatiwi leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, wasiogope kwamba watachukua mlolongo mrefu au watanyimwa uhuru wa kufanya kazi zao kwamba ni hadi wapate leseni, hao hawahusiki kabisa na leseni, wao wanachotakiwa kupata ni ithibati pamoja na vitambulisho. Kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi kwamba kuna masuala ya leseni. Msuala ya leseni ni vyombo vya habari na kwa mujibu wa Sheria ya *TCRA* leseni ni kwa redio na televisheni, lakini kwa mujibu wa sheria hii inatolewa leseni kwa machapisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kifungu cha 7(1)(b)(iv) ambacho pia imeonekana kama kuna tatizo. Wengi wamekuwa wakitetea kwamba kwa ule wajibu wa vyombo vya habari unaosema kwamba vyombo vya habari vitatangaza au kuchapisha habari au masuala ambayo ni muhimu kwa Taifa kwa kadri Serikali itakavyoelekeza. Kwa hiyo, imeonekana kwamba kwa sababu wao ni wafanyabiashara hawatahitajika kuagizwa na Serikali kutoa taarifa za masuala muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mushashu kwa ufafanuzi mzuri ambao ameutoa jana, amelieleza vizuri sana jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee tu, kwa mfano, kuna nchi moja ya China, mwezi wa kumi kulitokea watabiri wa hali ya hewa, walitabiri kwamba kutatokea upepo mkali katika baadhi ya Majimbo kule China, lakini kwa kushirikisha vyombo vya habari waliweza kutangaza kwa wananchi kwamba upepo huu unatokea wapi na una *speed* gani. Vilevile, vyombo vya habari vikawatangazia wananchi wanunue chakula cha kutosha wiki nzima na wakaambiwa wakae ndani, wasitoke nje mpaka pale watakapotangaziwa kwamba hali imeshakuwa shwari na waliweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hilo, hayakuweza kutokea madhara makubwa kwa binadamu na badala yake yalitokea madhara madogo madogo ambapo ilikuwa magari yaliyokuwa yame-*park* nje miti ikawa imeangukia, lakini siyo kwa binadamu. Pia yalitokea madhara machache kwa wale ambao walikaidi na pengine wale wanaoendesha pikipiki, upepo ule kwa sababu ulikuwa ni mkali uliweza kuwazoa. Vinginevyo visingekuwa vyombo vya habari kushirikiana na Serikali, ina maana kwamba sasa hivi yangekuwepo madhara makubwa katika nchi ya China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono muswada huu kwa sababu una umuhimu mkubwa sana kwa wanahabari, kwa vyombo vya habari, lakini pia kwa kila mmoja wetu ambaye yuko hapa na kwa wananchi wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia kusema tena, naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa ufafanuzi wako mzuri. Sasa namwita mtoa hoja mwenyewe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ahitimishe hoja yeke. Karibu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati wachangiaji wote wa hoja niliyoiwasilisha jana kuhusu Muswada wa Huduma za Habari wa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua michango yao na ninashukuru sana kwa hoja mbalimbali zilizotolewa, hoja ambazo kwa namna moja ama nyingine zimesaidia katika kuboresha muswada tuliouwasilisha hapa. Pia nyingine naamini zitatumika wakati wa kuandaa kanuni zitakazosaidia utekelezaji wa sheria tutakayoipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikufahamishe kuwa tumepokea michango kwa njia ya maandishi na kwa njia ya uchangiaji wa kuongea moja kwa moja wakati wa kuijadili hoja niliyoiwasilisha hapa jana. Naomba kutambua maoni na mapendekezo mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii; maoni ambayo yalisomwa hapa na Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuiongoza Kamati yake na kupata maoni aliyoyawasilisha hapa. Nampa pole kwa kunyooshewa vidole sana na wengine mpaka wakampa majina mabaya, wakamwita jipu. Ukweli ni kwamba kama kuna jipu, basi jipu lilikuwa huu muswada usioisha na leo tunautumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kutambua maoni yaliyotolewa na Kambi ya Rasmi ya Upinzani Bungeni ambayo ndani yake yako mawazo mazuri ambapo kama Serikali tumeyaona na yale ambayo yatahitaji kuzingatiwa kwenye kanuni, tutayazingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia iko michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Tumepokea michango na hoja zaidi ya 94 ikiwa ni michango ya maandishi kama nilivyosema pamoja na wale waliozungumza. Kamati ya Bunge imetoa hoja karibu 30, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hoja 28; Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa njia ya maandishi walikuwa kumi; waliochangia kwa njia ya mjadala ni Wabunge 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kupitia hoja moja baada ya nyingine, nitajibu hoja chache kwa ujumla. Nachukua nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kauli yake ya kutia moyo sana aliyoitoa jana kwamba yuko tayari kui-*sign* sheria hii tukiipitisha hapa siku yoyote ikifika mezani kwake. *(Makofi)*

Namshukuru kwa moyo huu na ni uthibitisho kwamba ana mapenzi mema na tasnia hii na ndiyo maana yuko tayari kutia *sign* sheria hii tukiipitisha. Na mimi natoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuipitisha sheria hii, tumpelekee Mheshimiwa Rais akai-*sign*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona marekebisho tuliyoyawasilisha Bungeni, yako mengi, ni ushaidi na uthibitisho tosha kwamba Serikali ya Awamu ya Tano licha ya maneno mengi ya washindani wetu, ni Serikali sikivu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulileta muswada, umejadiliwa; maoni yametolewa. Namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hata jana hapa wakati Waheshimiwa Wabunge wanachangia, katika michango yao akaona

haja ya kuendelea kufanya marekebisho. Huu ni ushahidi kwamba hii ni Serikali sikivu sana, tofauti na maneno yanayosemwa kwamba siyo sikivu. Ingekuwa siyo sikivu tungeweka mguu chini na muswada tuliouleta hapa, lakini mapendekezo haya ya marekebisho tunayoyaleta yanathibitisha kwamba tumesikiliza ushauri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipitie hoja chache. Nawashukuru wenzangu, wachangiaji wote ambao pamoja na kuchangia, lakini walijitahidi kujibu baadhi ya hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge wenzetu. Nawashukuru sana Mawaziri wenzangu, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, Mheshimiwa January Makamba, Mheshimiwa Possi na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri ya kujibu baadhi ya hoja. Sasa ziko hoja chache nitazigusia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni hoja ya ushiriki wa wadau; imekuwa ni hoja inazungumzwa ndani ya Bunge lako, lakini pia imezungumza hata nje ya Bunge. Pengine labda ni suala la kukumbushana. Ushiriki wa wadau katika utungaji wa sheria ya namna hii, uko wa awamu mbili. Awamu ya kwanza ni awamu ya ushiriki wa wadau wakati Serikali inafanya maandalizi ya muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wakati inafanya maandalizi ya muswada inao wajibu wa kuwashirikisha wadau kuhakikisha inapata maoni yao kabla hata ule muswada haujapitishwa kwenye Baraza la Mawaziri. Utaratibu huo tuliufuata, wadau wakateta maoni yao na maoni yao yapo kwa maandishi kwa ushahidi, yapo. Walishirikishwa vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata pale ambapo Serikali kwenye vikao vya juu waliona ushiriki bado hautoshi, Wizara iliagizwa kuongeza wadau wa kutoa maoni na tulifanya hivyo na ndiyo maana Baraza la Mawaziri likaridhia kwamba muswada huu uletwe hapa ndani ya Bunge lako. Hii ni awamu ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili, ni baada ya muswada kusomwa kwa mara ya kwanza ndani ya Bunge, ambapo ukishasomwa, inakuwa sasa ni wajibu wa Kamati ya Bunge kuwataka wadau kuja kutoa maoni yao na kwa kweli wadau ni hawa hawa ambao Serikali ilikutana nao, wakatoa maoni yao. Hii awamu ya pili wanaitumia kuja kuangalia ni kwa namna gani maoni yao walioyatoa kwa Serikali yamezingatiwa kwenye muswada uliosomwa kwa mara ya kwanza ndani ya Bunge. Huo ndiyo utaratibu ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii awamu ya pili walipokuja, ndiyo hapo pakawa na mgawanyiko; wakatokea ambao waliamua kutoa maoni yao, lakini wakatokea ambao waliamua kutotoa maoni yao. Na mimi naamini pamoja na maneno mengi yaliyosemwa, wale walioamua kutotoa maoni yao, pengine kwa namna moja ama nyingine waliridhika sana na namna

tulivyozingatia maoni yao kwenye muswada na ndiyo maana hawakuona sababu ya kutoa maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba muswada huu tunaoujadili na tutakaoupitisha leo ninaamini ni muswada ambao umezingatia sana maoni ya wadau na hivyo hatuna sababu ya kuwa na mashaka kwamba muswada huu haukuzingatia maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo umeguswa na watu wengi kidogo, lakini inagusa hisia, ni hoja ya tofauti ya muswada tuliouleta na Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976. Ni hoja ambayo imezungumzwa kwa hisia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanishangaza, *unless* tunataka kufanya siasa za uchochoroni; lakini kama nia yetu ni kujadili kwa ukweli, mtu anayesema muswada huu hauna tofauti na sheria ya mwaka 1976 ninapata shida sana kumuelewa kwamba hata lile ambalo halihitaji kwenda kusoma sana kujua yako mambo yana utofauti, nalo hili linapigiwa kelele hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 ilikuwa inampa Waziri mamlaka makubwa mno ukilinganisha na mamlaka ambayo Waziri anapewa kwenye muswada tuliyouwasilisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichofanya kwenye muswada huu; na hii ni nia ya dhati ambayo nimeieleza hadharani, siyo mara moja, siyo mara mbili; ni kwamba tunataka tupunguze *control* ya Serikali kwenye uendeshaji wa vyombo vya habari, badala yake tuchukue jukumu hilo kulipeleka kwenye Baraza Huru la Wanahabari ambalo linaundwa na wanahabari wenyewe na ndiyo msingi wa kuwa na Baraza Huru la Habari katika nchi yetu. Maana yeke ni moja tu kwamba tunapunguza mamlaka ya Waziri; na yamepunguzwa kwa kiasi kikubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ukisoma Muswada vizuri, Baraza Huru la Habari, moja ya kazi waliyopewa ni kuunda Kamati ya Malalamiko. Kamati hii itashughulikia malalamiko yanayotokana na uendeshaji wa magazeti na vyombo vya habari katika nchi yetu, ambapo Kamati hii pia iko kwenye *TCRA* upande wa utangazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilichofanyika ni nini? Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976, kila kosa likifanyika, likishtakiwa linakuja Idara ya Habari - Maelezo, linakwenda kwa Waziri na Waziri ana *discretion* ya kusema kwa kosa hili nakufungia miezi mitatu, ninakupiga mwaka au nakufuta kabisa. Mamlaka hayo yalikuwa yako kwa Waziri kwa makosa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu tuliouwasilisha, tumemwachia Waziri makosa mawili tu; usalama wa taifa na afya ya jamii. Haya ndiyo ambayo tumemwachia Waziri ashughulike nayo. Makosa mengine yote tumewapelekea Baraza la Habari washughulike nayo. Kweli tunasema huu muswada unafanana na sheria ya mwaka 1976? Siyo sawa sawa hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umepunguza sana mamlaka ya Waziri, sana. Sheria ya mwaka 1976; chombo cha habari wakiandika *story*, chombo kizima cha habari kinabeba dhamana, chombo kizima, ndiyo maana iko mifano. Gazeti la Mawio nililifuta kwa kutumia sheria ya mwaka 1976. Pale walikuwa wana wafanyakazi ambao kwa namna moja ama nyingine hawahusiki kabisa na ile *story*, lakini unafuta gazeti zima, unaadhibu hata wasiohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ambayo tunataka kuipitisha hapa, inashughulika na taaluma ya mtu mmoja mmoja. Kwa sheria hii, tutashughulika na mwandishi na taaluma yake badala ya kufungia chombo kizima. Bado tunaona inafanana tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hata hili kweli hatulioni? Tumezungumza hapa, kwa sababu inawezekana ndani ya chombo cha habari kukawa na mtu mmoja au wawili wakorofi, ndio wanapitisha *story* za ovyo. Sasa kupitisha kwao *story* kusimwathiri mhasibu, mhudumu, mfuagiaji au mwanasheria mwingine; hii sheria inakwenda kutatua tatizo hilo. Bado tunasema inafanana na sheria ya mwaka 1976. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya mwaka 1976 imeingiza mchapishaji *(printers)* kwenye kosa. Ndiyo maana yako makosa kwa mfano yale waliyoshtakiwa kina Kibanda na wenzake, iliwaingiza kina Makunga kwenye kesi kwa sababu wana mtambo wa kuchapisha. Sheria tuliyoileta hapa imezingatia mabadiliko ya teknolojia duniani kwamba leo unaweza ukatengeza gazeti lako Dodoma ukalituma Mwanza, likaingia mtamboni lisikutane na mtu, likachapishwa, likatengezwa, likachukuliwa, likapelekwa mtaani. Tukasema kwa mabadiliko haya ya teknolojia, tukiendelea na sheria ya mwaka 1976 tunakuwa hatumtendei haki huyu ambaye ana mtambo kwa sababu hana *room* ile ya kwenda kuliona gazeti. Tukaweka tu *exceptional* mahali ambapo, huyu mwenye mtambo ataamua kufanya makusudi; gazeti limefungiwa, yeye anafanya makusudi ya kuchapa; huyu tutamkamata. Sasa unasemaje sheria inafanana na ya mwaka 1976? Ya mwaka 1976 imemweka *printer;* ya mwaka 2016 imemuondoa *printer;* na bado tunaona ni vitu vinavyofanana, *unless* tunacheza siasa. Kama tunataka kuambiana ukweli, hizi ndiyo *facts.* Huu ndiyo ukweli. Hata siasa zenyewe basi, siasa gani za majitaka? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya mwaka 1976 haina Baraza Huru la Habari, haina! Sheria hii tunaweka Baraza Huru la Habari ambalo linajiendesha lenyewe. Hata hili linahitaji shule kujua kwamba sheria hizi hazifanani? Acha mambo mengine, sheria ya mwaka 1976, hapa pana hoja zilikuwa zikizungumzwa; hoja ya namna ya kuwalinda waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya mwaka 1976 ilikuwa haiwalindi waandishi wa habari, ndiyo maana leo yuko mwandishi wa habari mmoja anitwa Athuman Khamis nadhani, alipata ajali wakati wa kazi, ame-*paralyze* mwili mzima, yuko ombaomba kabisa. Ukiangalia anavyoishi, anaishi kwa shida, kwa taabu, lakini ametumikia sekta hii. Hapa tunasema, tumwekee bima ya mazingira ya kazi yake ili hata kama ikitokea amepata majanga ya namna hiyo, bado aendelee kuishi kwa sababu amechangia kwenye maendeleo ya nchi yetu. Tunasema kweli bado haifanani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kutakuwa na bima ya mazingira magumu, ukiacha bima za afya, lakini inasema pia sheria hii ya mwaka 2016 tukiitunga, inataka tuweke masharti ya umiliki wa chombo cha habari ambapo kule ndani tutatunga kanuni zitakazombana mmiliki wa chombo cha habari kuhakikisha anampa mkataba mwandishi wa habari. Leo tuna waandishi wa mabari ma-*day worker* wanalipwa shilingi 50, 000 kwa mwezi. Matokeo yake, huyu akipewa pesa ndogo akapewa *story* atakwenda akakupige tu, halafu mtajuana huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya mwaka 1976 haikuwa na mfuko wa kuwaendeleza wanahabari, wanajiendeleza wenyewe kama kuku wa kienyeji. Sheria hii tunatunga mfuko wa kuwaendeleza wanahabari. Hapa kuna jambo tunataka kutibu. Leo hili la shule sitaligusa, limegusiwa sana, lakini niwaambieni ndiyo maana magazeti mengi leo, nenda kaangalieni *lead story* ya magazeti yote wana-*lead story* na *story* za siasa. Kwa nini hawaendi kwenye kilimo au uchumi? Kwa nini hawaendi huko? Elimu. Ni rahisi kuandika habari za siasa, Nape kamtukana huyu, kamtukana yule; lakini tukiwabana kwenye elimu, watu wakawa wachumi hapa, watu wakajua kilimo chetu, wataandika vizuri na wananchi wanataka wapewe taarifa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja, Katibu Mkuu Kiongozi *(Chief Secretary)* alitoa taarifa, ameiandika. Taarifa ya idadi ya Wakuu wa Wilaya walioteuliwa na walioachwa. Alipoitoa ile taarifa, magazeti manne yalitoa takwimu nne tofauti na zote zilikuwa kwenye *lead story*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoa taarifa huyu, mmoja, kaisema, kaiandika, lakini waandishi walipoenda kuitafasiri, wakatoa takwimu nne tofauti. Tunataka kumlisha Mtanzania kitu gani? Kuna kitu kinapikwa na vyombo vya habari kwenda kuwalisha Watanzania; tunataka kitu hiki kipikwe kikiwa kizuri. Namna

ya kuwa kizuri, lazima tumpe elimu ya kutosha ili atoe jambo zuri mbele ya safari, *unless* tunataka kuiua hii tasnia. Kama lengo letu ni kuifanya iwe tasnia bora, hii ndiyo njia ya kuifanya kuwa tasnia bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mabadiliko na marekebisho hayo, bado kama lipo jambo zuri kwenye sheria ya mwaka 1976 halitufanyi tusilichukue tukaendelea nalo. Zipo sheria ngapi tumeendelea nazo hata kama zilitungwa miaka ya 1800? Nyingi tu, ili mradi lipo jambo zuri, unaifuta sheria ya msingi, lakini unabeba vitu vichache ndani ya sheria hiyo kama vitakusaidia katika mazingira uliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunataka tuwaaminishe watu kwamba kwa kuwa sheria ya mwaka 1976 imepigiwa kelele, basi sheria nzima ifutwe? Hii siyo sawa. Nadhani tusifike huko, tutendee haki nafasi tulizopewa, tushauri, tutunge sheria nzuri itakayofaa kuendesha tasnia yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nilidhani niligusie ni suala la uhusiano wa Bodi ya Ithibati na Baraza Huru la Habari. Kumekuwa na mkanganyiko mwingi sana hapa kuhusu nani ni nani; nani anafanya nini na mpaka wengine wanakwenda mbali wanasema Waziri amejipa madaraka makubwa mno kwenye hivi vyombo. *Unless* tumesoma hatukuelewa; au tumeamua kupotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada unazungumza wazi, vizuri, kwamba tutakuwa na Baraza Huru la Habari ambalo litaundwa na wanahabari wenyewe. Baraza hili Huru la Habari litaundwa na kila mwanahabari ambaye amekuwa *accredited*. Hakuna mkono wa Waziri kwenye Baraza hili. Ni Baraza ambalo tumelitofautisha na Baraza lililopo sasa hivi *(MCT)* ambalo kwa kweli kimsingi ni *NGO*. Nenda kasome sheria vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kimsingi tumelifanya liwe Baraza huru ambalo wajumbe wake ni wanahabari ambao wamekuwa *accredited;* watajichagua wenyewe, wataunda kamati wenyewe na tena ni kadri wanavyotaka, wataziunda na watatunga kanuni za kujiendesha wenyewe. Hawapewi hela na Serikali, hivi Serikali inali-*control* vipi hili Baraza mpaka inasemekana kwamba kuna mkono mkubwa wa Serikali humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa yapo maslahi na leo nataka niyaseme. *NGO* inayoitwa *MCT* walikuwa wanapata pesa nyingi sana kutoka nje, mabilioni ya pesa, nyingi tu kutoka nje. Sasa hapa tuna tatizo; kuna watu wanatetea ulaji wao. Wanatetea ulaji *at the expense* ya maisha ya waandishi wetu katika nchi hii. Mimi nitakuwa Waziri wa ovyo sana nikikubali utetezi wa namna hiyo. Mnatetea ulaji, tuache kuanzisha Baraza lenye tija kwa waandishi

wa habari tuendelee kuhangaika na *MCT* ambayo kazi yake ilikuwa ni kupokea pesa kutoka nje? Hapana, si sawasawa. Tutendee haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza hili liko huru, wanajitungia kanuni zao wenyewe. Tena kuna watu wanahusisha, sana sana nasikia vijembe wanatupa, kwamba wanasema bodi. Bodi ni chombo kilichotengenezwa ku-*enforce,* kutekeleza maamuzi yatakayofanywa na Baraza. Ni jambo la kawaida kabisa katika utungaji wa sheria wa aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulichofanya, Baraza Huru la Habari tumesema watatengeneza mpaka *code of ethics* za kuendesha taaluma ya habari. Wakishazitengeneza, kipo chombo hapa pembeni kinaitwa bodi na kinatengenezwa na Serikali; kazi yao moja tu, kutekeleza yale yaliyoamuliwa na Baraza kule. Tatizo linatoka wapi hapa? Tunabishana nini katika hili? Sasa mahusiano yake ni hayo tu. Bado hata bodi yenyewe, uundaji wake ina wajumbe saba, katika Wajumbe saba, wanne ni wanahabari, wametokana na Baraza lenyewe; lakini bado aah, unajua, unajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachodhani, hapa pana shida ya kutoaminiana. Mjumbe mmoja leo amethibitisha, anasema hatuamini kama Mheshimiwa Nape ataleta jambo jema ndani ya Bunge hili. Nadhani sasa hii ni *perception* yake na hii hainihusu wala haitusumbui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakachofanya, naamini Waheshimiwa Wabunge mtatuunga mkono, mtaunga mkono marekebisho tuliyoyaleta na tutapitisha Muswada huu kuwa sheria na tutampelekea Mheshimiwa Rais kama alivyoaihidi, atakwenda kusaini na itakuwa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muda, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maoni yenu. Ahsanteni sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono na zaidi ya Wabunge kumi. Ahsanteni.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Usinichanganye Mheshimiwa. Naomba ukae chini. Naomba ukae chini. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu naelewa, lakini kinachonisumbua mimi ni pale ambapo mnataka kutozingatia kanuni zetu kwa makusudi. Bunge letu limejiwekea utaratibu. Ingekuwa unataka kuongea suala la utaratibu, ningekuruhusu tu, kwa sababu ndiyo tunataka mambo yaende hivyo, lakini la Mwongozo katika hatua ambayo tumefika, hakuna na wala usipoteze muda wako. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu Utaratibu!

**MWENYEKITI:** Hakuna utaratibu sasa kwa maana hiyo, nimekufundisha…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu, kuna kanuni inavunjwa!

**MWENYEKITI:** Ngoja bwana!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuna kanuni inavu…

**MWENYEKITI:** Hebu niruhusu tu hatua ambayo nataka tuifanye, halafu nitakuruhusu.

Tunachotaka kufanya sasa hivi, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ashughulike na suala la muda ili tutakapokwenda kwenye Kamati tuyafanye yote ambayo tunataka kuyafanya kwa faida ya muswada huu. Aifanye hiyo, halafu ndiyo nitakusikiliza. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nitumie Kanuni ya 153, kwa mujibu wa Kanuni hiyo ya 153 kwa sababu ya muda sitaisoma, naomba nitoe hoja ya kuliomba Bunge lako liridhie kikao hiki kilichoanza leo asubuhi saa 3.00 kiendelee kukaa na kushughulikia agenda iliyoletwa kwenye *Order Paper* ya leo na kije kuahirishwa pale ambapo ajenda hii itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru kwa hilo. Sasa Mheshimiwa Mnyika.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 58(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 88(2), naomba nizisome. Kanuni ya 58(1) inasema kwamba; "Endapo Mbunge anapenda kupendekeza mabadiliko yafanywe katika hoja kwa kufuata masharti ya Kanuni hizi, anaweza kutoa hoja yake ya kufanya mabadiliko wakati wowote baada ya hoja anayotaka kuibadilisha kutolewa, lakini kabla Bunge halijahojiwa liifanyie uamuzi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 88(2) inasema kwamba, kwa upande wa mabadiliko ya sheria; "Mabadiliko yote yaliyopendekezwa kufanyika katika muswada wa sheria, sharti yawekwe katika jedwali la mabadiliko litakaloandaliwa kwa ajili hiyo na kugawiwa kwa Wabunge na katika kujadili na ama kuyapitisha au kutoyapitisha, vyovyote itakavyokuwa, mabadiliko hayo yatashughulikiwa kwa mpangilio utakaofuata na kwa kuzingatia mtiririko wa Ibara za Muswada wa Sheria unaohusika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati unaahirisha Bunge, ulisema Waheshimiwa Wabunge tuendelee kutafakari mabadiliko yaliyoletwa na Serikali pamoja na sheria inayohusika na asubuhi Waheshimiwa Wabunge ambao wanakusudia kuleta majedwali ya marekebisho wawasilishe kwa Katibu wa Bunge kama taratibu zilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wabunge mbalimbali wa Kambi ya Upinzani asubuhi ya leo tumepeleka majedwali ya marekebisho ya sheria ili katika hatua hii sasa ya kutunga sheria ambayo ndiyo tunakwenda kifungu kwa kifungu, tuweze kuirekebisha sheria kifungu kwa kifungu, lakini marekebisho yote hayo yamekataliwa. Taarifa nilizonazo ni kwamba yamekataliwa kwa maelekezo kutoka kiongozi mmoja wa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni niliyoisoma inaeleza bayana kwamba kabla uamuzi haujafanyika, wakati wowote, majedwali ya marekebisho yana haki ya kupokelewa na kuwasilishwa ndani ya Bunge hili Tukufu. Kwa hiyo,

naomba mwongozo wako na utaratibu wa kikanuni utimizwe na kwa utaratibu huo huo Serikali kwa upande wake, jedwali la pili la Serikali limegongwa muhuri kwamba limewasilishwa leo tarehe 5 Novemba, 2016.

Kwa hiyo, naomba utaratibu ufuatwe. Shughuli ya kuendelea kwenye Kamati isiendelee mpaka kwanza majedwali yote ya marekebisho yaliyowasilishwa na Wabunge kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge, yaletwe hapa mezani ndiyo hatua nyingine iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utaratibu huo ufuatwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, umesoma Kanuni sahihi kabisa, huo ndiyo mtiririko, wala sihitaji kuyarudia. *(Makofi)*

Kitu ambacho hukufanya, nadhani hukutaka kufika kwenye 86(11), lakini yote ni heri tu. Ndiyo maana jana nilisema hivyo na inathibitisha ule muitikio kwa sababu mezani hapa nina *schedule of amendment* ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waitara, ziko hapa.

Waheshimiwa Wabunge, jana nilikuwa nawaambia, tusifanye kazi ya kushinikiza au kushtukizana humu; ndiyo maana nilitoa rai mapema sana. Kwa sababu unaweza usipate nafasi ya kuchangia, lakini kusudio lako la kuleta marekebisho katika eneo ambalo unaona linahitajika ili na upande wa pili ukuunge mkono, yaani yule mwenye hoja yake, naye ni vizuri ayajue marekebisho yako; na pia kutoa nafasi ya kuweka utaratibu bora wa shughuli za Bunge kwa *matrix* ili tusiwe tunagonganisha. Kuna yale ambayo yanafanana unasema hili sawa, hili limeshughulikiwa na *schedule of amendment* ya Serikali; ndiyo maana yake hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu huu tumeutumia sana huko nyuma ili kuhakikisha kwamba tunaleta ufanisi katika kazi zetu. Kusema wakati wowote, haimaanishi kwamba kwa sababu hatujaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima huwezi ukaleta marekebisho yako, hapana.

Waheshimiwa Wabunge, uamuzi wangu sasa, tutaendelea na hatua inayofuata ya kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima ili twende kufanya kazi iliyokusudiwa. Mimi sina *amendment* yenu mezani hapa. Mimi nakwenda na kitu ambacho kipo mezani…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kimewekwa kabla ya saa 3.00 asubuhi na nyingine saa 3.00.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *amendment* ya Mheshimiwa Waitara imepatikana saa ngapi? Sijui.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mimi…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Ya kwangu nilipeleka jana.

**MWENYEKITI:** Uamuzi wangu…

**MBUNGE FULANI:** Huo ni utunzi gani wa sheria sasa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Zinatungwa kama sote tunazingatia haya.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Ya Serikali imeleta leo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila*

**MWENYEKITI:** Hebu tuelewane basi!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Ya Mheshimiwa Waitara ni ya jana.

**MWENYEKITI:** Hii ya Serikali ambayo mnasema imepigwa muhuri wa tarehe ya leo, inajibu nini?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo! Nilivyoiona mimi sijui imepokelewa saa ngapi kwenye Ofisi ya Katibu, lakini nasema…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Hapana. Waheshimiwa Wabunge, kama mtaona…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ndiyo shilingi milioni kumi hizo au milioni kumi kumi zinafanya kazi?

**MWENYEKITI:** Mnisikilize basi! Mheshimiwa Zitto…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuheshimu sana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Hata ukiniheshimu, nami nakuheshimu. Tu-*deal* na hoja!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Hapana, siwezi kubishana kwa kitu ambacho kipo wazi. Hamkuleta… *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Hamkuleta. Mimi sina kitu chochote mezani. Siwezi kuruhusu kitu ambacho hakipo hapa. Huo ndiyo uamuzi wangu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Katibu!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Msigwa, humwoni Mwenyekiti kasimama?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo sahihi!

**MWENYEKITI:** Kamati ya Bunge Zima!

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MBUNGE FULANI:** Tokeni nje jamani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa Mwaka 2016 *(The Media Service Bill, 2016)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MBUNGE FULANI:** Milioni kumi!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tufuate utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika keti, kaa chini.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hicho kifungu kina marekebisho, kwa nini…

**MWENYEKITI:** Kaa chini.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ndiyo, vifungu vina…

**MWENYEKITI:** Usibishane na mimi basi. *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Kwani wewe ni nani?

**MWENYEKITI:** Kaa chini basi.

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**MBUNGE FULANI:** Kumbe ni kweli mlipewa shilingi milioni kumi.

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha tatu kinatoa tafsiri mbalimbali na…

**MWENYEKITI:** Lakini tulipita. *Any way!*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Hapana, nilisimama wakati …

**MWENYEKITI:** Sikukuona, basi haya.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Na huoni sana siku hizi! Naona Mtemi umri umekwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha (3) kwenye tafsiri na kimeleta mjadala sana hapa Bungeni na ningependa bahati mbaya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hayupo lakini kuna wanasheria ndani ya upande wa Serikali, simuoni kwenye kiti chake hiki hapa…

Kiti chake hiki hapa! Kiti chake hiki hapa!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Zitto na wewe huoni! Nawe huoni Mheshimiwa Zitto!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, tafadhali!

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Kiti chake hiki hapa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, usipoteze muda wa Kamati.

**MBUNGE FULANI:** Kwa hiyo, tusiendelee. *(Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki upande wa tafsiri ya *media* ambapo kwenye tafsiri ya kiingereza inasema: "*media means the industry, trade or business of collecting, processing and dissemination of content through radio, television or newspapers, and includes online platforms;*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho, tafsiri ya *social media means online interactions among people in which they create, share, and exchange information and ideas in virtual communities, networks and their associated platform of new technology*.

Mhshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo hoja ambayo ilizusha mjadala wa maelezo ya kwamba ni maeneo gani ambayo muswada huu na sheria hii itakwenda ku-*regulate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kwenye Kamati mpaka sasa tafsiri hii ya kiingereza ya *media,* Serikali inakwepa kuitumia. Hata wakati ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Possi alivyokuwa anachangia, alikwenda kwenye tafsiri ya kiswahili ambayo tafsiri hiyo ya kiswahili inasema na inajumuisha maudhui ya mitandaoni ambayo ni tofauti na *online platform*. Tulibishana sana na Mheshimiwa Waziri katika Kamati kuhusu jambo hili. Nilitarajia kwamba kwenye *amendments* zake, jambo hili ama lingetolewa tafsiri inayoeleweka au lingeondolewa kabisa. Kwa sababu mara baada ya sheria kutungwa, itakapokuwa inatekelezwa, itatupa matatizo makubwa sana kwenye uhuru wa watu kupashana habari kwenye mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Adadi alizungumza jambo hili na alitoa tafsiri ya nchi mbalimbali za *Commonwealth* kuhusiana na *media*, na akasema kabisa kwamba *social media* ni *media* kwa mujibu maamuzi ya kimahakama.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba nipate maelezo ya Waziri kwamba ni kwa nini tafsiri ya kiswahili siyo ambayo ndiyo mantiki kwenye kiingereza? Kwa nini tusioanishe jambo hili au tuliondoe kabisa ili kuweza kuwaondolea wananchi hofu, kwamba Serikali sasa inataka kudhibiti hata majadiliano yao kwenye *facebook*, kwenye *twitter*, kwenye *whatsapp,* na kadhalika? Naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ila haukusema *context* ya *social media* imetumika wapi kwenye kifungu.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** *Problem* yangu ni *online platform* tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Zitto Kabwe kwamba suala hili kwenye Kamati lilijadiliwa sana, na mimi nilidhani kwamba tulielewana, lakini inaonekana bado kuna tafsiri inayotafsiriwa *either* kwa kupotoshwa au kwa kutoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ya Serikali kuweka kifungu hiki ni rahisi sana. Leo ukiwa na *print media,* kwa mfano gazeti; chukua gazeti lolote, mfano, gazeti la Serikali Habari Leo; gazeti hili unalichapisha kwenye *hard copy,* lakini kwa teknolojia ya leo gazeti hili linaweza kupatikana lote kwenye *soft copy* ambapo ndipo linapelekwa kwenye *online platform* ya gazeti husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inataka kushughulikia hili jambo pia kwa sababu ukishashughulika na *hard copy* peke yake, ikichukuliwa *the same contents* ikapelekwa kwenye *soft copy* na ikasambazwa na dalili zinavyoonekana kwa *introduction* ya vitu kama *m-paper* na huduma nyingine za aina hiyo, kuna uwezekano mkubwa watu wakahama kwenye kutumia *hard copy as it is,* badala yake wakai-*access* kupitia *soft copy* kwenye *online platforms za media* husika iliyosemwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lengo la kifungu hiki ni kushughulikia hiyo. Ndiyo maana hata ukiisoma tafsiri yake inasema hivi; *means the industry, trade or business of collecting, processing and dissemination of contents through radio, television, newspapers, and includes online platforms* za hizo ulizozitaja pale nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukizungumzia *media* hizi nyingine zote ili mradi ziwe na *source* kutoka kule kwenye yule aliyepewa leseni na sheria hii haitoi leseni kama ambavyo imekuwa ikizungumzwa hapa kwenye hizo *online platforms*. Inatoa leseni kwa huyu mwenye *print media,* lakini kwa kuwa huyu mwenye *print media* anaweza kuchukua hii *content* kama ilivyo huku, akaipeleka kwenye *online platforms,* ndiyo tunakwenda kushughulika naye huku. Sisi hatushunguliki na habari ya *facebook,* habari sijui ya *whatsapp,* habari ya kitu gani, haituhusu, siyo kazi ya sheria hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Zitto kwanza huna *schedule of amendment*…

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Ninayo.

**MWENYEKITI:** Iko wapi?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo imekataliwa. Umeikataa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najadili kifungu cha Serikali pamoja na marekebisho ya Serikali, ndiyo maana nimesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo yote ya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, naomba sasa ili kuweza kuhakikisha kwamba hayo maelezo ya Waziri ndiyo yanakuwa *reflected* kwenye tafsiri hii, isomeke hivi: "*television or*

*newspaper, including its online platforms.*" Ikiweka pale *newspapers, and including online platform,* ni vitu viwili tofauti.

Kwa hiyo, naomba *comma* ile iondoke na tumilikishe *online platforms* kwa hivyo vitu ambavyo Mheshimiwa Waziri anavisema. Tukiweka hivyo, sina shida kabisa na jambo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri au *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Umempata lakini Mheshimiwa Zitto?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Eeh, nimempata. Kama unataka kuandika sheria vizuri ni sawa. Wasiwasi wetu ni kwamba mtu badala ya kuanzisha gazeti akalisajili, (hii *print media)* yeye akaenda moja kwa moja anaanzisha gazeti la mtandaoni. Sasa hiyo hapo ndiyo...

**MBUNGE FULANI:** Msikilize kwanza.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, *please, please*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Zitto, atambue kwamba anapoleta hiyo hoja, lakini kuna hii *possibility*. Sasa huyu atakuwa *regulated* namna gani? Kwa hiyo, hata katika tafsiri ya kawaida ya sheria, hata usiposema "*its*", yaani kama *possessive pronoun,* unaona eeh, hata kwa maneno yale yaliyobaki hivyo bado inaweza ikaleta maana hiyo kwamba ina *include platform* ya hivyo vitu.

*(Hapa baadhi ya wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mnaona kuna ka-*dilemma* hapo.*(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Eeeh! *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Zitto kwa kukubali hoja yangu niliyoisema; na nashukuru kwa mawazo yake kwa sababu *spirit* nyuma ya kipengele hiki ni hiyo niliyoisema na kama kwa mapendekezo yake tutapata tafsiri ambayo tunaitaka na tunakubaliana kwa pamoja, hatuna matatizo nayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, hebu irudie sasa. Irudie!

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza isomeke, kama inavyoendelea vile; "*through radio, television or newspapers*, ile *comma* (,) iondoke, ile "*and*" iondoke, isomeke; "*including its online platforms.*"

**MBUNGE FULANI:** *Yes!*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, pendekezo hili ngoja kwanza nim-*test* AG. *AG* limekaa vizuri, maana inalenga *newspaper including its online platforms. (Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ni hivyo tuiboreshe zaidi kwa kusema pia "*including its own*" ya hiyo yenyewe. Eeh! *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ni kweli nafahamu, kadri ninavyoitafakari kwa haraka kichwani, tunabaki pale pale. *Improvement* ambayo alikuwa anaitaka, inatupeleka kidogo kwingine, kwa sababu inataka sasa itupeleke kule ambako hatutaki kufika.

Mimi kwa hatua ambayo tumefika na kwa ushauri wa wataalam nilikuwa nadhani…

**MBUNGE FULANI:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Hapana, maana kiingereza na uandishi wa sheria haiwezi ikawa *monopoly* ya mtu mmoja, lakini na wewe ukisoma kwa utulivu utaona. *Attempt* ya Mheshimiwa Zitto ni nzuri, lakini haijajibu hoja. *(Makofi)*

Ningependa ukakaa ukawa *safe* na kama ilivyokuwa imekaa, ile *comma (,)* ibaki "*and includes online platform.*" Maana uki-*restrict* sana sasa *then* inaanza kutuletea matatizo mengine kwamba mtu anaweza akaamua tu yeye aka-*stick* kwenye hiyo; mimi situngi sheria, nawaongozeni tu. Ninyi katika umoja wenu ndiyo tunatunga sheria. Mheshimiwa Waziri.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Waziri alikubali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

Nilichokieleza nilisema hivi, hapa tusigombane na *spirit* hii ndiyo tulikuwa nayo. Mheshimiwa Mbilinyi na Mheshimiwa Zitto walikuwepo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge. Wakati tukifanya marekebisho haya nilikuwa nikisema haya haya, *spirit* nyuma ya kutunga kifungu fulani cha sheria ndicho ambacho kinatufanya tuamue neno litakalotumika. Ndiyo utaratibu wa kutunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilichokisema, maana yetu ni hii niliyoieleza. Ndiyo nikasema kama mapendekezo yote yanayotolewa hayatuondoi kwenye hiyo maana sahihi; lakini kama mapendekezo yanayopendekezwa yanatuondoa kwenye hiyo maana, ni kupotosha *spirit* ya kutunga kifungu hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti hapa anatuambia, mapendekezo yanayotolewa yanatupeleka kwingine, siko ambako tumekusudia kutunga kipengele hiki. Kama ni hayo, hayafai. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbona ulikubali?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Nilikubali nini?

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri anayatoa ndiyo *spirit* na ninakubaliana naye kwa asilimia mia moja. Hiyo *spirit* wakati wa *enforce*ment ya hii sheria, inawezekana akawa siyo yeye Waziri, akawa mtu mwingine kabisa na nchi hii inakua; unajua ujenzi wa nchi kama ni kujenga nyumba hivi, kila mtu anaweka tofali lake. Mheshimiwa Nape yeye ameshaweka tofali lake la huu muswada. Kwa hiyo, tunasaidiana ili baadaye tafsiri isijekuwa tofauti.

Kwa hiyo, *Spirit* yako ndiyo ambayo wote tunakubaliana. Tafsiri ya hapa itakwenda tofauti na ndiyo maana baada ya mapendekezo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kaja na kitu kingine kipya kabisa kwamba mtu anaweza akaamua kusajili gazeti la mitandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri angenisikiliza kidogo, muache Mheshimiwa January ataongea na wewe baadaye ili tuweze kuelewana katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokiomba tuitafsiri hiyo ili ibebe hiyo *spirit* ambayo anaisema Mheshimiwa Waziri, *then* tutatoka hapa tutaendelea na vifungu vingine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza jambo moja linalonisikitisha sana na ndilo ambalo limekuwa wakati mwingine linatawala mjadala na hasa hoja za kutoka upande wa pili tunataka kuaminishana kwamba utekelezaji wa sheria *is a matter of good will.* Yaani *you say,* Nape leo upo, kesho haupo. *It is not a matter of good will.*

Sheria ipo, itekelezwe. Hili la kwanza kubwa sana! Hii habari ya kwamba leo Nape yupo, kesho hayupo, kama inatungwa sheria ya namna hiyo, haina maana. Tunatunga sheria hapa leo Nape yupo au hayupo, bado sheria iendelee kuitwa sheria na ifuatwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri nilionao, kama bado mabishano ni makubwa, twendeni kwenye kura tusonge mbele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunashukuru. Tumeridhika? Mheshimiwa January.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nipate fursa ya kuchangia kwa kueleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria kama ilivyoandikwa, kwa sababu tutakaposema tukaweka "*and its online platforms," yes; assumption* ni kwamba yule *licensee* ndiye anamiliki *online platform* ya gazeti. *It is possible* kwamba gazeti mtu mwingine akali-*digitalize* na akaliweka kwenye *online platform,* kwa hiyo, tukawa tumekosa.

**MBUNGE FULANI:** *Yes!*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa *spirit* ya Mheshimiwa Zitto, lakini naelewa pia *spirit* ya uandishi wa mwanzo, kwa sababu *licensee* siyo lazima yeye ndio awe anamiliki ile *online platform*; anaweza akawa mtu mwingine.

**MWENYEKITI:** Tuvumiliane, mbona kuna tatizo…

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa sababu wote hapa tunajua na tunafuatilia mwenendo wa *online publishing* na ndiko dunia inakoenda sasa hivi; kwa hiyo, nadhani kwa ilivyoandikwa na wanasheria ndiyo sahihi. Kwa sababu leo naweza nikalichukua gazeti la uhuru nikali-*scan* nikaliweka kwenye *platform* ya *online*. Kwa hiyo, utakaposema *its online platform,* maana yake ni *platform* ya *licensee,* wakati siyo *necessarily the spirit. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mara ya mwisho, halafu tunaamua.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mhshimiwa Mwenyekiti, napenda tupate *consensus.* Naelewa hofu ambayo Mheshimiwa January ameizungumza na inaeleweka kabisa. Ukienda kwenye tafsiri ya kiswahili, tafsiri ya kiswahili inakwambia, maudhui. Sasa sijui Mtemi maudhui ni nini? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ni *content*.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Ni *content*. Huku kwenye *online platforms,* kwenye kiingereza, hakuna maudhui. Sijui unanielewa vizuri hapo Mheshimiwa January. Kwa hiyo,…

**MWENYEKITI:** *Dissemination of content* au…

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** *Content yes,* maudhui.

Kwa hiyo, huku kwenye Kiingereza itatupa tabu sana. Kwa hiyo, hoja ambayo Mheshimiwa Makamba anaizungumza ya kuchukua gazeti, yeye amesema "Uhuru," mimi nasema "Raia Mwema," ukaliweka kwenye mtandao kama jinsi ambavyo tunasoma kila siku asubuhi, ndiyo ile maudhui au *content.*

Kwa hiyo, naomba Wanasheria sasa watusadie, hii *spirit* ambayo ipo kwenye kiswahili, ya maudhui i-*appear* kwenye kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu la mwisho, au basi. Nitaongea na Mheshimiwa Nape nje.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hicho kifungu, kina maneno *dissemination of content*. Haya maneno yako pale Mheshimiwa Zitto.

**MBUNGE FULANI:** Hii hapa, msomee.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Eeh! Yako pale Mheshimiwa Zitto.

**MWENYEKITI:** *Media means the industry, trade or business of collecting, processing and dissemination of content through…*" inaendelea. Wewe umesema hayapo huku, yapo.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uangalie ya kiswahili. Ya kiswahili inasema, Maudhui mitandaoni. Nilikuwa naomba uliangalie hivyo. Endelea Mheshimiwa Nape.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zitto sio mgeni wa utungaji wa sheria. Anajua inapotokea mkanganyiko kati ya tafsiri ya kiswahili na kiingereza inayosimama ni tafsiri ya kiingereza na Mheshimiwa Zitto anajua. Hapa ukitaka tupate *exactly* hicho unachokifikiria kule, mimi nadhani unataka kulipotosha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha msingi hapa ni kwamba tafsiri ichukuliwe kama ilivyo kwenye kiingereza na Mheshimiwa AG ameitafsiri vizuri hapa. Naomba kama bado kuna mkanganyiko, tupige kura tusonge mbele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tume-*discuss* vya kutosha, nawahoji. Kifungu hiki cha tatu mara ya pili na marekebisho yake, kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Kuhusu utaratibu.

Ibara ya 4

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(1). Nataka kidogo tupate Mwongozo wako, endapo mtoa hoja kwa mujibu wa Kanuni anatakiwa asimame mara tatu, lakini mchangiaji kama hoja sio yake anatakiwa achangie mara moja. Kwa hiki kifungu tulichokimaliza, nimeona mchangiaji anasimama zaidi ya mara tatu. Sasa ningependa kujua katika vifungu vingine vinavyoendelea, utaratibu unatakiwa uwe ni upi? Naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wangu ni *very straight* kwamba kwa sababu hii ya tatu; yeye anajua ndiyo maana nilimwuliza; je, una *schedule of amendment?* Akasema tumekataliwa. Mimi sidhani kama amekataliwa. Isipokuwa alifafanua kitu ambacho nadhani cha kutaka kusaidia. Serikali imejaribu kujibu na imejibu vizuri naye amejitahidi kuelezea, lakini kwa taratibu za kikanuni yule ambaye ameleta mapendekezo yake ndio anayewasilisha kama wapo wanaotaka kuyachangia kwa *ratio,* uwiano ule ule tunaoufahamu anahitimisha hoja yake, tunaamua.

Sasa maadam hili neno ndiyo limepewa picha ambayo ina sura tofauti, maelezo ya Serikali wengine wanasema siyo; ndiyo maana nimesema ikikaa vizuri tutakwenda vizuri. Kwa hiyo, naamini baada ya kutafakari, hata mimi sasa hivi Mheshimiwa Zitto, nakushukuru *for your industry* lakini sidhani kama litatufikisha huko. Na wewe nenda ukatafakari tukimaliza hapa; tutakaa tuongee wote, lakini halitatufikisha huko.

Kwa hiyo, nasema mwongozo wangu ni kwamba tuta-*stick* kwa Kanuni kwenye maeneo tunayoenda ili tumalize haraka. *(Makafi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninawahoji kifungu cha nne kimeafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya) Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 6

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, karibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimwa Mwenyekiti, nakushuru. Kifungu cha 6 kinasema umiliki wa wajibu wa vyombo vya habari na hofu ni ile tu kwamba namba 2 inasema, masharti ya umiliki wa vyombo vya habari yatatungwa na Waziri kwa maana ya kanuni lakini hapo wanamaanisha kutoa leseni kwa vyombo vya umma na vyombo vya watu binafsi. Sasa nataka tuone namna ya kuhakikisha kwamba kutakuwa hakuna uonevu katika kutoa leseni hasa katika vyombo vya watu binafsi. Ndiyo hoja yangu hapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza hiki kifungu kifutwe, kinampa madaraka makubwa sana Mheshimiwa Waziri na atakuwa anatumia madaraka yake vibaya.

**MWENYEKITI:** Tumekuelewa, ahsante.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria yoyote inayotungwa ikiwa kuna jambo ambalo linatakiwa kutengenezewa kanuni, sheria hiyo inampa mamlaka na madaraka ya kutengeneza kanuni Waziri. Hapa tulichokifanya ni jambo rahisi sana, kwamba hapa pana utoaji wa leseni kwa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji huu wa leseni ni lazima ulezwe utafuta utaratibu gani? Utajaza fomu, utapeleka vithibitisho gani; utafanya hivi; utafanya vile ambavyo ndilo jambo linavyozungumzwa kwenye kipengele hiki cha 6(2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukifuta kipengele hiki ni kulifanya zoezi hili liende holela; unafuata utaratibu gani katika kupata leseni? Hili la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo yeye anasema ndiyo hoja yake ya msingi, tunamhakikishiaje kwamba hakuna uonevu, viko vyombo vinavyohusika na ku-*redress* jambo ambalo mhusika *aggrieved*. Sasa hivyo vyombo ndivyo ambavyo vitakavyohakikisha kwamba unapata haki yako. Kwa hiyo, sioni mashaka hapa yanatoka wapi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, bado hofu inabaki pale pale. Ni kweli kwamba bado hata hii miongozo ataitengeneza yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ninayoiona ni kwamba namna gani itaonekana hapa kwamba hiyo nafasi hataitumia vibaya? Kwa sababu yeye Mheshimiwa Waziri binafsi kama Nape, tayari huo uhuru alikuwa hawezi kutoa leseni za kuruhusu chombo kiwepo au kisiwepo; vya umma na binafsi. Amekuwa akifuta magazeti na kufungia baadhi ya redio na akakataa kusajili. Sasa nauliza, hiyo hofu anaiondoaje hapa? Mtu wa kawaida anawezaje kuiona katika hizi kanuni au katika sheria tunayopitisha sasa? Ndiyo hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kifutwe au kuwepo na maneno hapa ambayo yataonesha kwamba haki itaonekana inatendeka. Vinginevyo naomba nitoe hoja ili Waheshimiwa Wabunge wengine waweze kutoa maoni yao katika hoja hii.

**MWENYEKITI:** Toa hoja sasa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MBUNGE FULANI:** Imeungwa mkono.

**MWENYEKITI:** Imeungwa mkono, nashukuru. Nitachukua kwa uwiano ule mnaoufahamu. Eeh, ndiyo! Nawashukuru tunaitoa kwenu; tunaanza na Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kifungu cha 6(1), ambacho Mheshimiwa Waitara anaomba kifutwe, *I mean* 6(2); kinaeleza kwamba suala zima la utoaji wa leseni za waandishi wa vyombo vya habari limeachwa mikononi mwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la leseni ni jambo zito sana. Vyombo vya habari vinaanzishwa, vinaajiri wafanyakazi, wataalamu na vinalipa kodi. Ila leseni unaweza ukaomba na ikabaki kwa Waziri kwa miaka miwili, mitatu, minne mpaka mitano usipate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu upo kwamba watu walioomba kusajiliwa magazeti, wamenyimwa na hakuna majibu yoyote yaliyotolewa kwa wale walioomba usajili wa magazeti. Hali kadhalika, magazeti yenyewe au redio au *television* zina leseni zenyewe tayari. Kuna hati za usajili ambayo kila mtu anapewa ili gazeti lake liendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri sheria ikasema kwamba kutakuwa na muda maalum ambao Waziri anafungwa nao kwa mujibu wa sheria, kwamba ikifika ndani ya siku saba awe ameshatoa leseni kwa chombo kile cha habari. Jambo hili lisiachwe wazi hivi, likiachwa wazi hivi linampa nafasi mtu mwenye nia mbaya ili asiweze kutoa leseni kwa chombo cha habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waitara.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waitara anapendekeza kwamba kifungu cha 6(2) kifutwe. Kifungu cha 6(2) kinasema kwamba, "*conditions for ownership of media houses shall be as prescribed in the regulations.*" Hapa nina mambo mawili ambayo nilikuwa napenda nipate ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza tunampa mamlaka Waziri ya kuamua kupitia *regulations* na kama mnavyofahamu *regulations* haziji Bungeni, kwamba mtu mmoja anaweza kumiliki *media houses* ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waziri anaweza akaja na *regulations* kwamba ukiwa na redio huruhusiwi kuwa na magazeti; ukiwa na *television* huruhusiwi kuwa na magazeti. Sasa nilikuwa naomba nipate maelezo ya Waziri, mantiki *(spirit)* ni hiyo? Kama *spirit* ni hiyo, haoni kwamba ni vizuri kifungu hiki kikawa kwenye sheria badala ya kuwa kwenye *regulations*, kama namna ambavyo Mheshimiwa Waziri anapendekeza hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo inanifanya niungane mkono na Mheshimiwa Waitara ni *percentage* ya *ownership;* na jana kulikuwa na mjadala huo hapa. Kuna watu ambao waliona kwamba ni vizuri kuweka masharti ya kiwango cha asilimia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu pia ni hiyo hiyo kwamba kuweka jambo hili zito namna hii kwenye mamlaka ya Waziri kuamua kwa mujibu wa *regulations*, hatumpi mamlaka makubwa sana Waziri ya kuamua kuhusu jambo hili? Kama ni hivyo, kama tunaona kuna haja ya kuweka hizo *conditions* za *ownership in percentage,* kwa nini lisiwe kwenye sheria. Kama litakuwa bando lipo kwenye *regulations*, namwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kabla sijamwita Waziri au *AG* nataka nisahihishe ulichokisema kwamba *regulations* huwa haziwasilishwi Bungeni. Hapana bwana! *Regulations* zote ndiyo maana Serikali huwa inawasilisha *subsidiary legislations* zote Bungeni. Hiyo ni kwa mujibu wa sheria; tafsiri ya sheria za nchi *section 38.* Kila siku, juzi wamewasilisha hapa. Hizo ndiyo *GN* zote zinakuwa na *regulations, by-laws* zinakuwa na kila kitu. Ndiyo maana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ambao mlikuwa wengi hamuipendi, duniani kote ndiyo wanafanya kazi hizo kwa niaba ya Bunge. Sasa tuendelee Mheshimiwa Waziri au AG, *whoever*. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna hoja za watu wawili; kuna ya Mheshimiwa Kubenea na ya Mheshimiwa Zitto. Nilidhani utaratibu ulikuwa wanajadili wote kwanza; lakini acha nijibu. La kwanza…

**MWENYEKITI:** Subiri kwanza.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Naam!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na hoja ya Mheshimiwa Waitara. Kitu ambacho Mheshimiwa Waitara anataka kifutwe ni kile ambacho kinasema *condition for ownership of media houses shall be as prescribed in the regulations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kikifutwa, kunabaki na ombwe. Swali linabaki, je, umiliki wa *media houses* uwe na masharti gani? Kwa hiyo, hakutakuwa na masharti yoyote. Hiyo ni hatari ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja aliyoisema Mheshimiwa Zitto Kabwe kwamba tukiweka hii tunampa Waziri kusema kwamba ukimiliki gazeti usiwe na redio, hapana, siyo kweli. Kwa sababu sheria ndogo zozote kwanza haziwezi zikatafsiriwa kinyume na matakwa ya sheria mama na Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namkumbusha tu Mheshimiwa Zitto kwa mfano, Katiba inasema kila mtu ana haki ya kumiliki mali, kwa hiyo leo Waziri hawezi akatunga *regulations* na kusema miliki kitu kimoja na kingine usimiliki *that interpretation is wrong.* Sasa kwa sababu hii *condition* ikiwa *deleted* tutakuwa na ombwe la masharti ya umiliki wa vyombo vya habari. Kwa sababu Mheshimiwa Waitara hajaleta sasa mbadala uwe nini, masharti ya kumiliki hiyo *media houses* yawe yapi, itakuwa sasa *the provision* haito- *make sense* kwamba hata mimi leo tu nikiamua kutaka kumiliki *media house* nitapewa hiyo *media house* bila masharti.

Mwisho, lile la Mheshimiwa Kubenea la kusema kwamba kuna watu waliomba leseni*, I don't know whatever* hawakupewa, *well*. Kama kuna sheria imewahi kusema *if somebody applies one, two, three the authority shall grant their application, then* hiyo sheria ni *unreasonable,* kwa sababu *whenever there is an application* basi kuna *discretions* ya kukubali au kukataa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijielekeze kwenye hoja mbili na mimi nichangie. Kwanza tulitunga sheria hapa ya *EPOCA (Electronic And Postal Communications Act)*. Kulikuwa na kifungu cha 26 ambacho kilihitaji kuwe na *minimum requirements* za *local shareholding* kwa makampuni ya simu, jambo kubwa sana, kifungu cha 26 kikampa Waziri kwamba kwa kutumia kanuni ndiyo ata-*prescribe minimum local shareholding* kwenye makampuni ya simu.

Kwa hiyo, kuna *precedent* hapa ya kumpa Waziri mamlaka ya aina hiyo ya kuweka *minimum shareholding* kama tumempa nafasi na uwezo kupitia kanuni wa kuweka *minimum shareholding* kwenye makampuni makubwa kama ya simu, inawezekana kabisa pia tukampa uwezo huo kwenye vyombo vya habari, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni hili lililosema bahati nzuri limeshajibiwa la leseni na sheria ndogo na kanuni, lakini inawezekana kabisa na ni sahihi kwamba Waziri tumpe nafasi ya kufanya *consultation* na wadau ili aweze kuandika kanuni zinazozingatia hali ya soko kuliko tukilifanyia *prescription* hapa kwenye sheria hii nadhani linafaa kwenye kanuni na kuna *precedent* hiyo kwa sheria zilizopita.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe ulisaidia sana ulipo-*cheap in* kuelezea na vilevile Dkt. Possi ameelezea vizuri tu.

Mimi nataka nisisitize tu kwamba hakuna wasiwasi kuhusu hizi *regulations* ambazo atatunga Mheshimiwa Waziri, kwa sababu *regulations* tunazoziongelea hapa zinaangukia kama ulivyosema kwenye *category* ya *subsidiary registration*.

Vilevile utungaji wa *subsidiary registration* unafuata taratibu za kisheria, *there are must be consultation of interest,* wadau watahusishwa *definitely*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili *comfort* yangu kubwa ninayoipata hapa ni kwamba hii *as a subsidiary registration* kwa mtu yoyote ameona haki yake imekiukwa bado kuna haki ya kwenda mahakamani *for review* ambayo ipo pale *automatically* wala siyo suala la kuwekwa hapa kwenye maandishi tena, ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru ambao wanaunga mkono hoja ya Serikali hapa, kama ulivyoeleza maelezo yako na Dkt. Mwakyembe na Mheshimiwa Possi yanaondoa mashaka aliyokuwa nayo mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Kubenea kwamba kuna magazeti sijui yameomba na hayakupewa nalo Dkt. Possi amelielezea vizuri. Lakini niseme nchi hii ilikuwa na magazeti na majarida 881, tulipoingia katika kushughulika na jambo hili tukaanza kushughulika na yale ambayo kwa kweli kwa namna moja ama nyingine yametoka nje ya sheria. Ukiwa unafanya hivyo lazima usimamishe kwa muda wakati ukishughulika na jambo hilo na hili ni jambo la kawaida imefanyika hivyo hata kwa wafanyakazi hewa, lakini hakuna mtu ambaye amenyiwa kusajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii tunayoipendekeza hapa inaeleza ikiwa mtu amezuiliwa au amenyimwa haki yake imetengeneza utaratibu ambao unakupeleka mpaka mahakamani na hii ni tofauti kati ya sheria iliyopita na hii tunayoipendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni hili alilolieleza Mheshimiwa Zitto, Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003, inaeleza wazi kwamba watu wataruhusiwa kuanzisha vyombo vya habari, tena siyo kwa namba. Sasa inawezekanaje leo Waziri, sio tu sheria haitakiwi kupingana na sera, lakini hata kanuni hazipaswi kupingana na sheria na sera nakwendaje kutunga kanuni ambazo zitapingana na sheria, zitapingana na sera. *(Makofi)*

Mimi nadhani hapa tunarudi kwenye ule ugonjwa wa kutokuaminiana na ninajua ipo kampeni inafanywa kubwa sana na kampeni yenyewe ni ya wamiliki wa vyombo vya habari wa kutoka nje ambao wanataka waendelee kumiliki vyombo vya habari vya ndani kwa asilimia mia moja. Mimi nadhani hili siyo sawa sawa na hii kampeni kwa mlango huu haifai, tuwatendee haki wazawa wa nchi hii, tuwape fursa ya wao pia kushiriki kwenye jambo hili. Mimi nadhani mashaka haya tuyaondoe hakuna mahali mtu atabanwa, kama sera imesema na sheria haikuelekeza tukabane hivyo, ninatungaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kanuni hizo zikishatungwa kama ilivyosemwa zinaletwa hapa. Pamekuwa na hoja inazungumzwa kama vile hizi kanuni zikitungwa ni za Mheshimiwa Nape na familia yake wanaamua, *but that is a process* na *process* ipo wazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara mzalendo wa Tanzania.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza nafikiri mambo mawili nimeyaona katika mjadala. Kwanza kuna matumizi mabaya ya kura za wingi wa CCM humu, Mheshimiwa Waziri unaweza ukamkuta anazungumza vizuri halafu baadae anasema tupige kura kwa sababu anajua wale wenzake wapiga makofi watamuunga mkono ambayo siyo sawa kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni habari ya kutuhumu hapo kwamba kuna mtu anafanya kazi. Mimi siyo mwandishi wa habari, nimesema tu kwamba kwa namna tu ninavyotazama hapa kumekuwa na matendo yake yeye mwenyewe. Kwa hiyo, kama yupo na mabaya anafanya yeye kwamba yeye kuna magazeti kayafungia. Kwa hiyo, habari ya kutoa hoja Mheshimiwa Waziri unatuhumu watu siyo kweli. Mimi sikufanya kampeni wala wamiliki siwajui. Nilisema hapa katika maelezo yao yanaonyesha kwamba hutakuwa na matumizi mabaya ya nafasi yako. Kama hayo uliyozungumza ndiyo utakayomaanisha na kama kanuni zitakuja na kama wadau watashirikishwa sina shida na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu kama kuna maelezo yoyote na wenzangu wamependekeza kwamba angalau yawepo kwenye sheria ambayo itaonyesha kwamba hiyo hofu ambayo watu tunayo na waandishi wanayo kwa nini Mheshimiwa Waziri wa Habari ambaye ni shemeji yangu kwa namna watu wanavyomtazama, ni kivuli chake ndicho kinachomfanya watu wakuogope, kwamba huyu hana nia njema na waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna maneno ya kuweka hapa mazuri ya kuonyesha kwamba Watanzania, waandishi wa habari, Waheshimiwa Wabunge, sitatumia nafasi yangu vibaya haki itatendeka na mkiomba leseni siwezi kuwa na nia ovu ya kuwaumiza, sitakuwa na shida na kifungu hicho. Kama hakuna haya maelezo yakaingizwa katika eneo hili kifungu kifutwe, kama hakifutwi turudi kwenye utaratibu ule mliouzoea kwamba walio wengi wapige ndiyo hapa halafu tusonge mbele, kwa maana ya kura zipigwe. Hata hizi chache za kwetu watarekodi kwamba sisi tulipinga ili madhara yakitokea huku mbele wote tusiwe kwenye mkumbo huo, lawama zibaki kwa Mheshimiwa Nape na wenzake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, basi ninaitoa hii hoja muiamue.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiko yoyote)*

Ibara ya 7

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kifungu cha saba tukusikie.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba mabadiliko kwenye maeneo mawili kwa hiyo naomba niondoe ili ya kwanza nimejiridhisha na wenzangu hapa kwamba haina shida. Lakini nibaki na kifungu cha 7(b)(iv) ambayo inasema *to broadcast or publish news or issues of national importance as the Government may direct*.

Mimi shida yangu ipo hiyo *as the Government may direct,* haya ndio tulikuwa tunasema kwamba wanataka Serikali ielekeze watu waandike nini kwa sababu tayari sheria zipo, kama kuna mtu ameandika kitu ambacho ni cha uongo, amevunja miiko ya uandishi wa habari hiyo nadhani yenyewe inaweza ikatosha kumuwajibisha huyo ambaye ameandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza hili neno *as the Government may direct* liondoke ibaki kwa maneno mengine yote ambayo yanabaki pale ndiyo hoja yangu hapa. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waitara anaweza kuwa ana nia njema lakini nikisoma muswada huu sioni unaenda mpaka *sub clause 7*, kwa hiyo muswada huu haauna hizo *sub clause 7,* hazipo. Kwa hiyo, anachokipendekeza Mheshimiwa Waitara hakipo kwenye muswada.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa anasema unashuka kwenye 7 unashuka nayo mpaka (b) halafu unateremka nayo mpaka (iv). Mimi kama Mwenyekiti huwa nina *guide* tu kutenda haki, yawezekana wengine kiingereza na hayo mambo sitaki mimi. Lakini nataka tumtendee haki, nadhani wote tunaona alichosema Mheshimiwa Waitara sasa tumjibu, mwisho *as the Government may direct*.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho Serikali tunaona kwamba ni bora ibaki hivyo kwa ajili ya kuendeleza ushirikiano kati ya Serikali na vyombo binafsi.

**MWENYEKITI:** Maelezo umeyasikia?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo majibu yao?

Mheshimiwa Mwneyekiti, hata unaona majibu yenyewe yalivyo yamekaa kichenge - chenge kweli siyo Chenge kwa maana ya jina lako yaani yamekaa kichenge chenge kweli kwa maana ya yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nitoe hoja kwa sababu hichi ndiyo kitu ambacho ni kinyongo chenyewe. Tena amesema vizuri hapa kutangaza au kuchapisha habari au masuala ambayo ni ya muhimu kwa Taifa, mimi nikataka iishie hapo. Ukishasema mtu achapishe au aandike mambo ambayo ni muhimu kwa Taifa watu wote wanaelewa, lakini ameongeza hilo neno kwa kadri Serikali itakavyoelekeza, maana yake Waziri na Serikali akitaka kuona jambo hili sisi hatupendezwi nalo hataki liandikwe ndiyo maana yake. Kwa hiy, hayo majibu hayatoshelezi na huo ni ukandamizaji na hiyo ni hofu, na huo ni uoga. Kama ni kuwatengenezea utamaduni Watanzania kwamba mambo ya Kitaifa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja jambo hili lijadiliwe na tupate maoni ya Wabunge wengine na ninaomba mniunge mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wawili huku na huku nione. Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Ole-Nasha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ninaunga mkono kifungu kama kilivyo na sababu yangu ni moja tu, unapozungumzia suala la mamlaka na wajibu wa chombo kutoa habari ambayo ina maslahi kwa jamii ni kwa yale mambo ya msingi jambo hilo linatakiwa kufika kwa watu kwa haraka linazungumzia, kwa mfano, afya, kilimo, janga fulani, jambo la dharura hivi, hivi ubaya upo wapi kama Waziri au Serikali maana hapa neno lililotumika tena siyo Waziri maana pengine Waziri lina ukakasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno lililotumika hapa ni Serikali kwa tafsiri ya kisheria ni pana siyo Waziri peke yake, najua wanasheria mnanielewa limepewa uzito huo ili lisiwe la mtu mmoja. Serikali hata ninyi wenyewe ni sehemu ya Serikali kwa sababu ni watu na mtu yeyote anayefanya shughuli anaweza akaitwa Serikali. Kwa hiyo, inaweza ikawa katika mazingira fulani kama

tunavyoita vyombo vya habari kuwaeleza jamani hili jambo liifikie jamii ni la haraka. Haiwezekani vikaitwa vyombo vya habari vikaambiwa andika habari zetu za chama fulani au andika habari za kitu fulani au za kampeni ya mtu fulani haiwezekani yatakuwa mambo mahsusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza kifungu hiki kwa maslahi mapana ya Taifa kibakie hivi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naunga mkono kifungu hicho kama kilivyo. Wasiwasi wa Mheshimiwa Waitara ni kwamba kifungu hicho kinaweza kikatumika vibaya kwa maslahi ya chama kilichopo madarakani, lakini nimfahamishe tu kwamba lengo la kuweka masharti kwamba Serikali ndiyo hasa inaelekeza ni kwamba kusipokuwa na mtu wa kueleza nini ambacho ni cha umuhimu kwa Taifa maana yake vyombo vya habari tulivyonavyo vingi kila kimoja kinaweza kikaamua kitu chake ambacho kinafikiri kwamba ni cha muhimu kwa ajili ya Taifa. Kuna wengine akiona wakati huo labda kuna *fiesta* anaweza akasema hiki ni kitu cha *national importance,* mwingine akiona kwamba kuna mashindano ya urembo anasema hiki ni cha *national importance*, mwingine kama kuna tamasha la singeli, sasa ni lazima kuwe na *source* moja ambayo ndiyo itasema kwamba hiki kitu ni muhimu kwa Taifa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Waitara anasema tuweke tu kwamba vyombo vya habari vitakuwa na majukumu ya ku-*broadcast* vitu vya *national importance,* lakini suala ni kwamba kama hakuna mtu wa ku-*enforce how do we enforce it* kama haisemi kwamba kuna mtu anayei-*direct*, hauwezi ukaacha tu juu juu vinginevyo hakuna haja ya kuweka. Kwa hiyo, naomba tu asiwe na wasiwasi haiyumkiniki katika mazingira ya muswada huu ambao tunasema unajaribu kulinda haki za vyombo vya habari tukaleta *restriction* au tukaleta mazingira ambayo ni tofauti kabisa na masharti yenyewe au ni tofauti kabisa na makusudio ya muswada wenyewe. Kwa hiyo, mimi naomba tuendelee na kifungu kama kilivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Angellah Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninaunga mkono mapendekezo kama yalivyoletwa na Serikali katika kifungu hicho cha 7(1)(b)(iv).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutakuwa nchi ya kwanza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka utaratibu ni wakati gani vyombo vya habari vinaweza kuelekezwa na Serikali kutangaza au kuandika masuala yenye umuhimu wa Kitaifa. Vilevile ukiangalia katika kile kifungu kidogo cha (iii) kama ni masuala tu

ya *promotion* ya *public awareness* yapo wazi kabisa wameachiwa. Lakini inapofikia kwenye masuala yenye umuhimu wa Kitaifa ni lazima kuwe na chombo, ni lazima Serikali iweze kuingilia kuhakikisha kwamba ina-*protect* wananchi wake wakati ambapo masuala yenye umuhimu wa Kitaifa wanatakiwa wapatiwe waweze kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishuhudia wakati wa tetemeko, Mheshimiwa Heche tulia; wakati wa tetemeko tulishuhudia baadhi ya vyombo ukiangalia ndugu zetu wengine wamepata madhila makubwa, wengine mpaka walifikia kufariki. Lakini vipo baadhi ya vyombo vilikuwa vikiendelea na miziki ya burudani na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima hili lifike mwisho, kifungu hiki ni sahihi kabisa tusipoteze muda hapa, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Wakati jana nachangia nililizungumzia pia hili, hapa tunatunga sheria na maelekezo ya Serikali kwamba ni vitu gani *media* wazingatie mmeandika kwenye hicho kifungu cha 7(2). Hivyo vitu vyote ambavyo mnavizungumza mmeviweka hapa. Kwa hali ya kawaida, kuna *media* za watu binafsi ambao hamuwapi ruzuku, mnataka waandike vile ambavyo ninyi mnavitaka? Ndiyo maana utafiti wa hivi karibuni sikumbuki ni utafiti gani tumesoma hata kwenye mitandao TBC imekuwa ya mwisho watazamaji hawaangalii tena kwa sababu ya vitu ambavyo mnaviandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, TBC imekuwa ya mwisho kwa sababu mnaelekeza vitu gani waandike na warushe. Kwa hiyo, kama tatizo ni Serikali itakavyoelekeza pia mmetoa kwenye kifungu cha 50 faini zile zote kwamba atakayekiuka, atakayetoa taarifa za uchochezi, za uasi, adhabu zake zikoje, tumeandika kwenye sheria hii. Sasa mnataka muelekeze kitu gani tena na niseme kwamba, hivi karibuni pia tumeshuhudia jinsi ambavyo Serikali inaingiza miguu mpaka kwa wahariri kwamba hivi vichwa vya habari vifutwe ndiyo hicho kitu mnachotaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida hoja ya Mheshimiwa Waitara ina mashiko, kwamba ibakie vilevile, lakini atakayekiuka adhabu tumeshaziweka kwenye sheria hii, kwa hiyo, hakuna sababu ya kuandika tena vile Serikali itakavyoelekeza. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waitara kwamba hayo maneno kwa kadri Serikali itakavyoelekeza yaondolewe, kwa sababu katika kifungu husika na katika sehemu ya tafsiri ya sheria hakuna mahali ambapo *national importance* au masuala yenye umuhimu kwa Taifa yametafsiriwa maana yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunapokuwa na ombwe la kwamba, hakuna maana ya tafsiri yenye umuhimu kwa Taifa. Serikali inaamua yenyewe lipi ndiyo liwe jambo lenye umuhimu kwa Taifa kunaweza kukawa na mambo ambayo hayana umuhimu kwa Taifa lakini yana maslahi kwa *propaganda* za Serikali yakalazimishwa vyombo binafsi yaweze kupenyezwa kwa vyombo binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu hiki killichopo hivi sasa kinaficha naunga mkono kiondolewe kwa sababu kinaficha nia ovu iliyokuwepo kwenye muswada uliopita kwamba kuna wakati Serikali ielekeze vyombo binafsi viunganishe matangazo kwenye Televisheni ya Taifa, vitangaze matangazo ya television ya Taifa. Baada ya wadau kupinga sana hiki kifungu Serikali inakirudisha kwa mlango wa nyuma kwa kuweka kipengele hapa kulazimisha kwamba, masuala muhimu yenye maslahi kwa Taifa yatolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira kama haya kifungu hiki kikiwekwa kinaingilia uhuru wa vyombo vya habari. Kama ni masuala ya maslahi kwa Taifa viachiwe vyombo vyenyewe binafsi visimamie maslahi ya Taifa, kwa sababu kuna vyombo vya umma ambavyo vinafanya kazi kwa vyombo vya umma. Kama kuna chombo ambacho kitakiuka masuala ambayo yanakatazwa yapo maeneo kwenye sheria ambayo yanashughulikia makatazo kwa hiyo, hakuna ulazima wowote wa kuwepo kwenye kifungu hiki maelekezo haya Serikali kuweza kuagiza vyombo binafsi viweze kurusha matangazo ambayo siyo yale ambayo yameamuliwa kwa uhuru na vyombo binafsi vyenyewe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tumemaliza nimetenda haki. Nafasi ni hizi na ndiyo kanuni uwiano huo jamani. Tunaendelea sasa Mheshimiwa mhitimisha hoja lazima labda Serikali ungewasikiliza kidogo tu halafu nikupe nafasi uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuelezea jambo dogo amelisema Mheshimiwa Gekul kwamba wameshuhudia hivi karibuni Serikali imefikia mahali inaelekeza vichwa vya habari vya magazeti, huu ni uongo uliokubuhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiyo Waziri mwenye dhamana hatujawahi kufanya hilo popote, kazi hiyo siyo yetu na wala hatutafanya hivyo, itakuwa

jambo la ajabu sana kwenda kuelekeza vichwa vya habari vya magazeti, mimi nadhani hili jambo tusifikie kwenye kutumia uongo *cheap like that,* ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, bado Serikali tunaamini kwamba kifungu hiki ni chema na kina manufaa. Liko jambo linajengwa hapa kujaribu kuogopesha sana watu juu ya kifungu hiki. Ukikiangalia kilivyo na kilivyoandikwa kwanza hakuna adhabu inayoambatana na kifungu hiki, haipo adhabu hatujaweka adhabu hapa. Ukiisoma maana yake ni nini, maana yake ni maelekezo ambayo Serikali inasema kwa hali ilivyo sasa hivi njia hii ni salama, ni sahihi kwa manufaa ya nchi yetu. Hatukusema hivi mtu asipofanya anafanywaje, hakuna mahali pameandikwa jambo hilo, tunapowatisha watu kwamba, sijui watafungwa, sijui watafungiwa, sijui watafanywa nini ni uongo, kutaka kufanikisha nia ovu nyuma ya hao wanaokipinga kifungu hiki, ndiyo maana hapa hakuna. Kwa hiyo, bado Serikali tunaamini kifungu hiki nia yake ni njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekeza anayoyatoa ya kutoa Serikali mbele ya kifungu, Tanzania leo kwa idadi ya magazeti niliyotaja, Tanzania leo ina *community radio* zaidi ya 145 kila mmoja aamue la kwake hii nchi itakuwa nchi ya ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya sheria ni kusaidia nchi iende kwa utaratibu. Lakini tukitaka kila mmoja aamue ndiyo yale mwalimu amefariki wengine wanapiga ndombolo. Sijui mna jambo gani limetokea wengine, mtakuwa kwenye msiba mkubwa wa Taifa wengine wanafanya sherehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kama tunaweza kuiamini Serikali tukakubali kwa mujibu wa Katiba Rais anatangaza nchi kwenda vitani leo kuiamini Serikali kuelekeza jambo la umuhimu kwa Taifa tunaona ni jambo kubwa sana, lakini tunaweza kuruhusu tukaelekezwa tukaenda vitani hapa tunataka kulipeleka wapi Taifa letu. Mimi nadhani kifungu hiki kiendelee, kifungu hiki kinafaa na tunaamini kipo kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana Mheshimiwa Nape yale maneno ambayo yalikuwa yanazungumzwa kwamba nia yako siyo nzuri na hasa kwa waandishi wa habari ndiyo unathibitisha hapa. Kulikuwa na tetesi sasa umetamka dhahiri kwamba unaenda kulazimisha *channel* ikifika saa mbili waungane na TBC waone ulivyovaa magwanda ya kijani ukipiga kidumu ndiyo unachokifanya hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nape ni Waziri wa Habari wakati tetemeko lipo kule kwa watani zangu Kagera, yeye na Naibu Spika walikuwa wanacheza ngoma kule Mbeya, kwa hiyo, ningeona hilo.

Pili; Wakati wa Uchaguzi Mkuu TBC ilikuwa inaonesha kampeni zote za CCM na inaonyesha kipande kidogo sana cha Vyama vya Upinzani na hayo kwako ndiyo maslahi mapana ya Taifa ndiyo unachokielekeza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nape haya mambo unayoyafanya na wenzako kama wanakudanganya yasipokukuta wewe utakutwa na kizazi chako, na nisingependa wale wakwe zangu wakutwe na madhambi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba kura ziamue katika jambo hili kwa sababu kama kuna malalamiko makubwa basi hujui Mheshimiwa Nape yalikuwa hapa. Hapa ndiyo siri ya shiliingi milioni kumi ulizopewa na ndiyo maana mjadala umebadilika, kwa sababu vyombo hivi vya habari kuna vile vya Serikali, vya umma wale ndiyo unaelekeza pale, hawa watu wabinafsi wanaolipa kodi kwa Tanzania kwa Serikali hii, ina mana unapokuwa unaweka hata mambo mengine ambayo hawavunji sheria, watu wanakuwa *conviced,* wanakuwa *interested* wanapata pesa, wanapata na matangazo. Wakati Mwalimu Nyerere amefariki magazeti yote hata ya udaku, *tv* zote zilionesha.

Mheshimiwa Abdul Jumbe amefariki juzi hapa Watanzania walijulishwa, haiwezekani unakuja kutambua kwamba yaani Serikali peke yake ninyi ndiyo mna akili na Watanzania wote ni wajinga hawawezi kujua jambo la msingi katika Taifa? Kwamba kuna maafa mahali watu hawawezi kuandika kweli!Tupige kura katika jambo hili ili historia iandikwe katika Bunge hili wale wapiga makofi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, endelea ukamilishe 7(iii) umeiondoa eeh!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Nimekiondoa.

**MWENYEKITI:** Haya ameiondoa *record* zionyeshe aliiondoa.

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shemeji yangu hapa kidogo alikuwa msikivu naona amezingatia kwa hiyo, hiyo imekuwa *taken by the event*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ondoa basi rasmi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kimeondolewa hicho, kwa sababu marekebisho yamezingatiwa.

*(Hapa Mhe. Mwita M. Waitara aliondoa mapendekezo yake)*

**MWENYEKITI:** Haya.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu naliondoa kwa sababu limezingatiwa katika maboresho ya Serikali. *(Makofi)*

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu nilitaka kupata tu maelezo ya Serikali kutokana na kifungu hiki cha 12(d). Hii ni *function* ya *board* ilivyoandikwa hapa kwamba *function* ya *board* itakuwa ku-*advise the government on matters pertaining to the education and training of journalist.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotegemea kwa sababu hii ni bodi na bodi yenyewe itakuwa inashughulikia masuala ya *journalist* kwa ujumla wake. Sasa hapa nataka kupata maelezo hii *board* itawezekanaje ikawa ina-*advise* Serikali kutokana na maeneo ya elimu na *training* ya *Journalist rather than* ingekuwa kwenye kifungu cha (e) ingekuwa imekuwa *covered* hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi haiwezi ikai-*advise* Serikali, kwa sababu Serikali siyo peke yake ambayo ita-*train,* lile soko ndiyo lita-*determine which kind of training* ambayo *journalist* watakuwa wanahitaji. Sasa mimi ningeona kwamba hii (e) ingekuwa tayari imeshakuwa *covered* kuliko hiki kifungu cha (d).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata maelezo ya Serikali tu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilikuwa nimetegemea angekuwa ame-*move amendments* ili tupate hasa alitaka twende wapi lakini nadhani maelezo anayoyahitaji hapa ni ya namna Bodi inavyoweza kuishauri Serikali kuhusiana na mambo ya mafunzo ya waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hapa sheria hii inaianzisha Bodi kama chombo kinachosimamia taaluma, sasa katika *process* ya kusimamia taaluma upande mmoja una Serikali ambayo ndiyo inaisimamia hiyo sera ya kutoa hizo elimu, nadhani hapa ndipo ambapo tunakutana bodi na Serikali katika kushauriana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hali tuliyonayo sasa hivi tunavyo vyuo vinavyotoa elimu ya uandishi wa habari, lakini hivi vyuo kwa kweli vingi kwanza ni vya uchochoroni vinazalisha waandishi wa habari katika ubora ambao tunadhani siyo mzuri sana. Kwa hiyo, bodi hapa tumeipa dhamana ya kuliangalia na kuishauri Serikali kuangalia namna gani tutatengeneza sera hata na sheria ambazo zitavisaidia hivi vyuo vinavyotoa hii elimu vitoe katika ubora unaotakiwa ni *venue* ya mashauriano kati ya bodi na Serikali.

**MWENYEKITI:** Nadhani alikuwa anataka maelezo maana wewe Mheshimiwa Mkuya katika hatua hii nimekuruhusu tu, lakini tuna-*deal* kama hukuleta marekebisho haya ndiyo maelezo ya Serikali turuhusu tuendelee.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18

*Ibara ziyotajwa Hapo Juu zipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20

*Ibara Iliyotajwa Hapo Juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kifungu cha 24(3) ambacho kinaonyesha viongozi wa Baraza hilo baraza huru. Wametaja pale Mwenyekiti wa Baraza, ametaja Makamu Mwenyekiti wa Baraza na Wanahabari wengine wawili watakao pendekezwa na taasisi za habari *of course* pale mwanzoni imeshazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikawa napendekeza hapa kama hili litakuwa ni Baraza Huru sikuona hapa amependekezwa Katibu wa Baraza atakuwa ni nani, napendekeza kuwepo na Katibu hapa atajwe, hata kama yupo atajwe hapa kwamba atakuwa ni viongozi wa Baraza. Kama Baraza litakuwa na chembechembe za kifedha hivi sikuona Mweka Hazina wa hili Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza mambo mawili yaingizwe moja atajwe kama Katibu wa Baraza naye miongoni mwa viongozi hapa, pili atajwe Mweka Hazina wa hili Baraza, haya ndiyo mapendekezo yangu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Maelezo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwanza hii hoja ya Katibu wa Baraza imezingatiwa kwenye kifungu cha 29 kinasema; *"There shall be a Secretary to the Council who shall be appointed by the Council through competitive recruitment,"* hii ya kwanza.

Pili Katibu hapa ana sura ya utendaji ndiyo maana hatukumpa sura ya uongozi na hawa tuliowaorodhesha hapa ni wale ambao wanachukua sura ya uongozi moja kwa moja ndiyo maana hatukuwaweka kuwa sehemu, lakini katika utekelezaji wa majukumu *obvious* Katibu hapa anakuwa katika ile *hierarchy* ya juu, isipokuwa hatukumweka hapa na ana kifungu chake maalum kinachomweleza anavyopatikana na kazi zake, nadhani kiuandishi kumweka tena huku pengine ingekuwa ni *repetition* ambayo haina sababu *as long as* ametambuliwa huku na anafahamika anavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukisoma vifungu hivi vinathibitisha nia njema ya kuunda Baraza Huru la Habari kwa sababu hata hawa viongozi wenyewe wametokana moja kwa moja na uchaguzi wao mle ndani na hata hilo sasa la maeneo mengine na ukisoma kuna vifungu vinavyoruhusu wao kuunda hata Kamati zingine. Kwa hiyo, yale tumeyaacha ndani ya wigo wao wenyewe Baraza Huru la Habari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waitara nadhani imeeleweka.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hoja imeeleweka.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya Mpya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima bila na mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye kifungu cha 32(1) ambacho sasa ni kifungu cha 35 kinasema jambo lolote kama likichapishwa, kutangazwa linaweza kuharibu sifa ya mtu yeyote kwa kumfanya achukiwe, adharauliwe au afanyiwe kejeli au linaloweza kumharibia mtu kazi yake kwa kuchafua jina lake au kumvunjia heshima yake, hayo mengine yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niliona kuna jambo muhimu sana linakosekana hapa. Amesema jambo lolote kama likichapishwa mimi nimependekeza kwamba yaingizwe maneno; jambo lolote ambalo halina ukweli likichapishwa ndiyo haya mengine yote yanaweza yakafuata yakaingizwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara nisaidie ya kiingereza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Eehh?

**MWENYEKITI:** Nisaidie muswada huu wa kiingereza kwenye eneo hilo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema lakini si lugha zote zinaruhusiwa au?

**MWENYEKITI:** Lakini hapa tunatunga hii *version* ya kiingereza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Aahh sawa, kwa hiyo, namba 32(1) anasema; *"Any matter which, if published, is likely to injure the reputation of any person by exposing him to hatred, contempt or ridicule."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa nimependekeza yaingie yafuatayo:-

**MWENYEKITI:** Mnacheka nini? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napendekeza; "*a published matter shall be conceived as a defamatory matter if it contains false information which is likely to injure or demage the reputation of any person in his profession or trade,*" hayo ndiyo mapendekezo.

**MWENYEKITI:** *Okay, AG* umeipata? Mheshimiwa Waitara anadhani yalivyokaa sasa anapendekeza *language* hiyo*; a published matter shall be conceived as a defamatory matter if it contains false information which is likely to injure or damage the reputation of any person in his profession or trade*.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeiona hoja ya shemeji yangu Waitara na hasa baada ya kurudi kwenye kiingereza. Lakini tafsiri iliyoko hapa ni tafsiri *standard* ya neno lililotumika. Sasa kubadilisha tafsiri ambayo kwa kweli ni *universal* nadhani ni kujaribu kuipa maana nyingine ambayo inaweza ikatupeleka mahali ambako siyo sahihi.

Kwa hiyo, tafsiri iliyotumika hapa ni tafsiri ambayo inatumika duniani kote, ni *standard* tafsiri ya neno *defamation*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli, naomba nitoe hoja ili jambo hili lijadiliwe tupate maoni na michango ya Wabunge wengine.

**MWENYEKITI:** Haya, toa hoja.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Naomba nitoe hoja na naomba niungwe mkono.

**MWENYEKITI:** Waziri Kivuli humuungi mkono Mheshimiwa Waitara?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Hiyo yote nimetoa hoja naomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono tujadili jambo hili kwa mapana.

**MWENYEKITI:** Haya tuanze. Mheshimiwa Mnyika

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ukikisoma kifungu; "*Any matter which, if published, is likely to injure the reputation of any person by exposing him to hatred, contempt or ridicule or likely to damage any person in his profession or trade by an injury to his reputation, is a defamatory matter.*" Imeweka mambo ambayo kimsingi mtu anaathirika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Waitara ambayo ninaiunga mkono ni kwamba *what if* jambo ni la kweli? Kwa mfano, Waziri wa Serikali ameiba pesa, amefanya ufisadi mkubwa, halafu chombo cha habari kimeandika kwamba amefanya ufisadi mkubwa, kwa vyovyote vile hiyo habari itakuwa imemharibia jina lake, imemuumiza, amepata maumivu na mambo mengine kama hayo, lakini jambo lililoandikwa ni la kweli.

Katika mazingira ya kifungu kilivyo hivi sasa inaweza kutoa mianya kwa wakati ambapo mtu ambae amefanya jambo ambalo ni la kweli kabisa akaenda mahakamani bado akadai fidia kutokana na habari ambayo imeandikwa na chombo cha habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili jambo hili lisitokee ni vema mapendekezo ya Mheshimiwa Waitara yakachukuliwa ili yale ambayo yanahusu *defamation* yawe ni taarifa za uwongo peke yake, taarifa za ukweli kwa namna yoyote zisiingie katika mlango wa mahakama kwenye masuala ya *defamation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono jambo hilo liweze kukubaliwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kifungu hiki na ukisikiliza hoja ya Mheshimiwa Waitara na ukimsikiliza Waziri unaona kwamba kuna mapungufu katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kwamba jambo lolote liwe kashfa ambapo mtu yeye anaona kwamba hiyo ni kashfa siyo jambo sahihi. Waziri mwenyewe ni shahidi. Ulikuwepo mkataba mmoja ambao Waziri alifanya mkutano na waandishi wa habari akasema mkataba huu umefungwa akiwa katika mchakato, akiwa kiongozi tu kwenye chama chake, akasema mkataba huu ulifungwa katika mazingira ya rushwa, ulifungwa katika mazingira ya utapeli, akaupinga kweli kwenye mkutano na waandishi wa habari. Vyombo vya habari vikaandika. Mmoja wa aliyetuhumiwa akafanya na yeye mkutano na waandishi wa habari akasema hili jambo nimezushiwa, ni jambo la uongo, wamenikashifu, naenda mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lile jambo lilikuwa la kweli na yule mtu hakwenda mahakamani akaishia njiani. Sasa tusiamue kwamba jambo tu lolote lile liwe ni jambo la kashfa, ni lazima jambo hilo likathibitishwe mtu huyo aende Mahakamani na liwe jambo la uwongo, lisiwe tu moja kwa moja kama hivi ilivyowekwa kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waitara.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Tizeba.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa kinachozungumzwa zaidi ni uandishi wenyewe wa sheria, kwa sababu katika hiki kifungu neno *defamation* lenyewe linayo tafsiri ambayo kama yale *content* siyo ya kweli ndiyo unaingia kwenye hatia yenyewe lakini kama *content* ni ya kweli neno *defamation* haliwezi ku-*apply* hapa; kwa hiyo, hatuoni sababu, *otherwise* tutakuwa tunarudia *definition in every clause* humu kujaribu kutengeneza picha ambayo sijui ni ya namna gani, huu ni uandishi tu wa sheria kwamba neno ambalo lina *definition* huna haja ya kuendelea kulitolea *definition in every other sentence* unayoandika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kutafuta uhalisia wa haya maneno wakati huo tukizingatia kwamba lugha zenyewe zimekuja na meli tutapata shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli upo tu kwamba kifungu kama kilivyoandikwa kwenye mapendekezo haya ya Serikali kipo sahihi tu kwa sababu kama mtu atakuwa ameandika taarifa kwenye gazeti lake na taarifa hizo zikawa ni za kweli na mtu akaenda akalalamika mahakamani, akafungua mashitaka ya *defamation*, mahakama ikaanza kusikiliza hilo shauri, mahakama itaamua kwamba hizi taarifa alizoandika huyu mtu ni za kweli ama siyo za kweli, kama ikiona taarifa hizo ni za kweli mahakama itatupilia mbali shitaka la mtu ambae ameshtaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wa Mheshimiwa Waitara kwamba lazima tuweke hapa, mtu akiandika taarifa zikawa ni za kweli basi hakuna maana ya kuweka hiki kifungu hapa, kwa hiyo, tuache mambo ya tafsiri ya sheria na hivi vifungu yakafanyike mahakamani sisi kazi yetu ni kutunga sheria na mapendekezo haya ya Serikali yanajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kusema tunavyotafsiri sheria za Tanzania tunakumbushwa pia *through the Judicature and Application of Laws Act,* kwamba tutafsiri sheria hizi kwa kutumia *common law, doctrines of equity and*

*statutes of general application and satatutes of general application.* Huko kwenye *common laws* ndiyo ilitokea *concept* ya *defamation* ambayo yenyewe tu kama kitu ni cha kweli siyo *defamation.* Turudi kwenye kifungu 34 ambacho sasa nafikiri ni 37, hayo yaliyosemwa huko yamerekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie tu hapa, tutofautishe; *the subject matter of defamation which is defamatory matter and concept of defamation itself,* kwa hiyo, *as it is* hiki kifungu kibaki kwa sababu kiko *cured* na kifungu cha 34 ambacho sasa kimehamia 37. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri sasa kama una ya ziada.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini wenzetu wametuelewa, kama hawajatuelewa hata ukienda kifungu cha 35 bado kinazungumzia hizo *defamatory matters* zikoje, zinafanyikaje. Kwa hiyo, wasisome tu kifungu kimoja wakaishia hapo wakataka tafsiri hapo hapo. Ukienda mbele kule imeleeleza vizuri sana na wenzangu wamejitahidi wamelieleza vizuri, nadhani wametuelewa na msimamo wa Serikali kwamba kifungu hicho kibaki kama kilivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kura ziamue.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nawahoji sasa. Hapana jamani tuvumuliane tu hajachoka.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 36

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili..

**MWENYEKITI:** Umeiona?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili eneo lilizingatiwa kwenye marekebisho ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 37

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utata uliokuwepo umeondoka. Tumekiondoa.

*(Hapa Mhe. Mwita M. Waitara aliondoa mapendekezo yake)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kifungu hicho kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38
Ibara ya 39

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu cha 37(1) na chenyewe kinasema mtu atakayetangaza jambo linalodhaniwa ni la kashfa kwa mtu mwingine anaweza, kama atadai kuwa jambo hili alitangaza kwa nia safi kuhusu mtu huyo. Shida yangu ipo kwenye maneno hapa linalodhaniwa. Nikaona kama limekaa kimtego sana maana yake huyu aliyeandikwa au Serikali au Waziri ndiyo anaweza akasema anadhani namna gani. Kwa hiyo, nikasema maneno haya yawe na lugha ambayo inaonesha jambo ambalo lina uhakika badala ya kudhani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kwenye kiingereza utakuta unatumia maneno *you claim or you alleged* hebu twende kwenye ile ya kiingereza tusaidiane ili uisome mwenyewe tu. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo inasema; "*a person who publishes words alleged to be defamatory of another person may, if he claims that the words were published by him innocently in relation to that other person, make an offer of amends and in that case where-*

**MWENYEKITI:** Umeiona *thrust?* Mheshimiwa Waitara maana muda...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri suala hapa ilikuwa ni tafsiri, kwa hiyo, nakiondoa.

*(Hapa Mhe. Mwita M. Waitara aliondoa mapendekezo yake)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara wasilisho.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwa ujumla wake. Marekebisho mengine yote ambayo yanafuata nilipinga kwa sababu hakuna tafsiri ya neno uchochezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote ukisoma hata yatakayofuata baadae ilikuwa inataka tafsiri, kwa sababu hapa inazungumza makosa mbalimbali lakini inasema uchochezi, uchochezi, uchochezi, sasa kama nitapata maelezo mazuri ya jumla pia ya neno uchochezi kama ina tafsiri sahihi maana yake naweza nikaondoa vifungu vyote vinavyobaki kwa sababu, lengo lilikuwa ni hilo kwamba nani anatafsiri neno uchochezi ili liwe kosa.

**MWENYEKITI:** *Seditious intention* nani anatafsiri? *AG,* msaidieni, mimi ni Mwenyekiti naongoza kikao, lakini ni chepesi sana kumjibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waitara atuelewe tu kwamba kweli tuna sheria mbalimbali zinazoanzishwa makosa ya jinai, lakini baadhi ya *origin* ya sheria hizo ni kwa wenzetu wa *common law* na hapo ndiyo *seditious intention* ilipotoka. Kwa hiyo, inaweza isiwe hapa lakini kwa kutumia *common law* tunapata hiyo *meaning* ya *seditious intention. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante!

Mheshimiwa Waitara, ndiyo historia. *Jurisprudence* ya Tanzania huwezi kuiangalia tu kwenye muswada, lazima usome na sheria nyingine ambazo zitakusaidia. Mimi nakushukuru kwa *attempt* yako maana anayeuliza ana kiu ya kufahamu. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yake ni mazuri, lakini hoja yangu ni kwamba hapa katika haya maneno ya kwenye kitabu cha hii sheria, hiyo tafsiri haiwezi kuwekwa mahali popote hapo? Ndiyo ilikuwa hoja yangu kubwa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge akienda ukurasa wa 20 kipengele cha 49 cha kiingereza pembeni pana maneno *seditious intention,* 49(1) inasema; "*A seditious intention is an intention to:* halafu ina (a), (b), (c), (d), (e). Kwa hiyo, tafsiri hii hapa imepatikana. Shemeji yangu nadhani amenielewa. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo, nadhani vifungu vyote kama nilivyosema mwanzoni vinavyofuata itabidi niviondoe kwa sababu hoja ilikuwa imejengwa katika msingi huo. *(Makofi)*

*(Hapa Mhe. Mwita M. Waitara aliondoa mapendekezo yake)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa mwenyekiti, jambo la mwisho ninataka niulize hapa, maana wakati najiandaa mimi nili-*deal* sana na hilo upande wa kiswahili, sasa unakuta unachukua muda ku-*link* hivi vitu viwili, unajua tafsiri ya kiingereza na kiswahili tofauti. Kuna watu walikuwa wanapiga makofi hapa hawaelewi hoja ilikuwa ni nini.

**MWENYEKITI:** Wameelewa sana.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize katika mijadala hapa ni lugha gani hasa ambayo inaongoza mjadala ili mtu aweze kujikita katika eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Unaruhusiwa kutumia zote, lakini kwa vile humo kwenye Kamati ya Bunge zima tunatumia *version* ya kiingereza ndiyo maana tunahojiwa kwa namna hiyo. Ile Serikali wanatusaidia muswada huu unatafsiriwa kwa kiswahili, wananchi na wenyewe waelewe vizuri. Lakini tunapoingia humu sasa hata *schedule of amendments* unayoleta wewe umeileta katika lugha ya malkia, ndiyo nzuri! Kwa hiyo, ndiyo tunaenda kwa mtiririko huo. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 51
Ibara ya 52

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 53

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 54

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufanya marekebisho pale kwenye hiyo Ibara Mpya ya 54. Imeandikwa; *A person shall not be convicted of any seditious offence,* sasa *that was serious omission* yaani *oversight*. Lengo letu lilikuwa ni kwamba *shall not be prosecuted for any seditious offence*. Kwa hiyo, tunakirekebisha kwa kuondoa maneno *convicted of,* na badala yake kuweka maneno *prosecuted for.* Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Hilo unalisema ni kwa sababu unataka makosa haya, tofauti na jinsi muswada ulivyokuwa umechapishwa yapate sasa idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*
*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 55
Ibara ya 56

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 60

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara Mpya ya 64

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 65

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 66
Ibara ya 67

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la Muswada

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. LINAH KITOSI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waziri Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria wa Huduma za Habari wa mwaka 2016 Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Huduma za Habari wa mwaka 2016, kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa natamka rasmi kwamba Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa mwaka 2016 *(The Media Services Bill, 2016)* sasa umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana kwa kazi nzuri mliyofanya tangu jana, muswada huu ulipowasilishwa. Kwa michango yenu mizuri, lakini kubwa zaidi ni katika kazi ambayo mmemaliza sasa hivi ya kupitia vifungu vya muswada huu, siyo kazi nyepesi lakini tumeimaliza kwa ufanisi mkubwa.

Waheshimiwa Wabunge, ombi langu pamoja na wengine ambao tulijaribu kutumia kanuni tuendelee na utaratibu huo, lakini tukiwa tunawahi kuwasilisha marekebisho ndiyo tunarutubisha miswada, tusifanye hii kazi ya kuviziana, haina tija.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache, kwa hiyo niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yako ya wataalam Wizarani hapo, nimshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na timu yake, naelewa jana hawakulala hawa mimi najua, nimepitia huko. Lakini kwa kazi hii, inapoletwa hivi

*schedule* unadhani ni nyepesi sana, lakini naelewa *what it takes*. Hongera sana endeleeni na kazi hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ester Bulaya anasema amedondosha hereni yake tena ya dhahabu nzito, kwa hiyo, kama kuna mtu ameiona jamani kwa heshima zetu mjue ni ya mwenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la wageni, sijui kama bado wako. Wageni wa Mhesimiwa Immaculate Sware Semesi ambao ni wafanyakazi wa Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira *(WWF)* kutoka Mkoa wa Dar es Salaam wakiongozwa na Meneja Mradi wa Mazingira ya Baharini kutoka shirika hilo Mheshimiwa Mathias Kigulu, sijui kama bado wapo, sidhani! Hata hivyo karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la semina; kesho mnakumbushwa kwamba kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano wa Kiuchumi kati ya nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya *(Economic Partnership Agreement)* katika ukumbi wa Bunge, humu kesho saa tano asubuhi, tuwahi maana kuna kitu kitakuja wiki ijayo kwenye suala hilo.

Tangazo la kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Hesabu za Serikali za Mitaa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba tarehe 5 Novemba saa saba mchana mara baada ya kikao cha leo kuahirishwa kutakuwa na kikao cha Kamati kwa ajili ya kupitia taarifa za mwaka ya Kamati kwa kipindi kinachohusu ukaguzi uliofanyika kwa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 na mwaka 2014/2015, mnaombwa mfike kwenye ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa *APNAC* Tanzania, Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati Kuu ya *APNAC* kuwa leo Jumamosi tarehe 5 Novemba, saa nane mchana katika Ukumbi wa Msekwa B kutakuwa na kikao cha semina kwa Wajumbe wa Kamati Kuu. Hayo ndiyo matangazo niliyoletewa hapa mezani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo na shukrani nilizowapatia, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 8.35 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 7 Novemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*